**22 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 22 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tisa, Kikao cha Thelathini, leo tarehe 22 Mei, 2025.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Katibu tuendelee.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 378

### Mkakati wa Kuwalinda Wanafunzi Shuleni

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuwalinda Wanafunzi Shuleni?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa wanafunzi ni kipaumbele cha Serikali ambapo mikakati mbalimbali imekuwa ikitekelezwa ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanakuwa katika mazingira salama shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mikakati inayotumika kuwalinda wanafunzi ni pamoja na kampeni za kupinga ukatili wa kijinsia kuanzia nyumbani, njiani na shuleni kwa kushirikisha vyombo vya ulinzi na usalama; mafunzo kuhusu shule salama kwa wadau muhimu wa ulinzi na usalama wa wanafunzi, ambapo mwaka wa fedha 2024/2025 yameendeshwa mafunzo kwa Walimu 7,451 wa ushauri na unasihi, Wakuu wa Shule za Msingi 17,817, Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya kata 900, Wenyeviti wa Kamati za Shule 1,980 na Wenyeviti wa Bodi za Shule 580.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati mingine ni kuanzisha Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto. Aidha, katika ngazi za vijiji na mitaa yameanzishwa mabaraza ya watoto yanayojumuisha

wanafunzi wa msingi na sekondari na watoto waliopo kwenye mfumo usio rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kufanya tathmini ya kina kuhusu changamoto zinazowakabili wanafunzi shuleni, njiani na nyumbani ili kuboresha mikakati ya kuzitatua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUwAKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwanza ninaipongeza Serikali kwa jitihada mbalimbali ambazo wanazichukua. Hata hivyo, nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kumekuwa na changamoto hasa kwa wanafunzi wetu wa msingi ambao wanapanda kwenye *school bus.* Unaweza ukakuta mwanafunzi anaweza kufika mwaka mzima hajawahi kukaa kwenye *seat*. Je, Serikali hawaoni kuwa sasa kuna haja ya kuandaa au kutoa kauli maalum kwa skuli zetu ambazo zinatumia *school bus* ili kuona sasa kuwa wanaweza kuwasaidia kwa kuweka *matron* na *patron* katika *school bus?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; pamoja na jitihada hizo zinazochukuliwa bado mmomonyoko wa maadili umeendelea kuwa changamoto katika skuli zetu. Je, Serikali haioni sasa kuweka nguvu maalum kwa kuwaandaa walimu maalum wa maadili katika skuli zetu nchi nzima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mbunge wa Vijana Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali kwa swali lake ambalo linalenga kuendelea kutengeneza mazingira salama zaidi kwa ajili ya wananfunzi wetu na hasa kipindi wanapokuwa wanaelekea shuleni, vilevile hata wanapokuwa nyumbani, kwa kuwa usalama wa wanafunzi ni kuanzia nyumbani, njiani hadi shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza, tayari Serikali imekwishaweka utaratibu mzuri na maelekezo yalikwishatoka, kwamba kuwe kuna *patron* na *matron* kwenye mabasi yanayowapeleka watoto shuleni. Yote hiyo ni njia mojawapo ya kuhakikisha watoto wetu wanakuwa katika mazingira ya usalama kuanzia nyumbani, wanapokuwa njiani na pia wanapokuwa shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili linalohusu walimu maalum kabisa wa maadili; kama nilivyotangulia kujibu kwenye jibu la msingi, Serikali inaendelea kuongeza mafunzo kwa wadau muhimu ikiwemo walimu. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 yameendeshwa mafunzo kwa walimu 7,451 kwa ajili ya ushauri na unasihi; Wakuu wa Shule za Msingi 17,817; Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya kata 900; Wenyeviti wa Kamati za Shule 1,980; na Wenyeviti wa Bodi za Shule 580.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, si tu walimu wanaoandaliwa kwa ajili ya kusimamia maadili na usalama wa wanafunzi wanapokuwepo mashuleni bali pia kuna wadau wengine ambao nao wanajengewa uwezo ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanakuwa salama.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Mtaturu.

Na. 379

**Wahitimu wa Diploma Kutoajiriwa Kuwa Watendaji wa Vijiji**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU K.n.y. MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali haiwaajiri wahitimu wenye *diploma* kuwa Watendaji wa Vijiji?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ajira za watendaji wa vijiji katika utumishi wa umma hufanyika kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika Muundo wa Utumishi wa Kada za Watendaji wa Vijiji/Mitaa uliotolewa na Serikali kupitia Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na.1 wa Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, muundo huo umeainisha watendaji wa vijiji/mtaa wanaoajiriwa katika utumishi wa umma wanatakiwa kuwa na kiwango cha elimu ya kidato cha nne au sita waliohitimu mafunzo ya Astashahada *(Certificate)* katika moja ya fani zifuatazo; utawala, sheria, elimu ya jamii, usimamizi wa fedha, maendeleo ya jamii na sayansi ya sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo) au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na masharti hayo, wahitimu wa mafunzo ya Stashahada *(Diploma)* katika fani tajwa hawawezi kuajiriwa kwenye utumishi wa umma katika nafasi ya mtendaji wa kijiji/mtaa kwa kuwa sifa hiyo haijatajwa katika muundo husika. Hata hivyo, wahitimu wenye sifa hizo wanaweza kuajiriwa katika utumishi wa umma katika kada nyingine zinazotaja sifa hiyo kama sifa ya kuajiriwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni taaluma zipi ambazo wanaweza kuajiriwa ili nao waweze kupata haki ya kuajiriwa baada ya kuwa wamepata mafunzo mbalimbali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ninataka nijue; tumekuwa na upungufu wa watendaji katika vijiji na kata na tumekuwa tukichukua muda mrefu sana kujaza nafasi hizi na imeathiri sana utendaji wa Serikali kwenye maeneo yetu. Je,

Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kuhakikisha kwamba nafasi hizo zinajazwa na kuondoa *gaps* ambazo zipo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu kwenye majibu ya msingi, kwamba ajira za watendaji wa vijiji na mitaa zimeainishwa kwa mujibu wa Mwongozo wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2013; na kwamba wenye sifa hizo ni wale waaliohitimu kidato cha nne au kidato cha sita na kupata *certificate* katika maeneo ya utawala, sheria, elimu ya jamii, usimamizi wa fedha, maendeleo ya jamii, sayansi ya sanaa kutoka Chuo cha Hombolo au chuo kingine chochote ambacho kinatambuliwa na Serikali. Kwa hiyo, hawa ndiyo wenye sifa za kuajiriwa kama watendaji wa vijiji au mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wenye diploma wana nafasi kwa maana ya sifa katika ajira/nafasi nyingine, lakini si watendaji wa vijiji au mitaa. Wameendelea kuajiriwa katika nafasi mbalimbali kwa nafasi hiyo ya diploma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kuhusiana na watendaji wa vijiji; ni kweli kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya maeneo; kwamba kuna vijiji vinakosa watendaji wa vijiji. Hata hivyo, Serikali imeendelea kufanya tathmini mara kwa mara na kutambua vijiji ambavyo havina watendaji na kuendelea kuwaajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ambao unapita unatokana na taratibu zile za ajira ambazo zinachukua muda kidogo. Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba kila mahali ambapo tunakuwa hatuna mtendaji wa kijiji au mtaa, basi anapatikana mapema kwa ajili ya kujaza nafasi hiyo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, aulize swali lake.

Na. 380

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Mpalinga – Bahi**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza:-

Je, lini Serikali Itaanza Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mpalinga – Bahi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga fedha ya nyongeza shilingi bilioni 53.5 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye kata 214 za kimkakati. Awamu ya kwanza inaanza na ujenzi wa vituo 120 ambapo shilingi bilioni 30 zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Bahi shilingi milioni 250 zitapelekwa awamu ya pili katika Kata ya Mtitaa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD),* choo cha nje, kichomea taka na shimo la kutupia kondo la nyuma.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati kote nchini ikiwemo Kata ya Mpalinga katika Halmashauri ya Bahi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Serikali kwa dhati kwa namna ambavyo imeweza kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mtitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Serikali imejenga Kituo cha Afya Babayu, lakini

hadi sasa zile huduma za kituo cha afya hazijaanza kutolewa, hususani upasuaji, je, ni lini zitaanza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni kwamba, Serikali ilianza ujenzi wa Kituo cha Afya pale Kata ya Chifutuka na kilishakamilika lakini jengo la *OPD* halikujengwa. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Chifutuka kwenye *OPD* ili wananchi waanze kupata huduma kamilifu?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Ernest Kenneth Nollo, kwa namna ambavyo ameendelea kuwasemea na kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Bahi. Vilevile ninafahamu kwamba anafuatilia sana kuhusiana na kukiwezesha Kituo cha Afya cha Babayu kuanza kutoa huduma. Mimi na yeye tulifanya ziara katika kituo kile cha afya na tuliona majengo yakiwa hatua za mwisho za ukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa jengo la upasuaji la Kituo cha Afya cha Babayu limekamilika, lakini taratibu za kuanza huduma ya upasuaji ziko mwishoni. Ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bahi; kwa sababu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alikwishapeleka fedha, milioni 500 na majengo yamejengwa likiwepo jengo la upasuaji na limeshakamilika. Vilevile, Mheshimiwa Rais amepeleka fedha za vifaa tiba vyote kwa ajili ya upasuaji. Kwa hiyo ninaomba nitoe maelekezo haya kwa mkurugenzi kwamba tunawapa mwezi mmoja. Ifikapo tarehe 30 Juni jengo la upasuaji katika kituo hiki cha afya lianze kutoa huduma za upasuaji kwa wananchi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka, nimekuona.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Kituo cha Afya cha Ngongoele kilipata fedha

milioni 250 zile za matokeo makubwa sasa, mradi ambao ulishakwisha. Je, Serikali ina mpango upi wa kutupatia fedha, milioni 200 nyingine ili kukamilisha kituo kile?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kujenga vituo vya afya na kuvikamilisha kwa awamu. Tunafahamu kwamba Kituo cha afya cha Ngongoele katika Jimbo la Liwale bado hakijakamilika. Serikali ilikwishapeleka fedha kwa awamu ya kwanza. Nimhakikishie kwamba tutaendelea na awamu ya pili, ambapo tutapeleka fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kituo hicho kinajengwa na kukamilika ili kianze kutoa huduma kwa wananchi ambazo zina ngazi ya kituo cha afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa Kituo cha Afya Mafisa katika Manispaa ya Morogoro? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Mafisa katika Manispaa ya Morogoro ni moja ya vituo vya afya ambavyo vina upungufu wa majengo. Tayari Serikali ilikwishaainisha majengo yanayopungua na tumekwishaweka kwenye mpango wa bajeti kupitia Mfuko wa Benki ya Dunia. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, fedha zitapelekwa kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo hicho cha afya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Rose Vincent Busiga, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 381

**Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Afya Runzewe Mashariki - Bukombe**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA K.n.y. MHE. ROSE V. BUSIGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za kukamilisha ujenzi wa wodi ya mama na mtoto katika Kituo cha Afya Runzewe Mashariki – Bukombe?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE**) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Bukombe imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Msonga kilichopo Kata ya Runzewe Mashariki. Mpaka sasa jumla ya shilingi milioni 413.08 zimepelekwa na kutekeleza ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD),* jengo la maabara na jengo la kliniki ya mama, baba na mtoto *(RCH)*. Majengo yote yamekamilika na yanatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe imetoa shilingi milioni 164.05 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wazazi *(maternity)* na jengo la upasuaji. Ujenzi wa majengo haya umefikia 85%. Aidha, katika mwaka 2025/2026 Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri imetenga shilingi milioni 80 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kufulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa wa miundombinu ya msingi ikiwemo wodi ya mama na mtoto katika Kituo cha Afya Msonga katika Kata ya Runzewe Mashariki Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Halmashauri ya Mbongwe imetoa fedha za mapato ya ndani shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Nyakafuru (Jengo la *OPD*). Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo katika Kituo hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Nhomolwa Mbongwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Halmashauri ya Mbongwe kwa kutimiza wajibu wake wa kutenga fedha hiyo shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Afya ambacho Mheshimiwa Mbunge Dkt. Christina, amekitaja. Nimhakikishie kwamba Serikali kwa kutumia mapato ya ndani na kupitia fedha za Serikali Kuu, tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba majengo yote katika Kituo hicho cha afya yanakamilika; na tutahakikisha kwamba kituo hicho kinaanza kutoa huduma mapema iwezekanavyo kwa masilahi ya wananchi katika eneo hilo.

Mheshimia Mwenyekiti, kwa swali la pili, kuhusiana na Kituo cha Afya ambacho tayari kimeorodheshwa kwenye idadi ya vituo vya afya vya kimkakati kwa kila jimbo; nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali inaendelea na taratibu za kutenga bajeti kwa ajili ya kwenda kujenga kituo hicho cha afya cha kimkakati katika kata ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Kungu, nimekuona.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Namiungo kulikuwa kuna ahadi ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ya kujenga Kituo cha Afya katika Kata ile ya Namiungo. Vilevile, baada ya kuona mchakato ule ni mrefu sana na ahadi ile haikamilishwi, baada ya kuletewa fomu humu ndani za sisi Wabunge kujaza vituo vya kimkakati, nilijaza fomu ile kwa kuelekeza kituo kile kikajengwe Kata ya Namiungo ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais. Sasa ninataka kufahamu; je, ni lini pesa zile zitakwenda kwa ajili ya ujenzi wa Kituo kile cha Afya katika Kata ya Namiungo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na utekelezaji wa ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Namiungo. Pia, tayari sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tulishakiweka kituo hicho kwenye Kata za Kimkakati na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge mwenyewe alianisha kata hiyo kama kata ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amekwishatenga fedha shilingi bilioni 53.5 kwa ajili ya majimbo yote 214; na tayari hivi sasa fedha zimekwishaanza kupelekwa kwenye majimbo yote 120, jumla ya shilingi bilioni 30. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo hicho cha afya kitapata fedha wakati wowote mwaka huu, kwa sababu fedha zimeshaanza kupelekwa kwenye halmashauri zetu.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange pamoja na Mheshimiwa Zainab Katimba kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Tunaendelea na Wizara ya Maji; Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, aulize swali lake.

Na. 382

**Kuchimba Visima vya Maji kwenye Taasisi za Umma**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, Serikali haioni ni muda muafaka kuchimba visima vya maji kwenye Taasisi za Umma kama shule, zahanati na hospitali zote nchini?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza inapatikana katika maeneo yote ikiwemo taasisi za umma kama vile shule na vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Serikali huzingatia uwepo wa taasisi hizo wakati wa usanifu wa miradi ya maji na hivyo kuhakikisha mahitaji yake yanajumuishwa. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali kupitia miradi mbalimbali iliyotekelezwa imefikisha huduma ya maji safi na salama kwa taasisi za umma 31,130 ambapo kati ya hizo, shule za msingi na sekondari ni 25,820 wakati Vituo vya kutolea huduma za afya ni 5,310.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuzingatia mahitaji ya maji kwa taasisi zote za umma nchini kupitia miradi inayoendelea na inayotarajiwa kujengwa pamoja na kufikisha huduma ya maji kadri itakavyohitajika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri yanayoleta faraja ya upatikanaji wa maji kwenye hizi huduma, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza; sote tunafahamu kwamba utunzaji wa mazingira ya maeneo ya shule

yanahitaji maji mengi na tunafahamu kwamba maji mengi ambayo yanatumika walimu wanashindwa kuwaruhusu watoto kuyatumia vizuri kutokana na gharama kubwa ya ulipaji wa maji hayo. Je, ni kwa nini sasa Serikali kutokana na uwepo wa mitambo ya uchimbaji wa visima isichimbe visima kwenye taasisi hizo ili kupunguza gharama za ulipaji wa bili kwenye taasisi zinazotoa maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; utoaji wa elimu pia unatolewa na sekta zisizo za Kiserikali, kwa mfano kuna shule za binafsi na wao pia ni sehemu kubwa ya wanaosaidia upatikanaji wa elimu nchini na shule zao pia zina changamoto au zahanati zao zina changamoto ya huduma ya maji. Je, Serikali inaweza ikafanya mawasiliano na wawekezaji hao ili kuwasaidia kutumia mitambo ya Serikali kuweza kupata huduma ya maji kwa urahisi kwa sababu wanatoa huduma kwa wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya kwa niaba ya wananchi wake wa Kibaha Vijijini. Kwenye swali la pili, Serikali iko tayari kufanya kazi na wadau wote ambao wana nia njema kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaboresha utoaji wa huduma ya maji nchini ikiwemo katika taasisi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa swali la kwanza, ni kweli kabisa gharama ya kuhudumia na hizi fedha ambazo wanazipata shuleni inawezekana hazitoshi kuhudumia gharama ya kulipa maji endapo wanafikishiwa zile bili. Sisi kama Serikali tumeshaliona hilo lakini pia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tunaendelea kuangalia njia bora zaidi ya kutatua changamoto hii kwa sababu kuna maerneo mengine ya shuleni hata kama tuna mitambo ya kuchimbia visima maeneo hayo katika maeneo husika hakuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba ni lazima tuchimbe maeneo mengine halafu yasukumwe yapelekwe pale. Yakishapelekwa katika eneo husika maana yake kuna gharama za umeme ambazo zitakuwa zimetumika ambapo kwa namna moja au nyingine uchangiaji tu lazima utakuwepo. Hata hivyo, kwa maeno ambayo hakuna changamoto ya upatikanaji wa maji Serikali imeendelea kutumia mitambo ya Mheshimiwa Rais ambapo alinunua mitambo 25 kuhakikisha kwamba tunaendelea kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji katika taasisi za umma, shule pamoja na vituo vya afya. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Robert Maboto na Mheshimiwa Cecilia Paresso nimewaona.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Bunda Mjini, Kata ya Wariku Mradi wa Maji uko 40%. Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili mradi huu uweze kukamilishwa uweze kutatua tatizo la changamoto za maji katika kata hiyo? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Maboto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshawasiliana na Mheshimiwa Mbunge na jana tuliongelea kuhusu hili suala na kuna *MD* wetu kutoka kule Bunda pia ameliongelea. Ni kweli kabisa kulikuwa na changamoto ya fedha zilikuwa hazijafika, lakini tayari tumeshawasilisha hati ya madai Wizara ya Fedha ili waweze kulipwa na tayari mchakato uko katika hatua nzuri kabisa na mradi huu ni mradi wa kimkakati katika eneo hilo la Bunda na katika kata ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja na amekuwa akiongelea sana kuhusu hili suala na sisi tumejizatiti kwenda kutatua ili mradi huu ukamilike na wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Kata ya Mbulumbulu Serikali iliahidi kuchimba visima vinne vya maji, lakini mpaka sasa tunapoongea ni angalau kijiji kimoja tu wameanza kuchimba. Vijiji vingine vyote zoezi hilo haliendelei. Nini kauli ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, pia ninamshukuru Dada yangu, Mheshimiwa Paresso kwa kuendelea kuwasemea wananchi wa Karatu na hakika kweli tunaelewa kwamba dhamira ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na falsafa ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani ninamwona Mheshimiwa Mbunge pia anaendelea kuiishi kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali, kwenye sekta ya maji tunatambua kabisa kwamba katika programu ya visima 900 kuna maeneo ambapo tulikumbana na changamoto ya kutokupatikana kwa maji, lakini tumekuwa tukitafuta njia mbadala badala ya kuchimba kisima tunaweza tukatafuta mradi ulioko karibu tunafanya usanifu, tunaangalia namna ya kuyafikisha maji katika vijiji husika ambavyo havijapata maji chini ya ardhi. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge vijiji hivyo tutavizingatia, lengo ni kwamba wapate huduma ya majisafi na salama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninasimama kwa mara ya saba nikiuliza kuhusu Mradi wa Mfumbi kwa maana ya Usalimwani Mfumbi zaidi ya shule tano za msingi na sekondari ziko pale na hazina maji. Vijiji vitano havina maji na mradi huu walianza kujenga lakini umesimama hadi dakika hii. Ipi kauli ya Wizara kwenye hili suala ili iweze kutoa fedha mradi ukatekelezwe?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa kaka yangu Sanga, Mbunge mahiri kabisa kutoka Makete pale. Nimhakikishie kwa namna ambavyo amesimama kwa mara ya saba kwa msisitizo huo huo ninaomba nikitoka hapa niende nikalifanyie kazi kwa uzito stahiki kwa ajili ya wananchi wake wa Makete kwa sababu lengo la Serikali siyo kukwamisha miradi, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba miradi yote inakamilika na iweze kutoa matokeo yaliyotarajiwa. Kama Mbunge alivyowasilisha sisi tunachukua kwa namna hiyo. Baada ya hapo nitampa mrejesho kwa niaba ya wananchi wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namtumbo tuna Mradi wa Kumbara – Litola, mradi mkubwa ambao sasa umefanikiwa na maji yanatoka na umedhihirisha una maji mengi sana mradi huo, lakini tuna Kata jirani ya Namabengo ambayo ina shule ya kutoka kidato cha kwanza mpaka cha sita ambapo pia kuna shida sana ya maji. Iko kilometa sita kutoka mwisho wa mradi huo. Je, Serikali inaweza ikafanya usanifu na ikajenga tenki kubwa na kutandaza mabomba ikapeleka katika Kata hiyo ya Namabengo ili waweze kupata maji ambayo wana shida ya maji pia eneo hilo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni habari njema sana. Tunapokuwa na chanzo cha uhakika na tunakuwa na kiu ya kutosha ya maji, sisi kama Serikali ni kuhakikisha kwamba maeneo husika yanayozunguka hicho chanzo cha maji wanapata maji ya uhakika. Serikali iko tayari kufanya usanifu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri ili kata jirani waweze kupata huduma hiyo ambayo ni msingi wa uhai wa binadamu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Mheshimiwa *Engineer* Mathew Kundo kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi; Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 383

**Kuboresha Uwanja wa Ndege Mafia**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza:-

Je, lini Uwanja wa Ndege Mafia utaboreshwa ili ndege kubwa ziweze kutua?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kutokana na umuhimu wa Kiwanja cha Ndege cha Mafia katika kuhudumia watalii na wananchi kwa ujumla kiwanja hiki kina barabara nzuri ya kuruka na kutua, barabara ya kiungio na eneo la maegesho kwa kiwango cha lami. Miundombinu hiyo inawezesha ndege zenye uwezo wa kubeba takribani abiria 50 kwa wakati mmoja kama *ATR 42* na *fokker 50* kutumia kiwanja hiki kwa ufanisi majira yote ya mwaka (kiangazi na masika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Serikali imepanga kusimika mfumo wa taa za kuongozea ndege ili kuwezesha ndege kutua na kuruka nyakati za usiku. Mipango ya Serikali kwa miaka ya fedha ijayo ni kurefusha barabara ya kuruka na kutua pamoja na kujenga jengo jipya la abiria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, David Kihenzile nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kufuatia changamoto za usafirishaji na ukuaji wa uchumi katika maeneo ya ukanda wa bahari ikiwemo Mafia, Bagamoyo, Kibiti na Mkuranga, ni upi sasa mkakati wa Serikali kuhakikisha inaboresha bandari za maeneo hayo na kujenga meli zake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; nipende sana kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea na mkakati wa kujenga miradi mikubwa ya kimkakati. Swali langu ninataka kujua, ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha vijana wanaopata ajira zile ambazo zisizo na ujuzi *(unskilled labour)* kutoka katika maeneo hayo ya miradi kwamba wanazingatiwa vijana kutoka katika maeneo hayo yenye miradi husika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma kwa jinsi ambavyo amekuwa mfuatiliaji wa miradi mikubwa na hata ya kawaida katika Mkoa wa Pwani ikiwemo ya sekta yetu ya uchukuzi hususan pale Mafia, bandari na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma kwamba Serikali imeamua kuifanya sekta ya uchukuzi kama mishipa kwa kuitambua kwamba ni mishipa ya damu katika Taifa letu. Hivyo basi, inafanya maboresho ya bandari mbalimbali nchi nzima pamoja na kujenga meli katika maziwa makuu yote na sasa ninapozungumza kwa upande wa swali lake la msingi Bandari za Mafia, Mkuranga pamoja na Bagamoyo ya zamani, tayari tumeshapewa idhini na Serikali kupitia Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Hivyo, tunaweka kwenye mpango wa mwaka wa fedha 2025/2026 tuanze maandalizi ya kuzijenga bandari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inakwenda sambamba na kuanza kujenga meli. Tarehe 8 Machi *TASHICO* (Kampuni yetu ya Meli Tanzania) ilisaini mkataba wa kuanza usanifu wa kina kwa ajili ya kutazama fursa zilizopo katika mwambao wa Bahari ya Hindi. Lengo ni nini? Ni kutazama biashara iliyopo. Tunao mpango kama Serikali kuona kwamba tunaimarisha usafiri wa nchi jirani kama vile Visiwa Comoro, Madagascar, Shelisheli pamoja na maeneo kama vile Mtwara, Tanga, Lindi na kadhalika. Hivyo, tutakapokamilisha usanifu huo tutakwenda hatua ya pili ya kuanza kujenga meli hizo kulingana na mahitaji na kujua fursa ambazo ziko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameuliza kuhusiana na vijana waliopo katika maeneo hayo wapewe kipaumbele. Kwanza, swali hili limekuwa likiulizwa sana hapa Bungeni. Ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba nchi hii ni yetu sote. Ni haki ya kila Mtanzania kuajiriwa mahali popote bila kujali kuna mradi au hakuna mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazingatia pia kwamba, kodi zinazojenga miradi hiyo ni kwa Watanzania wote. Aliyekuwepo Iringa analipa kodi katika mradi uliokuwepo mkoa mwingine. Hivyo basi, ninapenda kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba tuendelee kutoa fursa kwa vijana wetu nchi nzima wafanye kazi popote. Aidha, tukubaliane pia yako maeneo ambayo vijana hawapendelei sana kufanya kazi zile ambazo ni *unskilled*. Hivyo, hata mjenzi angependa kwenda kutafuta sehemu ambapo vijana wako tayari kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijahitimisha nitoe rai pia kwa kutambua umuhimu kwamba mradi unapotekelezwa kwenye eneo fulani ni vyema vijana wa eneo wakapewa kipaumbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaagiza wakandarasi waliopo kwenye sekta yetu ya uchukuzi watazame pamoja na kuchukua

maeneo nchi nzima ya nchi hii lakini pia watazame katika eneo mradi uliopo ili wapewe kipaumbele vijana wa eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, Mheshimiwa Suma na Esther nimewaona.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itaboresha Uwanja wa Ndege wa Kilwa na Nachingwea, ukizingatia kwamba Uwanja wa Ndege wa Nachingwea umetumika sana katika ukombozi wa Bara la Afrika? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Pathan kwa swali lake la nyongeza. Serikali inao mpango wa kuboresha viwanja vyote katika nchi hii na katika viwanja alivyovitaja kwa sasa hivi tupo kwenye hatua za awali kwa ajili ya kulipa fidia. Tukimaliza fidia pamoja na kutwaa maeneo tutakwenda kwenye hatua ya pili kwa ajili ya kuviendeleza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Fyandomo.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Je, ni lini safari za ndege za kutoka Dodoma kwenda Mbeya zitaanza, ukizingatia Mbeya kuna abiria wengi sana? Unapokwenda Mbeya mpaka uende Dar es Salaam ndiyo uende Mbeya.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza dada yangu Mheshimiwa Suma Fyandomo kwa swali lake aliloliuliza la kufuatilia safari za ndege Mkoani Mbeya. Ni kweli Mkoani Mbeya kuna abiria wengi na ndege hazitoshi, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Suma kwamba siyo Mbeya tu, kutokana na kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia

Suluhu Hassan ameifanya ya kujenga viwanja vingi mahitaji ya ndege yameongezeka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tungesema kila Mbunge asimame karibu Wabunge zaidi ya 20 wangeweza kusimama ili tuongeze ndege kwenye maneo yao. Hata hivyo, kutokana na umuhimu huo mkubwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imepanga kununua ndege nyingine mpya za masafa marefu na mafupi pamoja na ndege ya mizigo. Tunategemea kwamba kadiri muda utakavyozidi kuongezeka ndivyo tutaendelea kuboresha na kupeleka ndege kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine kabla sijamaliza kujibu swali lake ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba viko viwanja hivi ninavyoongea zaidi ya vitano ambavyo vinafanyiwa maboresho vikikamilika navyo vitahitaji ndege. Kwa hiyo, Mheshimiwa Suma na Wabunge wote waendelee kutuvumilia wakati Serikali inaendelea kutafuta suluhu ya kudumu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwisho niziombe sekta binafsi kwa maana *private operators* wa hizi ndege watazame fursa zilizopo Mkoani Mbeya na maeneo mengine kwa sababu siyo lazima kupeleka ndege za Serikali. Tunazo kampuni nyingi, hebu zichangamkie fursa hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Shally Raymond nilikuona.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbuga ya Serengeti ni kati ya mbuga kubwa na maarufu kwa Afrika ambapo watalii mbalimbali kutoka duniani hupenda kutembelea lakini kwa sasa hivi *the only entry point its either* watue Kilimanjaro au Arusha ndio waweze kuja Serengeti au watue Kenya waweze kupitia Tarime na kwenda Serengeti kitu ambacho kinakuwa kinawa-*discourage at a time*. Nikataka kujua ni lini Uwanja wa Serengeti utaanza kujengwa ili sasa watalii hawa waweze kuja

moja kwa moja na kuongeza uchumi wa nchi yetu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Matiko kwa hoja yake ya Serengeti. Hata wiki iliyopita nilikuwa ninazungumza na viongozi wa CCM wa Mkoa wa Mara, kilio chao kikubwa ni hichohicho. Ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Matiko kwamba Serikali inao mpango wa dhati na imeshaweka kwenye Bajeti ya 2025/2026 kuanza mchakato wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Serengeti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Subira Mgalu nimewaona.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Uwanja wa Moshi utakamilika? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Moshi tunaufahamu ni uwanja wa kihistoria katika Taifa letu. Serikali kwa kutambua umuhimu huo mkubwa ilishaanza ujenzi na hivi ninavyozungumza iko zaidi ya 50%. Nimwombe Mheshimiwa Shally Raymond atupe muda kidogo wakati tunaendelea kufuatilia taratibu za malipo zikamilike ili mkandarasi aendelee kulipwa na hatimaye aweze kukabidhi uwanja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imerejea mpango wake wa ujenzi wa Bandari Bagamoyo na kwa kuwa wapo wananchi ambao waliahidiwa ardhi katika Kata ya Zinga; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri aliwahi kujibu na kukubali ombi langu la kutembelea Kata ya Zinga ili awasikilize wananchi wa maeneo yale hususan wa Mlingotini. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kutekeleza

ahadi yake ili awasikilize wale wananchi ambao waliahidiwa kupata ardhi mbadala kwa ajili ya eneo ambalo limetengwa kujengwa Bandari ya Bagamoyo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari na Mheshimiwa Mbunge dada yangu Mheshimiwa Subira Mgalu, baada ya kutoka hapa tupange ziara twende Lindi tukazungumze na wananchi hao ili kuwaelewesha umuhimu na mawanda mapana ya Bandari yetu ya Bagamoyo Mbegani. Kwa sababu Taifa tayari sasa limeshaona fursa hiyo na tuko tayari kwa ajili ya kuanza uendelezaji wake.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa.

Na. 384

**Kuanzisha Kituo cha Meli Lifuma na Nsele Ziwa Nyasa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanzisha Kituo cha Meli katika Vijiji vya Nsele na Lifuma ili kuwaondolea adha ya usafiri wananchi wa maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Februari 2023, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* ilikamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya kuendeleleza Bandari za Mbamba Bay, Itungi, Kiwira, Ndumbi, Manda, Matema, Liuli and Lupingu. *TPA* ilianza utekelezaji wa ujenzi wa Bandari ya Ndumbi ambayo imekamilika. Kwa sasa *TPA* inaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa Bandari ya Mbamba Bay.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Bandari zingine katika Ziwa Nyasa vikiwemo Vijiji vya Nsele na Lifuma utaendelea kufanyika kadri rasilimali fedha itakavyopatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; tulikwenda pale Itungi na Mheshimiwa Naibu Waziri tukaiona ile Meli ya *MV*-Songea bado iko vizuri sana. Je, lini Serikali itatoa fedha ili meli ile ikarabatiwe na kuweza kusaidia usafiri wa wananchi wa Ziwa Nyasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; wananchi wa Ziwa Nyasa, Ludewa ina kata nane wanatumia usafiri wa maboti ambayo mengine hayana usalama kwa sababu ratiba ya meli ni mara moja kwa mwezi. Je, nini maelekezo ya Serikali ili kusaidia wananchi wale waweze kusafiri kwa usalama mkubwa ndani ya Ziwa Nyasa?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Kamonga kwa ufuatiliaji wake mkubwa wa usafiri katika Ziwa Nyasa. Ni kweli mimi na yeye tulikwenda pamoja na Wabunge wengine ambao wanapakana na Ziwa Nyasa tulifanya ziara katika Ziwa hilo tukatambua fursa zilizopo na changamoto ambazo zinawakumba wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mambo ambayo Waheshimiwa Wabunge waliishauri Serikali ikiwa ni kutimiza jukumu lao la msingi la kuishauri na kuisimamia Serikali, ilikuwa ni kuomba Meli ya *MV* Songea irejeshwe kwa sababu ni mbovu na imesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusikia kilio chao Serikali makini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, ilifanya maamuzi katika mwaka wa fedha 2025/2026 wa kurejesha meli hiyo. Tumetenga bilioni 4.0 na katika mwaka wa fedha 2025/2026 tunakwenda kukarabati meli

hiyo kwa sababu kwanza, ilivyotengenezwa inaendana na hali halisi ya Ziwa Nyasa kwa sababu inaweza kustahimili mawimbi pia inatumia mafuta kidogo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, amezungumza kuhusu ratiba. Kwanza, nimpe pole kwa sababu kuna changamoto pale Kyela ya mafuriko na hivi navyozungumza tunapata changamoto kubwa ya kupata vitendea kazi kama mafuta na vitu vingine. Hivyo, usafiri ni kama vile umesitishwa. Lakini mara baada ya hali itakapotengemaa naielekeza Kampuni ya Meli Tanzania *(TASHICO)* irejeshe ratiba zake angalau mara mbili badala ya kufanya mara moja kwa mwezi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi Mbunge wa Mpanda Mjini.

Na. 385

**Kufunga Taa za Kuongozea Ndege Uwanja wa Ndege Mpanda**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, lini Taa za kuongozea Ndege zitafungwa katika Uwanja wa Ndege Mpanda?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu gharama za usimikaji na uendeshaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege ni kubwa na hivyo Serikali imekuwa ikitekeleza miradi hiyo katika Viwanja vya ndege vyenye miruko na mituo mingi ambayo inapelekea hitaji la mashirika ya ndege kuja nyakati za usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanja cha Ndege cha Mpanda kina miundombinu ya barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio na eneo la maegesho katika kiwango cha lami na jengo jipya la kisasa la abiria na idadi ya ndege

zinazotumia Kiwanja cha Ndege cha Mpanda kwa ratiba maalum ni kutoka Shirika la Ndege Tanzania *(ATCL)* pekee ambayo inakuja na mara tatu kwa wiki Jumanne, Alhamisi na Jumamosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, serikali inatoa wito kwa wadau mbalimbali ikiwemo mashirika ya ndege yaweze kuanzisha safari za ratiba maalum katika kiwanja hiki na Shirika la Ndege la *ATCL* kuongeza idadi ya miruko na mituo ili kuwezesha Serikali kusimika mfumo wa taa za kuongozea ndege.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, niishukuru Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utayari najua kwa maana ya Bandari ya Karema imejengwa kuna meli nne zinaendelea kujengwa kuna barabara ya lami inapelekwa Karema huo wote ni utayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; Serikali inasema nini katika kufungamanisha Uwanja wa Ndege wa Mpanda na fursa nyingine zilizopo kama utalii na Soko la Kongo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; nini mkakati wa Serikali katika kusaidia Uwanja wa Ndege wa Mpanda kupata miruko iwe ni kutoka *ATCL* au makampuni mengine binafsi?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Kapufi, kwa maswali yake ya nyongeza mawili na nimpongeze kwa anavyofuatilia kwa karibu sana maendeleo ya mkoa wake na kipekee jimbo lake, lakini zaidi alivyotambua kazi kubwa ambayo Serikali imeshaanza kufanya katika eneo hilo la Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa Mkoa wa Katavi pamoja na uwepo wa

kuboresha ule Uwanja wa Ndege wa Mpanda na hii ni kutokana na ukweli kwamba, Katavi:

(i) Kuna utalii na sote ni mashahidi;

(ii) Madini ya kutosha;

(iii) Mazao ya kutosha;

(iv) Serikali inavyozungumza hivi inakamilisha ujenzi, maboresho ya reli ya kutoka Kaliuwa mpaka Mpanda na inaanza maandalizi mwaka wa fedha ujao 2025/2026 kujenga reli ya mita *gauge* kutoka pale Mpanda kwenda mpaka Kalema;

(v) Tayari tunajenga barabara ya lami kutoka pale Mpanda kwenda mpaka Karema; na

(vi) Tunajenga meli mbalimbali kwenye Ziwa Tanganyika yote haya na mengine ambayo sijayataja yanadhihirisha na kuthibitisha umuhimu wa Uwanja wa Ndege wa Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali tayari ninavyozungumza hapa imefanya makubwa katika Uwanja wa Mpanda. Kwanza, tumeshatengeneza na kukamilisha *runway* yenye urefu wa mita 2000. Pili, tayari tumejenga jengo la abiria la 1.4 bilioni na linatumika hivi navyoongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Kapufi akubali kwamba, jitihada hizi zinadhirisha na kuthibitisha dhamira ya dhati ya Daktari Samia Suluhu Hassan kuthamini na kutambua Mkoa wa Katavi. Hivyo basi, ninaomba nichukue jambo lake la taa za kuongozea ndege tuendelee kutazama huko mbeleni kadiri tukipata fedha tutaweza kujitahidi kuhakikisha kwamba, uwanja huu unakuwa na taa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taa hizo pia kama nilivyosema kwenye swali la msingi zinategemeana sana na miruko, ninaomba nitumie nafasi hii kuzishauri na kuziomba kampuni mbalimbali za

ndege nchini zilizo nchini na nje ya nchi kutazama fursa zilizopo katika Mkoa wa Katavi. Abiria wapo wa kutosha hebu tuongeze ndege, tukishaongeza ndege tutakuwa na miruko, tukiwa na miruko tuta-*justify* hata umuhimu wa kwenda kuweka taa za usiku kwa sababu ndege zitakuwa zipo za kutosha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suleimani Kakoso nilikuona.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa uwekezaji mkubwa sana uliowekezwa kwenye eneo la Mkoa wa Katavi hasa uwanja wa ndege pamoja na jengo la abiria na mengine ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwambauuliza Serikali ilikuwa imeahidi kufanya miruko ya ndege kutoka Dar es Salaam, Mpanda hadi Lubumbashi. Ni lini Serikali itatekeleza ahadi ambayo ilikuwa imetoa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo la nyongeza Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Miundombinu na Mbunge wa Kalema Mheshimiwa Kakoso kwamba, hoja yake tumeipokea na tunaendelea kuichakata Serikalini ili kutazama fursa zilizopo na uwezekano wa kuanza. Pia, Mheshimiwa Kakoso ninajua kuna suala ambalo amesahau kwa sababu tu pengine ni swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjulishe pamoja na Wabunge wengine wa Mikoa mitatu Rukwa, Kigoma na Katavi kwamba, jana meli yetu ya *MT*-Sangara ilisimama kwa muda mrefu imeanza kufanya safari zake rasmi kutoka Kigoma kwenda Mpurungu kwenda Kalemii na kwenda Bujumbura. Hii ikiwa inamaanisha nini? Utekelezaji wa yale ambayo wanayaagiza Waheshimiwa Wabunge lakini Serikali ikiahidi.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Isuma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 386

**Malipo ya Fedha za Likizo Kwa Askari Polisi**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, kwa nini Askari Polisi hawalipwi fedha za likizo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikitenga fedha kwenye bajeti yake kila mwaka kwa ajili ya malipo ya stahili mbalimbali ikiwa ni pamoja na malipo ya likizo kwa Askari Polisi. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Jumla ya kiasi cha fedha 4,359,600,000 kimelipwa na katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya kiasi cha fedha 4,475,000,000 kimetengwa kwa ajili ya askari kwenda likizo. Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya malipo na stahili mbalimbali za askari ikiwemo malipo ya likizo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Fyandomo.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Swali la kwanza, ninaomba kujua ni lini Serikali italipa madeni mbalimbali ya Maafisa Polisi na Askari wa vyuo mbalimbali pamoja na Askari Magereza fedha zao wanazozidai?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa nyakati tofauti tofauti Serikali imekuwa ikiahidi kwamba, inahakiki madeni yote ya askari hapa nchini, lakini mpaka sasa hakuna majibu yaliyotolewa. Je, ni lini Serikali itamaliza uhakiki wa madeni ya Askari Polisi wote wa Tanzania ikiwa ni pamoja na Askari wetu wa Mkoa wa Mbeya wanajitoa sana kufanya kazi, lakini wanadai fedha kwa muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze sana Askari wetu kwa kazi kubwa wanayofanya ya kulinda rai ana mali zao hapa nchini. Pia nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Suma Ikenda ambaye amekuwa akiwapambania sana Askari wetu hapa nchini pamoja na Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua je, ni lini malipo yatakamilika kwa Askari Magereza na Polisi? Kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka na kulipa Askari wetu. Kama nilivyojibu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 tayari wameshalipa fedha kiasi cha bilioni 4.3 na kwenye mwaka wa fedha huu unaoendelea 2024/2025 wametenga bilioni 4.7 tayari kwa ajili ya kulipa Askari wetu wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kulipa askari polisi hii itaenda sambamba pia na Askari wa Jeshi la Magereza na Askari wengine. Kila mwaka Serikali inatenga fedha kupitia majeshi hayo kwa ajili ya kulipa madeni ya Askari wetu ambao wanafanya kazi kubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, ni kweli Serikali imekuwa ikifanya uhakiki na ndiyo maana tumelipa hawa, baada ya kukamilisha uhakiki ndipo tunafanya malipo. Tunafanya uhakiki, baada ya kumaliza uhakiki tunapeleka Wizara ya Fedha

kwa ajili ya malipo. Kwa hiyo, Serikali itafanya hivyo kila wakati kuhakiki madeni na kulipa kama ambavyo nimejibu kwenye jibu la msingi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Sillo kwa majibu hayo kwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, aulize swali lake.

Na. 387

**Kupima na Kupanga Makazi Kandokando mwa Barabara ya Moshi – Arusha**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakuja na mpango wa kupima na kupanga makazi yaliyopo kando ya Barabara Kuu ya Moshi - Arusha na Arusha *bypass*?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Naibu Waziri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Programu ya KKK iliziwezesha Halmashauri za Wilaya za Meru, Moshi na Arusha ambazo zinapitiwa na barabara Kuu ya Moshi – Arusha na barabara ya mchepuko (*bypass*) kwa kuzipatia fedha kiasi cha shilingi billioni 1.9 ambazo zilitumika kupanga, kupima na kumilikisha jumla ya viwanja 4,160 na hili ni zoezi endelevu kukabiliana na hali hiyo ya ukuaji wa kasi wa miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa rai kwa Mamlaka za Upangaji nchini kuendelea kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuainisha maeneo au miji chipukizi ikiwepo ile iliyopo kandokando mwa barabara zetu iliyoiva kwa ajili ya kuendelezwa kama miji kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji ili maeneo hayo yaweze kupangwa, kupimwa na kumilikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka hizo zinashauriwa kuwasilisha andiko Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili kuwezeshwa Mikopo kwa ajili ya Miradi hiyo ya Upangaji, Upimaji na Umilikishwaji katika kukabili ukuaji wa Kasi wa Miji yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii tena na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini niseme tu kwamba, kumekuwa na makampuni mengi sasa hivi ambayo yanafanya biashara ya ardhi kwa sababu ardhi ni mali na mtaji mkubwa. Wanachokifanya ni kununua mashamba na kuyakatakata katika viwanja vidogo vidogo na kuuzia wanaohitaji. Je, Serikali haioni kwamba, sasa hivi ni wakati muafaka wa kutoa mwongozo wa namna gani ya kufanya biashara ya ardhi ili tuondokane na biashara hii kusababisha miji yetu inakuwa ni *squatters*?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunayo makampuni mengi ambayo yanafanya shughuli hizi za upimaji wa ardhi yetu hapa nchini, lakini tuna miongozo tayari inayowaelekeza namna ya kufanya kazi zao ili kuondokana na haya maeneo ya *squatter*. Inawezekana kabisa kukawa na ukiukwaji wa zile taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe maelekezo kwa makamishna wasaidizi wa mikoa, makampuni binafsi yatakapojishirikisha kwenye eneo lolote ambalo limebainika basi lazima yale maombi yao yapite kwa makamishna ili kuhakiki ili kusijitokeze tena ujenzi

holela kwenye maeneo ya wananchi na hata kuwa na *standard* za viwanja kwa sababu wanapima viwanja vidogo vidogo *square meter* 200, *square meter* 300 wakati mwingine hazileti tija kwenye maeneo yenu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi nimekuona.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu waishio maeneo ya Girafu Bara walitoa fedha zao kwa ajili ya kupimiwa viwanja hivyo, lakini mpaka sasa hivi ni zaidi ya miaka kumi bila kupata hati wala kupimiwa. Je, nini kauli ya Serikali juu ya wananchi wangu waliokaa miaka yote hiyo bila kujua hatma ya kupata hati zao? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa wakati mpango huu wa KKK ulipoanza ulijitokeza tatizo kwenye makampuni ambayo yalikuwa yanaendesha zoezi hili na kwa sasa tumekuja na mpango maalum wa ukwamuaji ambao unakwenda kutibu ugonjwa huu wa wananchi waliochukuliwa fedha zao na makampuni ili wapate hati na kumilikishwa maeneo yao. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge tuvute subira kidogo wakati tunalichakata kwa sababu si tatizo la sehemu moja kimsingi ni tatizo la nchi nzima.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge. Muda wetu wa maswali umekwisha kwa siku ya leo na sasa nina matangazo hapa. Kuna matangazo ya wageni ambao wametembelea Bunge asubuhi hii.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza ninaanza na wageni waliokaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, tuna mgeni wa Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo ambaye ni Mheshimiwa Paul Chacha, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, na Ndugu David Mwaka Mwenyekiti wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika Mazao Mchanganyiko. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wanne wa Mwenyekiti wa Bunge ambaye ni mimi mwenyewe ni wageni wangu ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Kitivo cha Sheria, wako watatu pale, kuna Ndugu Latifa Njaa, Ndugu Geremana Sweke na Ndugu Lorein ambao wameambatana na mlezi wao hapa Dodoma Ndugu Zelda Mashulano. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wasichana hawa wa Chuo Kikuu cha Mzumbe wametupatia tuzo Nchini Austria kwenye mashindano ya *Best Claimant Memorandum* ambapo Chuo Kikuu cha Makerere na Chuo Kikuu cha Mzumbe ndiyo kimeweza kuwa washindi kwa Afrika. Hongereni sana wasichana wetu kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe ambao pia wamefika robo fainali ya mashindano ya *Willem Vis International Commercial Arbitration* huko huko Austria. *(Makofi)*

Hongereni sana naamini wasichana wa Kitanzania watakuwa wamepata moyo na wameona kwamba tunaweza na ni sifa kwa nchi yetu kuona mwanamke au mtoto wa kike anafika mbali na kuingia kwenye nyanja za Kimataifa. Hongereni sana na karibuni katika Bunge letu. *(Makofi)*

Tuna pia mgeni wa Mheshimiwa Charles John Mwijage ni Ndugu Leonard Nzimbehya ambaye ni Mwekezaji Sekta ya Kilimo kutoka Mkoani Kagera. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Ndugu Atus Celestina, rafiki yake kutoka Kyerwa Mkoani Kagera. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya ambaye ni Ndugu Ernest Jerome, Meneja Mahusiano kutoka Shirika la *Kickstart International* Tanzania. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana watoto wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Robert Chacha Maboto ambao ni ndugu zake kutoka Bunda Mkoani Mara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Makatibu wa Kata wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Ilongero Mkoani Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Jacquline Andrea Kainja, Ndugu Aziza Abdallah, maarufu kama Ziza Malick, Rafiki yake na Mtangazaji wa kipindi cha *Central Clouds TV*. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 15 wa Mheshimiwa Abbas Gulam Tarimba, Kikundi cha *Twende Pamoja na Mama Sports Promotion* kutoka Dar es Salaam, wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Ndugu Mohamedi Haji, pia yupo Mchezaji wa Zamani wa Simba na Yanga na Timu ya Taifa, Ndugu Mwanamtwa Kiwelu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 18 wa Mheshimiwa Mbarouk Juma Khatib, Waheshimiwa Madiwani kutoka Kaskazini Unguja na Mjini Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili mafunzo. Tunao wanafunzi 91 na Walimu Nane wa Shule ya Awali na Msingi Didas kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Gairo Mkoa wa Morogoro. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka huko Morogoro karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 50 na walimu 10 wa Shule ya Sekondari Chibelela kutoka Wilaya ya Bahi Mkoani Dodoma pia. Karibuni sana wanafunzi wetu na wageni wote ambao mpo leo, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Katibu, tuendelee.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wetu kwa Wizara ya Kilimo. Tunaanza na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde wajiandae, Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. Waheshimiwa Wabunge niwaombe kwamba hii bajeti ambayo kila mtu anasema ni nzuri tuipitishe, lakini niwakumbushe kwamba makubaliano ya viongozi wa nchi huru za Afrika yaliyofanyika Malabo mwaka 2014, Malabo ni kule Equatorial Guinea, viongozi walikubaliana kwamba bajeti za Wizara za Kilimo za nchi zote za Afrika ikiwa chini kabisa iwe 10% ya bajeti ya Taifa hilo. Kwa hiyo, hapa tunachopaswa kufanya kwanza toka 2014 walisema tulikuwa kwenye bilioni 294 tuko trilioni 1.2, kwa hiyo tutoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwamba tunaelekea. Kwa hiyo, kila mtu ajue bajeti ya mwaka huu ni kiasi gani, halafu apige hesabu kwenye *ten percent* tuko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili sisi watu wa Jimbo la Musoma Vijijini tuna furaha kubwa sana kwenye hii bajeti, hii ni kwa sababu tunayo mabonde mawili makubwa, Bonde la Mto Suguti na Bonde la Bugwema, mabonde yote mawili yamefanyiwa tathmini na yanafaa kwa umwagiliaji mkubwa na ambalo limepitishwa sasa ni hili Bonde la Bugwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa shukrani Mheshimiwa Rais alivyokuwa Jimboni kwangu sikuomba vitu vingi nilimwomba viwili tu, bonde hili na barabara na yote tumepata. Tunampa shukrani nyingi sana na Jimbo la uhakika ambalo anajua ana kura nyingi ni la Musoma Vijijini kuzidi yote hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Bonde la Bugwema tumepata, mkandarasi amepatikana. Hili ndugu zangu kwa nini ninamsifia Mheshimiwa Rais ni kwa sababu mwalimu alianza kulijenga mwaka 1974, kwa zaidi ya miaka 50 Mheshimiwa Rais amefufua tena huu mradi sisi watu wa Musoma Vijijini tuna furaha kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu ni kwamba huyu Mkandarasi ambaye atakabidhiwa hivi karibuni malengo ya mwalimu ya miaka ya 1970 kwamba asaidie wakulima wadogo yapo pale pale, kwa hiyo, hili ni bonde kwa ajili ya wakulima wadogo na wakulima wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatubahatishi tumeshapanga na mazao yatakayolimwa humu, kwanza ni mpunga, pili ni mahindi, tatu ni alizeti. Halafu tunachukua mazao haya yanayofanana fanana yaani mbaazi, dengu, choroko na maharage vilevile tutalima pamba. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Bashe kwa kazi nzuri unazozifanya usishawishike Bonde la Bugwema kuanza kulima miwa, hesabu na mimi nipo kwenye Kamati ya Kilimo hesabu tuliyonayo ni kwamba kuanzia mwakani tutakuwa na sukari ya kutosha kwa hiyo Watanzania kila mabonde yote yasigeuke kuwa mabonde ya miwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni biashara, mazao tuliyoyachagua ni kwa sababu tutafanya biashara ya ndani mwaka huu tuko watu milioni 70.5, mwaka 2050 wakati tunatimiza dira yetu tutakuwa watu karibu milioni 140. Kwa hiyo, soko la ndani limo ndiyo maana tunataka kilimo kikubwa kwenye Bonde la Bugwema halafu soko la nje ni nchi za Kiafrika tuna mikataba mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Afrika tuko watu bilioni 1.5 tukifika mwaka 2050 tutakuwa bilioni 2.5 wote hawa wanataka chakula na wote hawa huenda wataanza kununua kutoka kwenye Bonde letu la Bugwema. Sasa ninatoa umuhimu wa kilimo ni biashara. Mpunga tunataka kuulima kwa sababu duniani ambapo sasa hivi kuna watu bilioni 8.2 zaidi ya 50% wanatumia mchele, wali au mpunga kama chakula kikuu 50% kwa hiyo hatutofanya kosa sisi kulima mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile soko la mpunga miaka mitatu inayokuja duniani ukubwa wake kibiashara utakuwa wa bilioni 350 na sisi tunataka tunyemelee hilo soko. Mahindi yanamatumizi matatu kama chakula kwa binadamu kwa mifugo halafu viwandani yanatumika kutengeneza *ethanol,* kwa hiyo tukipata mengi sana tunaweza kufikiria mambo ya *ethanol.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaazi tunazichagua kwa sababu biashara yake sasa hivi duniani ni bilioni 68 na ikifika mwaka 2030 itakuwa ya bilioni 75 kwa hiyo Mheshimiwa Bashe uko sahihi kusema 'Kilimo ni Biashara' na sisi Musoma Vijijini tunaenda mbali tunataka viwanda. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge isiwe tu kwamba kilimo ni biashara lakini kilimo vilevile ni viwanda, kwa hiyo sisi tunataka mazao yatakayolimwa kule Bugwema kwenye bonde kubwa kabisa, yatakuwa yanachakatwa na humo na tunaongezea thamani ya mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunalima pamba ombi letu ni kwamba ile *ginnery* ya Mgango, Waziri Bashe ile *ginnery* unafahamu na Waziri wa Viwanda lazima ile *ginnery* ifufuke halafu pamba tunayoilima tunataka kuanza kiwanda kipya pale majirani zangu Musoma Mjini wawe na kiwanda. Huko Bugwema kuna wafugaji sana, tunataka kufufua viwanda vyetu vya maziwa vya Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara na Musoma Vijijini tumeanza uvuvi wa vizimba na huko Musoma Vijijini mimi nimepanga ndani ya miaka minne ama mitano tuwe na Kiwanda cha Samaki Musoma Vijijini. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuende na kilimo ni biashara tuende na kilimo ni viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuwaeleza kidogo kuhusu maji ya Ziwa Victoria, maana tunataka kuyatumia sisi binadamu, mifugo yetu inataka kutumia maji ya Ziwa Victoria na sasa tumeingia ukulima mkubwa wa umwagiliaji wa kutumia maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaenda kujadiliana na nchi zingine ambazo zinatumia maji ya Ziwa Victoria ninaomba jamani mjaribu kutumia watu wa Musoma Vijijini ambao wana historia nzuri ya Ziwa Victoria. Ziwa Victoria siyo la zamani sana umri wake ni miaka laki nne tu siyo la zamani sana. Kwa hiyo wale wenzetu wa Kaskazini na hii *point* ni muhimu sana, watakaokuwa wanaenda kwenye *discussions* na nchi za Kaskazini tunasema Lake Victoria *is four hundred thousand years old,* lakini Mto Nile wanasayansi zamani walipiga mahesabu wakadhani Mto Nile umri wake ni miaka milioni tano, lakini juzi mahesabu yamepigwa upya tena Mto Nile unaonekana umri wake ni miaka milioni thelathini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mtu akija kusema msitumie maji ya Ziwa Victoria kwa kuwa yataisha kwenye Mto Nile lazima ufanye majadiliano ya kisayansi, kwamba Mto Nile ulikuwepo kabla ya Ziwa Victoria kuwepo na maji ya Mto Nile tutaongea siku nyingine huwa yanatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Ziwa Victoria nalo tulitumie kwa umakini mbali ya kuwa na umri wa miaka laki nne Ziwa Victoria limewahi kukauka mara kadhaa, lakini msiogope, limewahi kukauka mara kadhaa, mara ya mwisho kumbukumbu zetu huku kwa wanasayansi huku ndiyo zinakuwa kumbukumbu tu, pengine Daktari zipo? Haya. Kumbukumbu zetu ni kwamba mara ya mwisho lilikauka ilikuwa ni miaka 17,000 iliyopita, kwa hiyo ni siku nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna haki ya kutumia maji wa Ziwa Victoria kwa sababu 49% ya Ziwa Victoria iko Tanzania, Uganda ina 45%, Kenya wana asilimia sita. Kwa hiyo, kama tunatumia kwa uwiano tuna haki ya kufanya kilimo kikubwa cha umwagiliaji kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mto Nile ambao mnaweza kuanza kuwa na wasiwasi, nimewaeleza ni wa umri wa miaka zaidi ya milioni 30, halafu hesabu imepigwa *discharge* yake yale maji yanayotembea Mto Nile mle ndani, *discharge* yake kwa sekunde moja ni lita milioni 3.5 yaani ile *average discharge* ni 3.1 *million liters per second.* Kwa hiyo, ukichukua maji yanayoweza kutunzwa kwenye Mto Nile na Maziwa yake na mito yake *storage capacity* yake kwa mwaka ni *cubic meter* bilioni 180 ambazo ukipiga mahesabu ni sawasawa na *cubic kilometer* 180. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujazo wa Ziwa Victoria, ni *cubic meter* 2,760, ukipiga hiyo *ratio* ni *less than ten percent,* kwa hiyo ndugu zangu Watanzania tuna haki ya kutumia maji ya Ziwa Victoria kwa binadamu kwa mifugo na bado kwa umwagiliaji na siku tutakavyoitwa kwenye huo mjadala nimesema kodisheni majeshi kutoka Musoma Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa upande wa umwagiliaji kwa nini lazima tufanye umwagiliaji? Siyo kitu kigeni sisi tumechelewa, mambo ya umwagiliaji yalianza kabla hata ya *Jesus Christ,* inajulikana kwamba miaka 6,000 kabla ya kuzaliwa Yesu Kristo. Mambo ya umwagiliaji yalikuwa yanafanyika kwenye kule *Middle East,* nchi hizo zamani zilikuwa zinaitwa Mesopotamia kwenye Mto wa Tigris na Euphrates. Kwa hiyo jamani sisi tumechelewa kufanya kilimo cha umwagiliaji na ninaomba niunge hoja kwa sababu niliambiwa ni dakika tano kumbe wameniongeza dakika, tayari zimekwisha? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya nimalizie na Mheshimiwa Musukuma ame-*support* haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jamani namalizia kwa kusema kwamba tunachoiomba Serikali kwenye mpango wa maendeleo, kwenye ile *draft* wale wa mpango wa maendeleo lazima hili suala

la umwagiliaji waweke kipaumbele kikubwa, kwa sababu uchumi mkubwa na watu wengi walioajiriwa ni kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo. Nilimtaja Mheshimiwa Charles Mwijage na Mheshimiwa Livingstone Lusinde ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia hii sekta ya uzalishaji, moja ya sekta ambazo nimeziishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo manne ya kusisitiza kabla ya sijazungumza. Mafanikio katika hii Wizara, katika Serikali yanaonekana, tumeona ongezeko la uzalishaji, tumeona ongezeko na bei nzuri ya mazao, ninashauri kwamba tuongeze zaidi uzalishaji tukilenga zaidi kwenye kuongeza tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba wengi tumepata mavuno makubwa lakini siyo kila sehemu tumetumia tija kubwa. Suala la pili unapokuwa umeongeza bei, wananchi wanafurahia zao lile, tuongeze mazao zaidi wananchi waepuke kutegemea zao moja wawe na *portfolio*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwetu Kagera tuliwahi kutegemea kahawa ilipoanguka kilikua kizaazaa na ni historia mpaka watu wakakata mibuni yao tumekuja kuamka leo. Tuwekeze katika kutafuta masoko, Mheshimiwa Waziri wekeza katika kufuta masoko. Watu wanapofurahia kilimo unapowahimiza kulima wanapozalisha mazao lazima tuwape *assurance* ya kufuta masoko. Nichukue fursa kuishukuru Serikali na kipekee Mheshimiwa Rais katika hii diplomasia, diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina uzoefu katika masuala ya masoko, kuna masoko tulishindwa kuyaingia lakini sasa hivi masoko hayo yanatutafuta, hii ni diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni maeneo ya kilimo. Nawapongeza Serikali kwa kujenga sekta za umwagiliaji na napongeza mpango wao wa kuja na umwagiliaji mdogo mdogo. Ninashauri maeneo madogo madogo yapewe kipaumbele kwa sababu matokeo yake yanakuja mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ya kulima kuna matumizi bora ya ardhi *(land classifications)*. Unakuta mtu anapanda mazao katika eneo ambalo halipaswi kupandwa. Mfano rahisi ni kwetu, sisi kwenye *land classifications* - daraja *one* na *two* tumepanda miti na haipaswi, miti inapaswa kupandwa tabaka la sita ama la saba hata jangwani kwenye tabaka la nane nitalieleza zaidi, lakini kwetu Kagera tunalielewa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu katika maeneo ya kulima kuna kurejesha ardhi. Kuna maeneo leo hatulimi kwa sababu unakuta ni tambarare kama barabara, watu wameharibu mazingira. Lazima tutafute mbinu za haraka namna ya kutumia maeneo hayo kwa sababu eneo haliongezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tatu; nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa *BBT* ngazi ya Halmashauri; ninadhani hapa tumekubaliana na tofauti zetu sasa zimekwisha. Hii *BBT* ya Halmashauri ni dawa ya Kichina, Mchina ukiumwa jicho anapiga sindano kwenye jicho. Hii *BBT* ya Halmashauri inawafuata watu mahali walipo, hakuna haja ya kuzoea mazingira. Kama kwenu ni Moshi tunaku-*BBT* Moshi, kama ni Songea tunaku-*BBT* Songea na kwetu Makongora tumeshaanza kuwa-*BBT* vijana na Taifa letu linakwenda kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, marekebisho kwenye *BBT* ya Halmashauri; tusiwalenge vijana na wanawake tu, tuwalenge waliotayari. Wapo watu wana miaka 50 si vijana hawa ni wanaume, lakini wapo tayari kutumika. Wapeni hizo ruzuku, wawezeshe waweze kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais na nimshukuru. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri ile hadithi imefika mwisho, lakini ikafika mwanzo wa mwisho. Mradi wa Mto Ngono

umefika mwisho sasa na tunaanza mwisho wa mwisho. Nimesikia taarifa yake wameshapima, unatafuta wakandarasi. Niwaombe wakandarasi wa dunia nzima ikiwemo Uyahudi, Argentina, (mabingwa wa *irrigation*), njoo mchangamkie utengenezaji wa hekta 16,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Waziri mtumishi wake wa umwagiliaji Kagera anastahili amwandikie hata barua. Jana lilipojibiwa swali langu hapa kuhusu mawanda ya Bonde la Mto Ngono, kijana yule baada ya saa mbili alikuwa *site* katika Kata ya Katoke, akiainisha eneo la kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mheshimiwa Profesa Muhongo, sisi umwagiliaji wa Kagera tunahusisha kilimo cha kahawa na nikipata nafasi nitazungumzia kwa nini tunakwenda kwenye *coffee*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunahusisha mpunga lakini tunahusisha malisho ya mazao kwa sababu fursa ya Mkoa wa Kagera ni uwekezaji katika ufugaji hasa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na mbuzi (bidhaa ambazo zimepata soko kule duniani). Kwa hiyo, mazao kama *Jongos*, *Napier, Usin***,** tunakwenda kuyalima. Hiyo ni katika kuongeza wigo *(diversification)* na kujenga *portfolio* ili mkulima asitegemee zao moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchangia. Nimezungumzia umwagiliaji wa kahawa. Sisi tunapanga mwaka kesho tuzalishe tani 85,000. Ninatambua juhudi za Serikali lakini hapa siyo tunapopaswa kuwa. Hatupaswi kuwa hapa. Mheshimiwa Kavejuru jana amezungumza hatupaswi kuwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi ya Uganda ambayo eneo lake la kulima kahawa ni sawa na Mkoa wa Kagera, mwaka jana wamepata *1.5 billion US Dollar.* Sisi tunalima tani 85,000 wao wapo kwenye tani karibu 380,000; haikubaliki. Nikushukuru Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri aliniita tukakaa chini akasema tufanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ni kuongeza tija, lakini pia kuweza kufanya *irrigation* kama ambavyo tumeamua sisi tunaanza kufanya *irrigation.* Sisi maamuzi ya Mkoa wa Kagera chini ya Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, *RC* Fatma Mwasa ni kwamba anatafuta ekari 10,000 Mkoa mzima wa Kagera, lakini ukifika Muleba Kituo cha Basi, swali la kwanza unaulizwa nioneshe unapolima na kama hulimi mibuni, haujalima chochocte kwa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *the concept is,* kama sisi Tanzania tunaweza kupata mazao *export 3.54 billion* na Uganda anaweza kupata *1.5 billion* na sisi tunamzidi ardhi ukijumlisha eneo lote la Tanzania; hii maana yake ni kwamba tukiwekeza nguvu zetu na tunaweza. Ninatambua mikakati yako Mheshimiwa Waziri, tunaweza kupata Dola bilioni nne kwenye kahawa tu. Sasa, haya mazao mengine yakasindikiza, unakuta haraka kuna *leap frog* na kwenda kwenye Dola bilioni 10 kutoka kwenye mazao tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo tena mazao mengine niliyochagua suala la mpunga au mchele. Afrika tunatumia tani milioni 60 za mchele, lakini Tanzania tunayo *potential* ya kuzalisha tani 14,000. Sasa, ufanye mahesabu utaona kwa nini mimi ninawatabiria kwamba tunaweza kwenda kwenye uwezo mkubwa wa kuleta fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni zao la kakao. Kakao ina bei kubwa lakini tasnia ya *chocolate* ambayo inategemea kakao ni Dola milioni 110 duniani na kakao yenyewe ni Dola bilioni 17. Sasa Mheshimiwa hapa tunachopaswa kufanya katika vipaumbele vyangu vile katika uangalizi kwamba tutambue maeneo Tanzania ambako tunaweza kulima kakao, tulime kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kufanya, Kiwanda cha Kakao sio muujiza. Nguvu ya kakao ni *industry* ya *chocolate.* Sasa kutengeneza *chocolate* siyo sawa na kutengeneza *satellite* ya kwenda mwezini. Tuwakamate Watanzania hawa, tuwafundishe kuanzia viwanda vidogovidogo, viwanda vya kati, kusudi

wawekeze kwenye kakao na *chocolate* tuweze kuuza *chocolate,* Tanzania, Afrika Mashariki na Dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *horticulture*. *Horticulture* inavutia, tuwapatie nguvu watu wa maparachichi. Ninamwambia Waziri watu wanasema mazingira ya biashara ya Tanzania, haimhusu yeye ni Serikali nzima, si mazuri. Mtu anatoka Njombe na gunia lake la *avocado* kupeleka *sample* tani 100, anasimamishwa na watu 1,000, kila mtu anamdai *ribora*. Kwa hiyo, mazingira *(the ease of doing business)* haijawa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la sukari. *Potential* ya Tanzania kwenye sukari ni tani 2,000,000. Hili suala ninalijua na nimelifanyia kazi. Kwa hiyo, tuhimize watu na namna ya kuhimiza ni kuhimiza kwenye viwanda vidogo, ili ile *import* ya *industrial sugar* tu-*refine* Tanzania *sugar* yetu, lakini tuweze ku-*satisfy* soko letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya muda, ninaomba kuunga mkono hoja. Safari imeanza na ni safari ya uhakika. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais. Tunakwenda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Mwijage. Nilimtaja Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mheshimiwa Boniphace Butondo ajiandae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kunipatia nafasi ya kuzungumza ili niseme machache kuhusu Wizara nyeti kabisa katika nchi yetu, Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzee wa *speed 120* Mwijage ametoka kumaliza sasa hivi, ameonesha kwamba; katika nchi ambazo kuna *gap* kubwa kati ya matajiri na maskini na maskini wengi wakilengwa kuwa ni wakulima, ni muhimu *speed* ya Wizara ya Kilimo ikawa ndio matarajio yetu ya ku-*close gap* kati ya maskini na matajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama namna ambavyo Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara wamejipanga unaona wamechechemua kilimo chetu, sasa tunajadili kilimo cha biashara kutoka kilimo cha kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ya Awamu ya Sita ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumeiona katika kilimo. Kwa Mkoa kama Dodoma ambapo tuna tatizo la kuwa na mito inayotiririka maji muda wote, hututegemei kuingia kwenye kilimo cha umwagiliaji bila kutujengea mabwawa, kwa sababu Mkoa wetu sisi mito yetu inatiririka na kuondosha maji moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namna pekee ya kutufanya tuingie kwenye ushindani wa soko la umwagiliaji ni kutengeneza mabwawa makubwa ambayo tutatunza maji halafu maji hayo tutayatumia katika kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, niwe na shukrani kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mvumi kwa ajili ya Serikali kukubali kuanza kutujengea mabwawa mawili makubwa pale Kata ya Manda na Mpwayungu. Hii itakuza uchumi wa eneo lote la Wilaya ya Chamwino. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tumemwona akifanya vitu ambavyo si vya kawaida. Kwa mfano, wote tulikuwepo hapa wakati wa sakata la sukari na bei ya sukari tukafikiria itaishia kwenye shilingi 5,000 mpaka 6,000 lakini kwa kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na timu yake, leo sukari ipo shilingi 2,500. Kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri maana yake Watanzania kama ingebaki ile ile, leo shutuma zote zingekuwa kwake. Ila kwa namna ambavyo wamepambana, wamefikisha mahali ambapo baadhi ya watu hawaamini macho yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tumeona Wizara ikiagiza mitambo ya kuchimbia visima vikubwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Tumwombe tu Mheshimiwa Waziri mitambo ile itakapozinduliwa na Mheshimiwa Rais na kuanza kufanya kazi basi na sisi wa Jimbo la Mvumi watukumbuke, ili tuweze kupata visima vikubwa. Maji yapo chini, kama tumeyakosa maji ya juu basi

tupate haya maji ya chini ya ardhi, ili yaweze kutusaidia katika kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tumeona akipambana kuhusu mbolea. Tuna kiwanda cha ndani hapa Dodoma; kiwanda pekee cha mbolea kinatengeneza mbolea ya kukuzia, mbolea ya kupandia, mbolea ya kunenepesha mazao. Hiki kiwanda kimekuwa na tatizo la madai ya ruzuku yao. Kwa hiyo, tumwombe Mheshimiwa Waziri awasaidie wawekezaji wa ndani wanahitaji kulindwa. Hawa watu wanaajiri watu wengi, wanatusaidia mno, mbolea yao inafika kwa wakati. Kwa hiyo, ni vyema akawawekea ulinzi maalum wa kupatiwa fedha zao ili waweze kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaendelea kuwatia moyo Mawaziri pamoja na Katibu Mkuu na wenzake wote, kazi wanayoifanya ni kazi nzuri. Hii *BBT* ambayo imezungumzwa hapa, nimwombe Mheshimiwa Waziri, si kazi yake kujenga barabara lakini pale Ndogoye ambapo yeye ananielewa nikisema hivyo, kuelekea kwenye shamba lake kubwa pale watutengenezee barabara pale. Siku Mheshimiwa Rais atataka kwenda kule, mbadala watatumia *helicopter* kumbe wanakimbia kwenye ule mlima. Hebu nimwombe atazame ule mlima, aone namna bora ya kushirikiana yeye na TAMISEMI kuweza kuuweka vizuri ili mazao yetu yaweze kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la muhimu kabisa nimwombe Mheshimiwa Waziri atusaidie wakati akijibu hapa, wamefikia wapi kutengeneza ile Wakala ya Ugani ambayo Mheshimiwa Rais ameiagiza. Tunaomba tupate majibu, tuone hatua ambazo wamezifikia ili kuweza kuongeza *speed* ya usimamizi wa wafanyakazi hasa Maafisa Ugani ambao wanasimamia kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kuhusu stakabadhi ghalani. Kwetu sisi hapa panahitaji elimu. Watu wakielewa, wakaona wananufaika, watasimamia wenyewe. Ukiona mahali watu wanakataa kitu, siyo

wanakataa kitu kizuri kwa sababu ya ujinga, wanakataa kwa sababu hawakifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tufahamisheni na sisi siku moja tusimame tuzungumzie kama Mtwara wanavyozungumza, tuzungumze kama Lindi wanavyozungumza na sisi tuwatoe wakulima wetu kutoka Kata ya Manda, Mpwayungu, Makamo waende wakajifunze namna ambavyo wenzetu wananufaika na hiyo stakabadhi ghalani, lakini kutueleza tu kwamba kuna stakabadhi ya ghala bila watu kujua manufaa yake hii nayo inaleta tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ninawatakia kila la kheri. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Livingstone Lusinde. Nilimtaja Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla na Mheshimiwa Ester Bulaya wajiandae.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana ambayo ina jumla ya kiasi cha fedha trilioni 1.24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo kwa kweli Taifa letu limekuwa likisonga mbele pakubwa sana katika maendeleo hasa katika Sekta hii ya Kilimo kwa sababu imekuwa ikipewa kipaumbele sana katika hii Awamu ya Sita na hasa kwa kutengewa fedha nyingi za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia *performance* kubwa sana katika eneo la kilimo na hasa katika hii Miradi mikubwa ya *BBT* ambayo kwa kweli tumekuwa tukizalisha vijana wengi ambao sasa wameanza kusaidia katika Sekta ya Kilimo, hasa huko wilayani ngazi za chini sana; wamekuwa msaada mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu kwa kweli tunaamini kama utasimamiwa vizuri; na ninampongeza na kumsisitiza Mheshimiwa Waziri kwamba aongeze juhudi ya kuhakikisha uzalishaji wa vijana hawa uendelee kwa sababu ndiyo msingi mkubwa wa mafanikio katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri Bashe, Naibu Waziri Mheshimiwa Silinde, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watumishi wote ambao kwa kweli kimsingi wamekuwa pamoja kabisa kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwanza kuzungumzia eneo la pamba. Mimi ninatoka Mkoa wa Shinyanga ambao ni mkoa wa pili katika uzalishaji wa pamba. Kimsingi unapozungumza Shinyanga uzalishaji wa pamba unazungumzia Wilaya ya Kishapu. Pamba yote inayozalishwa katika Mkoa wa Shinyanga 75% inatoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. Kwa hiyo, unapozungumza pamba Shinyanga maana yake unazungumzia Wilaya ya Kishapu ambayo ni Jimbo la kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka tu niseme zipo changamoto hasa katika masuala ya pembejeo, lakini kwa bahati mbaya sana ni utaratibu tu. Pembejeo inatoka lakini inatoka katika utaratibu wakati mwingine si mzuri na hasa viuatilifu (dawa za kuua wale wadudu na mbegu kwa ajili ya kilimo) na mbegu kwa ajili ya kilimo zinafika si katika wakati mzuri. Mbegu zinatakiwa zifike mapema kuanzia mwezi Agosti katika msimu wa pamba kwa sababu msimu wa kilimo unaanza mwezi Oktoba, ndipo tunapoanza maeneo ya kwetu huko Kishapu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri mbegu ziwe zinafika mwezi Julai na mwezi Agosti uwe ni mwezi wa mwisho. Pia, mbegu zile zitolewe kwa mujibu wa ile *allocation* iliyotolewa katika kila eneo kulingana na takwimu za idadi ya wakulima na ukubwa wa maeneo ya mashamba kwa sababu napo pamekuwa na tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukifika mahali mbegu zenyewe inabidi tena uombe ombi maalum la kuomba maeneo ya kata kadhaa ziongezewe mbegu, *as if* kama hakuna takwimu katika Idara ya Kilimo. Kwa hiyo, eneo hili ninafikiri wawe *smart* zaidi ilimradi mbegu ziwe za kutosha kuanzia mwanzo wa msimu mpaka mwisho wa msimu. Kwa hiyo, eneo hili ninaomba lizingatiwe sana ilimradi tuwasaidie wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa viuatilifu kumekuwa na tatizo kubwa sana. Kuna wakati pamekuwa pakitokea upungufu mkubwa wa dawa hizi kwa ajili ya kupulizia wadudu waharibifu. Kwa hiyo, hili jambo linatakiwa na lenyewe lisimamiwe, dawa ziwe za kutosha na ziwafikie wakulima kwa usahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita hasa kupitia Mheshimiwa Waziri kwa usimamizi mzuri sana wa hii Wizara ya Kilimo kwa namna ambavyo kwa kweli udhibiti sasa umekuwa mzuri. Dawa zinafika za kutosha isipokuwa ule wakati, ninaomba sasa jitihada hizi ziendelee kwa sababu wakulima wameanza kuona manufaa makubwa. Sisi tunasema ruzuku ambayo imekuwa ikitolewa katika dawa na mbegu inasaidia sana kuongeza ari ya wakulima kuendelea kulima zao la pamba. Kwa hiyo, hili nilitaka nilisisitize sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nilitaka nizungumzie suala zima la bei ya mkulima wa pamba. Bei hii siyo nzuri, tupo shilingi 1,100 na 1,200. Bei hii siyo nzuri. Zao la pamba lina mchakato mrefu sana katika kuliandaa kwenye kilimo kuanzia kuandaa shamba, kuja kupalilia, kuna masuala ya kunyunyuzia dawa, kuna masuala ya mavuno, ni gharama kubwa sana. Mheshimiwa Bashe wewe bahati nzuri unatoka kanda ambayo tunalima pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ekari moja tunapata kiasi kidogo sana cha fedha, lakini huwezi ukaamini ni kwa nini Serikali yetu tumekuwa tukilizungumza suala zima la kutengeneza kwanza, mjengeko wa bei na pia kuhakikisha kwamba tunatengeneza namna ya kulinda bei ya zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishasema kwamba tutaanzisha Mfuko wa Kulinda Zao la Pamba, lakini jambo hili limekuwa halitendeki. Mwaka kila mwaka tukizungumza halitekelezeki. Ninakumbuka yeye mwenyewe wakati hajawa hata Waziri moja kati ya jitihada zake ambazo alikuwa anazizungumzia ni suala zima la kumlinda mkulima kwa kutengeneza namna nzima ya kulinda bei ya zao la pamba, lakini jambo hili halifanyiki. Ninaomba sana jambo hili lifanyike haraka. Wachakate, wafanye utaratibu wa namna yoyote ambayo itasaidia sana kuhakikisha kwamba, *stabilization* ya *price* ya zao la pamba inakuwepo, kwa maana ya kuhakikisha kwamba tunalilinda hili zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nilitaka nilizungumzie ni suala zima la *ginnery*. Tuna *ginnery* ya Mhunze ambayo ni ya muhimu sana. Mheshimiwa Waziri aliahidi mwaka wa fedha uliopita kwamba, angetusaidia fedha upande wa *SHIRECU* ilimradi *ginnery* hii tuiponeshe, tuweze kusaidia pamba inayovunwa katika eneo la Kishapu izalishwe pale. Kiwanda hiki kinaenda kusaidia hata masuala ya ajira kwa watu wetu wa Mji wa Mhunze na kuuchangamsha Mji wa Mhunze pamoja na kupunguza tatizo la ajira katika Wilaya yetu. Ninaomba sana eneo hili alitazame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake kwa kweli ninamsifia sana Mheshimiwa Waziri, alizungumzia mambo mengi sana. Sisi tunasema katika Wilaya Kishapu tumefanikiwa pakubwa sana. Alituletea matrekta 22 na yametusaidia sana katika Wilaya yetu katika kuhakikisha kwamba kilimo cha pamba kinakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pia amemsaidia sana mkulima. Tunampongeza sana na kwa kweli Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hatutaweza kuisahau katika Wilaya ya Kishapu kwa sababu sasa tunalima pamba kwa bei ya shilingi 35,000 kutoka shilingi 70,000. Tumpe nini Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasema 2025, mwaka huu, majibu watakwenda kuyaona katika Wilaya ya Kishapu.

Tunaomba tu, Mheshimiwa Waziri, matrekta haya yaendelee kubaki kusaidia katika kusukuma uzalishaji wa zao la pamba katika Wilaya yetu ya Kishapu. Mheshimiwa Waziri, nilikuwa ninataka nizungumzie, nimekusikia katika suala zima la uuzaji wa *godown* la *SHIRECU,* ambalo liko kule Kurasini, Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili *godown* kwa mwaka mmoja linatusaidia karibu shilingi milioni 900 kwa kodi tunazopata kutokana na ukodishaji kwa mwaka mzima. Zaidi ya shilingi milioni 900 ambazo zimesaidia *SHIRECU* kutembea, walau kuwa na uhai kwa sababu, hatuzalishi pamba. Sasa kwa sababu, nimesikia katika hotuba ya Waziri ameweka utaratibu wa kutaka kuuza *godown* lile, basi baadaye fedha zile zisaidie upande wa *SHIRECU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, kwanza ushirikishwaji ufanyike ilimradi tuweze kutoa tafsiri nzuri kwa sababu, maneno ni mengi. Tuko Wabunge tunaotoka Mkoa wa Shinyanga, nina hakika akituhusisha tunaweza kusaidia na hasa eneo lile linalozalisha pamba.  Pia, ninafikiri tathmini ifanyike vizuri kwa sababu, *godown* lile tunaweza tukapata fedha nyingi sana, kama kweli litauzwa. Maana *evaluation report* ikishakuwa imetoka, tuone kama faida ipo ama haipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu zile zizingatiwe katika suala zima la uuzaji wa mali ya wakulima kwa sababu, lazima Mkutano Mkuu wa Wanachama uridhie na ukubaliane kwamba, kuna haja ya kuuza, baada ya maelezo na sababu za msingi zitakazokuwa zimetokea. Vinginevyo ninaona ni *godown* ambalo limekuwa likitupa fedha nyingi sana, zaidi ya shilingi milioni 900 na ninadhani kwa mwaka unaokuja 2026 tutakwenda kuwa tunapata, kwa kodi tu, shilingi bilioni moja kwa mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninafikiri tutapata wakati mzuri wa kutueleza hata sisi wawakilishi kujua umuhimu wa kuuza *godown* lile ilimradi lilete manufaa kwa mambo mengine. Vinginevyo tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yako nimeona kuna magari 44 unaenda kuyatoa; ninashauri sana

Wilaya ya Kishapu kwa sababu, ni wilaya ya kimkoa katika uzalishaji, kama inabeba 75%, ninaomba katika suala zima la ku-*allocate* hayo magari Wilaya ya Kishapu ipate gari moja kwa sababu, ni eneo kubwa sana lile la uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Vyama vya Msingi 88 sasa, si jambo dogo. Kwa hiyo, ninaomba katika yale magari kwa kweli, Waziri aelekeze Wilaya ya Kishapu, ilimradi kuongeza nguvu ya uzalishaji wa zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, nikutakie kila la heri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. Ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniphace Butondo.

Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi na Mheshimiwa Neema Lugangira wajiandae.

Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa muda huu. Nianze kwa kumpongeza Waziri wetu wa Kilimo pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambazo wamefanya. Mimi nimekuwa kwenye Sekta ya Kilimo tangu nikiwa kijana mdogo, kuanzia mwaka wa 1975 mpaka mwaka wa 2020 nilivyostaafu na kuja kwenye siasa. Nimeona mambo mengi sana, nikiwa kama mtumishi katika Wizara ya Kilimo na niseme ukweli nimepitia Marais wote ambao wameiongoza nchi hii, kuanzia Hayati Mwalimu Nyerere mpaka kwa Dkt. Mama Samia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa viongozi wetu hawa walikuwa na utashi mzuri wa kisiasa wa kukiendeleza kilimo na

kumwondolea mkulima umaskini, lakini Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na utashi wa kisiasa alikuwa na kitu cha ziada na anacho, anafanya kwa matendo. Ninasema hivyo kwa sababu, Rais wetu huyu ameongeza bajeti ya Wizara hii kutoka kule ilikokuwa aliposhika madaraka, mpaka ikafikia *1.2 trillion*. Hiki ni kitu kikubwa amefanya Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amemteua pia Waziri ambaye yuko makini kimatendo, anafanya kazi na zinaonekana. Ninaona hapa wamejiandikisha watu 65 kuchangia na ninajua wengine wamekatwa; kila mtu alitaka aseme kitu kuhusu Wizara ya Kilimo na utendaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha tatu, amemteua mshauri wake mkubwa kabisa wa kilimo, mtoto wa mkulima, Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Mizengo Pinda, anamshauri mambo ya kilimo nchi hii. Ameteua Wenyeviti wa Bodi na ma-*CEO* ambao wanafanya kazi na tunaona mambo yanakwenda. Sisi tumpe Rais wetu maua yake kwa haya matendo makubwa ambayo ameifanyia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna nukuu moja ametoa, ambayo imeugusa moyo wangu na mioyo ya Watanzania wote. Ninaomba nimnukuu: "Hatuwezi kuuondoa umaskini, kama hatuwezi kuwaondoa wakulima wadogo kwenye umaskini". Hili ni jambo kubwa na ndiyo *commitment* ya hii Wizara, Waziri wetu na wasaidizi wake kwenye kuondoa umaskini katika nchi hii. Niendelee kumwomba Waziri, kamata hapohapo tumsaidie mkulima mdogo aondokane na umaskini, fadhila zake atazipata kule juu mbinguni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kabla sijaanza kuchangia nimpe ombi Mheshimiwa Waziri. Kwenye jimbo langu nina Skimu ya Umwagiliaji ya Mabogini pale, ilijengwa miaka ya nyuma, imeshachoka sana, inahitaji iboreshwe watu wapate maji mengi na tuendelee kuzalisha mpunga kwa uhakika. Hii ni skimu ya uhakika ya mfano hapa nchini, imechoka tunamwomba aje atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Mandakamnono, ninashukuru inaendelea. Tukazanie ujenzi ili iishe, wale wakulima waanze kuzalisha mpunga pamoja na kuboresha ile Skimu ya Makeresho. Tunaomba waendelee kutusaidia, ikiwepo ile Skimu ya Arusha Chini, ambayo Waziri alishatuma wataalam wakaja kule, lakini bado haijaingia kwenye mpango. Ninamwomba chonde chonde tusaidiane, ikiwa ni pamoja na kuboresha mifereji ya asili na kupatiwa miche ya ruzuku ya kahawa. Bado wakulima wa Mkoa wa Kilimanjaro wanahitaji miche ya kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya ombi nianze kutoa ushauri. Ninataka nichangie tu ni nini kifanyike, ili Sekta ya Kilimo iweze kumwondolea mkulima umaskini. Tuweke mkazo kwenye vitu vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza, nitasema bajeti iongezeke. Ninakubaliana na Profesa Muhongo kabisa kwamba, Malabo walipokaa Viongozi wa Nchi mwaka 2003 na Maputo 2014, tulikubaliana chini kabisa iwe 10%. Sasa hebu tujiulize, tukimpa Mheshimiwa Bashe na jeshi lake 10% ya bajeti, ambayo ni karibu shilingi trilioni 5.5 na siyo kwamba tunashindwa, ni nini kitatokea nchi hii kwenye Sekta ya Kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwa kuwa, Rais wetu ana utashi wa kimatendo pamoja na wa kisiasa kumsaidia mkulima, hii bajeti iongezwe. Nitatoa mfano, kule Israeli walipopata tu uhuru, 30% ya bajeti yao ilikuwa kwenye kilimo na leo tunaona Israeli ni Taifa kubwa linalolima kwa wingi, pamoja na kwamba, nchi ya Israel inaingia mara 42, Israel 42 ndiyo Tanzania yetu, lakini ni *giant* wa kilimo duniani kwa sababu, waliwekeza vizuri kwenye kilimo. Kwa hiyo, niiombe Serikali itafakari na kuiongezea hii Wizara pesa. Bado hii shilingi *1.2 trillion* haitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili, ni kuimarisha ushirika. Ushirika ni *component* muhimu sana. Hata kule Israeli walipokuwa wameanza kuboresha kilimo waliunda vyama vya ushirika vya wakulima au wakawaunganisha wakulima wadogowadogo na wale wakubwa, wakawawezesha wapate

nguvu ya kuzalisha pamoja kwa wingi na nguvu ya kwenda sokoni ku-*negotiate* bei; ninajua tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano *BBT*; vile vikundi vyote tuviboreshe, tuviweke kwenye ushirika na yale mazao ambayo bado hayajaingia kwenye ushirika. Tuwaweke pamoja, waweze kuuza mpunga pamoja, mahindi pamoja, maharage pamoja, kama ilivyo kwenye kahawa, korosho, tumbaku na kadhalika. Tukifanya hivyo tutakuwa tumewasaidia sana wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kusema hilo ninaomba niseme, Mrajisi wa Ushirika na yule Mkaguzi wa Ushirika waongezewe pesa. Bado wana kazi kubwa ya kufanya kuisaidia Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa tatu ni, kuna pembe tatu maalum, ishara inayofahamika. Ninaomba waniangalie vizuri; hapa katikati iko Serikali, pale juu yuko mkulima, ambaye ndiye tunamhudumia, huku kuna utafiti, pembe ya chini huku kulia kuna utafiti, pembe ya kushoto kuna ugani. Sasa, hiki kitu Serikali ikiwaangalia watafiti vizuri, wakawekeza vizuri kwamba, watafiti wazalishe teknolojia, halafu watu wa ugani, kama alivyoongea Mheshimiwa Lusinde, wakawa chini yako uwe unawaangalia mwenyewe wapeleke teknolojia huku juu kwa wakulima, huo mzunguko tutafanikisha vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba tuendelee kuwekeza kwenye utafiti. Ugani umejitahidi, japokuwa hawako kwa Mheshimiwa Waziri, lakini amewapa hata pikipiki na vitu vingine, ili wafanye vizuri waweze kusaidia kupeleka teknolojia kutoka kwa watafiti kwenda kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mwisho ni, Msaada wa Kimataifa; tukipata pesa tupeleke kwenye umwagiliaji, Israeli walifanya hivyo. Ninatoa mfano wa Israeli kwa sababu, ni nchi ndogo na imefanikiwa sana. Waliwekeza kwenye maji, wakajenga bomba la urefu wa kilometa 250 kutoka Galilaya

mpaka kwenda kule Kusini kwenye jangwa. Baada ya watu kupata maji kule, Israeli, ndiyo tunaona mafanikio yaliyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, pamoja na kazi nzuri wanayofanya kui-*support* Tume ya Umwagiliaji, bado pesa ya ni ndogo, tuwaongezee pesa. Tuna mtendaji mzuri sana na Mwenyekiti wake wa Bodi, mzuri. Ni hakika tukifanya hivyo mambo yatatunyookea, mkulima umaskini utamwondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninawapongeza sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mchangiaji anayefuata, tuna tangazo moja hapa la kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni; Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, atakuwa nje ya Mkoa wa Dodoma kwa shughuli za kikazi. Kwa hiyo, wakati atapokuwa hayupo Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, atakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni hadi atakaporejea Mheshimiwa Waziri Mkuu au atakaporejea Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Nilimtaja Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Neema Lugangira na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara ujiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kabla sijaanza kuchangia napenda ku-*declare,* mimi ni mkulima wa parachichi. Zao la parachichi; maji, mbolea na miche ya uhakika; bajeti ya mwaka jana walituambia watatoa ruzuku ya miche, nimeiona lakini siyo kihivyo. Wakulima wadogo wa parachichi wanahitaji maji ya uhakika, ili waweze kupanga msimu wao wenyewe wa mavuno. Tunahitaji *pack house* wakulima wa parachichi; ninazungumzia

wa Njombe hapa na mimi ni mkulima mdogo tu wa Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaanza kuchangia. Nimewasikiliza Wabunge wengi wakichangia hapa. Ni kweli kabisa hawa vijana wawili, mimi ninawaita wazazi, wanafanya kazi nzuri na wametengeneza *confidence* kwa wakulima. Kama ambavyo humu ndani sasa hivi hatusikii kelele za kwenye madini kwa sababu, msingi wake Mheshimiwa Dkt. Biteko alitengeneza hiyo *confidence,* lakini mbali na mipango hii mizuri hapa waliyonayo, mbali na bajeti ya Kilimo kutoka shilingi bilioni 200 mpaka shilingi trilioni 1.2, pesa hazitoki zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, simwoni Waziri wa Fedha hapa! Kazi yetu sisi ni kuibana Wizara ya Fedha kupeleka pesa kwenye maeneo nyeti yanayogusa watu wengi. Leo bajeti ya mwaka huu 2025 tusingezungumzia tena shilingi trilioni 1.2, ingetoka yote tungewaza kuongeza iende ikasaidie Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitisha, mwaka jana 2024, shilingi trilioni 1.2, imetoka shilingi bilioni 664, sawa na 33%. Kwa nini sasa miradi ya umwagiliaji utekelezaji wake isiwe 27% sijui 28%? Kwa nini miradi mingi ya kilimo isikwame kwa sababu, hakuna pesa za kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo yanagusa watu wengi kwenye nchi hii. Kilimo, tunasema kinaajiri zaidi ya 70% ya Watanzania, huko tunatakiwa tuweke pesa za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia Wizara ya Afya, pesa zake zinatakiwa ziende vya kutosha. Unapozungumzia Wizara ya Maji pesa zinatakiwa ziende za kutosha. Kuna maeneo ya kimkakati yanamgusa Mtanzania mdogo, lazima tuweke pesa za kutosha. Haya, leo wao wana ndoto ya kumsaidia mkulima mdogo, hatuwapelekei pesa, hiyo ndoto itatekelezeka vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira njema kabisa na ni kweli, ndiyo Wizara ambayo inafanya nchi itulie, Wizara ambayo

inalisha Taifa. Hatuipelekei pesa Wizara ambayo inaajiri, inatengeneza ajira, hatuipelekei pesa! Tunapeleka 53%! *Serious*? Si bora hata ingefika 70% au 80%? 53%, kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, lazima tuibane Wizara ya Fedha, ili haya malengo mazuri, ambayo yamewekwa na hii Wizara yatimie, ili hao akinamama ambao wanasomesha watoto kupitia kilimo wafanikiwe. Haya yote yanadhihirika, pale kwangu Bunda, waliahidi kutuchimbia visima 150, lakini wameweka kwenye mpango Kisima kimoja tu cha Misisi, Kata ya Sazira, vingine vimekwama. Siwalaumu, hawana hela, lakini lazima niwadai kwa sababu, wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini wamenituma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Bwawa la Bitaraguru linahitaji ukarabati. Wakilikarabati lile bwawa ambalo linahitaji shilingi milioni 150, kuna *project* ya Kilimo cha Bustani ekari zaidi ya 200, zinazofanya kazi ni ekari 50 tu, haya ni lazima tuyaseme. Dhamira ni njema, ndiyo maana wakatutengea hivi, lakini pesa haziendi, watafanyaje kazi? Lazima tuhakikishe Wizara ya Fedha inapeleka pesa kwenye maeneo nyeti ili Watanzania wawe na uhakika na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimezungumzia hapohapo visima 150, nimezungumzia Bwawa la Bitaraguru, lakini Wizara ilienda kufanya *research* kwenye Kata ya Wariku kwa sababu ya kuwekeza, lile eneo ni *potential* kwenye miradi ya umwagiliaji. Umepita mwaka mzima hakuna kinachoendelea. Kata zangu saba zile za vijiji watu wanajihusisha na kilimo na wao wametambua, tunaomba utekelezaji wake tuuone kwenye Jimbo la Bunda Mjini, ili wananchi waweze kutumia kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mabwawa mengi tu yanahitaji ukarabati; kuna Bwawa la Kisangwa, Bwawa la Gushigwamara na Bwawa la Kinyambwiga, haya yote yakikarabatiwa wananchi wa Bunda watanufaika na kilimo cha umwagiliaji. Mheshimiwa Bashe anajua, Bunda pale tuna *ginnery*

tano, zinazofanya kazi ni *ginnery* mbili tu, nyingine zote zimekufa. Hizi zikifufuliwa zitasaidia ajira kwa vijana na akinamama wa Jimbo la Bunda Mjini, mwanzo zilikuwa zinafanya kazi. Tunaomba watufufulie *ginnery* hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa nilizonazo Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Mara kiliomba mkopo wa shilingi bilioni 3.7, kwa ajili ya kufufua *Ginnery* ya Ushashi, lakini mpaka sasa hivi hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni, Mheshimiwa Bashe, tuna *AMCOS* tatu; ya Butakale, ya Kinyambwiga na vilevile ya Kinyambiga, hizi zote hazina maghala. Kikifika kipindi cha mavuno wanakodi, unaweza ukakuta mtu anakodi ghala kwa shilingi laki tatu/nne wakati amepata mavuno ya shilingi milioni ya pamba. Tunaomba *AMCOS* hizi zipate maghala, ili ziepukane na hasara ya kwenda kukodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia Mheshimiwa Butondo, zao la pamba limeporomoka, wakulima wa pamba hawaridhiki na hii bei elekezi. Kuna kipindi tulifika shilingi 3,000 leo ni 1,100. Wakulima wa pamba wanatumia gharama kubwa kwenye maandalizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia pamba; Mheshimiwa Bashe, ametoka Kanda ya Ziwa, anaelewa; na mzazi mwingine Silinde hapo hata kama hawalimi pamba, yeye yupo wizarani, tunaomba watusaidie zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna chuo pale cha wanyamakazi kipo Serengeti Kata ya Mcharo ni chakavu, kina ekari kama 25 hivi. Kile chuo wakikiboresha kitakuwa na uwezo wakutoa mafunzo kwa wataalam zaidi ya 20,000 kwa mwaka waweze kujifunza ni namna gani wataweza kutoa mafunzo kwa wakulima kulima kilimo cha kisasa. Chuo ni chakavu sana, sana. Wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini tunaomba sana wakarabati hiki chuo na sisi wakulima wa Jimbo la Bunda Mjini wapewe elimu ya kulima kilimo cha kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Maafisa Kilimo Wizara yangu; *I mean* idara yangu ya kilimo wana uhaba wa vitendea kazi. Ili waweze kutimiza majukumu yao mazuri tunaomba visima, miradi ya umwagiliaji; nimesema hapa kuhusu ukarabati wa Chuo cha Wanyamakazi, ukarabati wa mabwawa Bunda Mjini na maghala kwenye *AMCOS. Ginnery* zifanye kazi ili uchumi kupitia sekta ya kilimo kwa wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini uimarike, na sisi tuone kilimo kuwa ni sawa na kazi zingine. Kwa kweli wanafanya kazi kuna mzazi nyuma hapa ameninong'oneza, anasema anashukuru sasa hivi lile wazo lake la *BBT* linakwenda vizuri. Ninakushukuru. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya. Nilimtaja Mheshimiwa Neema Lugangira, Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara na Mheshimiwa Condester Sichalwe, wajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa fursa ya kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. Nianze kwa kusema kwamba ninaunga mkono hoja; na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mageuzi makubwa ambayo ameyafanya katika sekta hii ya kilimo, mageuzi ambayo yanatambulika ndani na nje ya nchi. Halikadhalika ninampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Waziri Bashe, Mheshimiwa Naibu Waziri kaka Silinde, Katibu Mkuu na viongozi wote wa wizara hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika kuhakikisha kwamba tunaleta mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo ambayo ndio uti wa mgongo wa uchumi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kuipongeza sana Serikali chini ya Wizara ya Kilimo kwa kutambua mbegu za asili, ambayo imekuwa ni moja ya hoja zangu katika Bunge hili. Ninapongeza pia uamuzi wa kujenga *seed bank* kubwa, kwa maana ya *gene bank* hapa Tanzania, ambapo Tanzania itaungana na nchi kama za Norway ambazo zina *gene bank* kubwa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi ninaomba niishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunayo sheria ya mbegu ambayo kwa bahati mbaya inatoa haki ya wauzaji wa mbegu wakubwa; hivyo kuna haja kwa sheria hii kufanyiwa mapitio ili kuhakikisha kwamba sheria hii inatoa pia fursa na itambue umiliki na usimamizi wa mbegu za asili, kwa maana ya mbegu ambazo zinamilikiwa na wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika tunahitaji sera ya mbegu; sera hii ya mbegu ifanyiwe maboresho ili iweze kutambua namna ambavyo mbegu za asili zitasimamiwa na zitalindwa; na pia namna ambavyo hazitafifishwa kutokana na mikataba ya kimataifa iliyopo, ambayo inatoa upendeleo zaidi kwa mbegu za kisasa zinazozalishwa na wazalishaji wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ikamilishe mchakato wa *NPGRFA* ambao umeanza kutoka mwaka 2007, kwani kwa kufanya hivyo tutaweza kulinda haki za wakulima na pia tutaweza kulinda haki za mbegu za asili. Kwa kufanya hivyo Tanzania tutakuwa tunatekeleza mikataba ya kimataifa ambayo tumeridhia ambayo inalenga kulinda haki za wakulima ambayo ipo chini ya *UNDROP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali itajenga *seed bank* kubwa, kwa maana ya *gene bank,* nitumie fursa hii kuisisitiza sana Serikali chini ya Wizara ya Kilimo, kwamba ni lazima itenge fedha ili iwekeze na tuhakikishe kuwa tunakuwa na *seed bank* katika ngazi ya vijiji, kwa sababu ni muhimu sana kulinda mbegu za asili ngazi za vijiji. Tayari tumeshaona mifano mizuri kupitia wadau wa *SWISS AID* wako na *seed bank* ambazo wameanzisha pale Lindi, wadau wa *Iles de Paix (IDP)* ambao wameanzisha *seed bank* pale Arusha pamoja na Mkoa wa Manyara. Hivyo, nitumie fursa hii kusisitiza sana Wizara ya Kilimo, pamoja na kwamba tutajenga *seed bank* kubwa ya kitaifa ni lazima tuwekeze pia katika kujenga hizi benki za mbegu za asili kwa kuanzia walau kila mkoa uwe una mbegu za asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kusema, kwamba mbegu hizi za asili zina uwezo mkubwa sana wa kuhimili ukame, zina uwezo mkubwa sana wa kuhimili magojwa. Hivyo

tutakavyozidi kuhakikisha tunatumia na tunalinda mbegu zetu za asili tutaweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; jambo ambalo litaendelea kuwaweka wakulima wetu salama, lakini pia litapunguza utegemezi wetu kwenye mbegu za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu suala la mbegu ni suala pia la kidiplomasia, suala la mbegu pia linaweza likatumika katika kuleta athari ya usalama wa kitaifa. Kwa hiyo ni muhimu sana niendelee kusisitiza tuzilinde mbegu zetu za asili na tuhakikishe kwamba wakulima wetu wanalindwa na kunakuwa kuna nguvu ya ziada katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na hizi benki za mbegu za asili katika mikoa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo mbegu hizi za asili zina mchango mkubwa sana katika kuchangia kupunguza matatizo ya lishe, kwa sababu tafiti zimeshathibitisha kuwa mbegu za asili zina madini joto mengi, zina madini chuma mengi, zina protini nyingi pamoja na vitamini mbalimbali tofauti na mbegu za aina nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaendelea kuishukuru sana Serikali kwa kutambua na kuweka ulinzi juu ya mbegu za asili. Hata hivyo, niendelee kusisitiza, kwamba ni lazima sheria zifanyiwe maboresho kama ambavyo nimeshaeleza, lakini pia lazima tuwe tuna benki za mbegu za asili kwenye mikoa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijahitimisha nigusie hoja yangu nyingine ya kudumu katika Bunge hili kuhusiana na zao la *vanila*. Ninatambua kuwa Serikali chini ya Wizara ya Kilimo imefanya jitihada kubwa sana katika soko hili la *vanila*; lakini nikiwa ninatokea Mkoa wa Kagera bado wakulima wetu wa zao la *vanila* Mkoa wa Kagera bado wanahitaji Serikali iangalie zao hilo kwa jicho la kipekee kutokana na fursa ya rasilimali fedha inayoweza kuleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie fursa hii kuiomba sana Wizara ya Kilimo kupitia mamlaka yetu ya *COPRA* isimamie vizuri zao hili la vanila ili tuweze kupata soko. Wakulima wetu kilio kikubwa ni soko. Ninatambua kuwa chini ya dada yangu Irene

zipo jitihada kubwa ambazo zinafanyika za kuhakikisha kwamba tunapata soko la *vanila* nchini Japan pamoja na China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitano hii nimekuwa nikiongelea zao la *vanila*; bado hatujafikia kuliona hilo soko. Niombe sana tuweke kipaumbele katika zao hili la *vanila* ili wakulima wa zao hilo Mkoa wa Kagera waweze kunufaika na zao hili ambalo litakuwa na mchango mkubwa sana katika kuchangia fedha ambazo zitatokana na mchango wa sekta hii ya kilimo.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatokea wapi? Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**TAARIFA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninataka kumpa taarifa Mheshimiwa ambaye anachangia vizuri kuhusu zao la *vanila*. Zao hili kuna kipindi lilifika kilo moja 120,000; lakini kutokana na kwamba mazao ya *vanila* mengi yanaingizwa kutoka nje ya nchi bei hapa kwetu imeshuka. Kwa hiyo nilikuwa ninampa taarifa tu kwamba, mchango wake ni mzuri, asisitize kwamba tuzuie mazao ya *vanila* yanayoingizwa nchini ili *vanila* yetu ipande bei.

**MWENYEKITI:** Unaipokea taarifa hiyo Mheshimiwa Neema?

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Saashisha. Ninaendelea kusisitiza Serikali iweke jitihada kubwa kwenye zao la *vanila* kwa sababu hili ni zao la kimkakati. Ninatambua namna ambavyo kaka yangu Mheshimiwa Waziri Bashe anaendesha shughuli zake, ni mzee wa vitendo ni kaka wa vitendo. Hivyo basi hata na sisi katika zao la *vanila* tuone vitendo hivyo kupitia matokeo chanya kwa kaka yangu Bashe ili tupate soko la uhakika la *vanila*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe pia kwa kusisitiza, tunapoongelea maendeleo ya sekta ya kilimo hatuwezi kuacha watafiti wetu, wanasayansi wetu katika kukuza sekta hii ya kilimo. Watafiti wana nafasi kubwa sana, hivyo niombe sana... *(Makofi)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olelekaita.

**TAARIFA**

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpe dada yangu, taarifa hapa. Anavyozungumza habari ya watafiti, Profesa Patrick Ndakidemi, kwenye *journal* ya watafiti wanaoheshimika duniani ni namba mbili Tanzania; lakini inapokuja kwenye wataalam wa kilimo nchi hii ni namba moja ana *point* 56 na anayemfuata ana 41. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea sana taarifa hiyo na ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza sana mzee wangu, baba yangu Mheshimiwa Profesa Ndakidemi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pale ambapo nilipokuwa nimeishia; pamoja na uwekezaji mkubwa unaofanyika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ni lazima iwekeze fedha za kutosha katika tafiti ili wanasayansi wetu waendelee kufanya kazi iliyobora, ambayo pia itajumuisha kutafiti hizi mbegu za kisasa ambazo tunaletewa, kwamba zinakuwa zina madhara au zinakuwa zinatija pamoja na kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nirejee tena kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyofanya, nirejee tena kumpongeza kaka Bashe kwa kazi kubwa anayofanya na nisisitize umuhimu wa kuwa na benki za mbegu za asili katika mikoa yetu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Lugangira.

Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, wajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Nami nichukue nafasi hii kupongeza sana Wizara ya Kilimo, watoto wa mjini wamesema kwa kweli sasa hivi Kilimo kumechangamka. Kumechangamka kwa sababu Waziri mnafanya kazi vizuri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu rafiki yangu anafanya kazi vizuri na Wakurugenzi wote, yaani kunaonekana kila Mkurugenzi anafanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze sana sana kwenye hili eneo la mbolea, Mheshimiwa Bashe anakumbuka ilikuwa shida, nikawa ninakwambia kabisa kwamba Kijiji cha Mdundualo wakanunue mbolea Songea Mjini; walikuwa wanapigwa na kuna wanawake wengine hadi waliugua; lakini leo hii tunavyozungumza vijiji vinapata mbolea. Kwa mfano Kijiji cha Mdundualo yaani wakala yupo pale kijijini, kwa hiyo hakuna tena kusafiri, hiyo ni pongezi kubwa sana. Kama kuna kijiji cha Mheshimiwa Kunti kule basi ni vichache; wawasaidie na wao wapate mbolea kama wanavyopata vijiji vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia ile juhudi ya kupeleka pikipiki kwa wale Maafisa Ugani. Hata hivyo nimwambie Mheshimiwa Bashe, kwamba zile pikipiki haziwafikii wakulima. Ukipiga simu au mkulima anamhitaji yule afisa, anakuuliza una mafuta? Utaniwekea hela? Sasa ninafikiri wajipange kwa utaratibu. Gari anazotaka kupeleka na hizo pikipiki waziratibu vizuri na ikiwezekana sijui kuwe na wakala, *otherwise* watapeleka gari lakini haziwafikii wakulima. Vijana wanapiga *race* mitaani na zile pikipiki. Hilo ninamwambia Mheshimiwa Bashe. Yeye ni rafiki yangu, lakini lazima nimwambie ukweli. Suala la pikipiki lile ninakwambia limebuma, waangalie vizuri, waweke mwongozo

kwenye pikipiki, zinafanya kazi namna gani. Walisema watakuwa wanawafuatilia, hakuna kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwa sababu mimi nikiwaita pia wananiambia. Sisemi kama mimi ni Mbunge, ninasema tu kama mkulima ninahitaji, lakini wanakwambia tuwekee fedha ili tuweke mafuta. Kwa hiyo, ninataka kusema mkulima wa chini kupata huduma na wale maafisa ni shida kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo alituahidi, nimwambie Mheshimiwa Bashe, sijui walitoa mwongozo, maana nilitafuta trekta kulima kule sikupata. Safari hii ninaomba atupangie vizuri mwongozo; tunakwenda wapi sisi wakulima wa chini ili tupate matrekta, tulime kwa hiyo bei. Nimesikia mwenzangu mmoja anasema hapa ni shilingi 35,000, lakini ninakumbuka walituambia 40,000. Sasa *which is which,* ninaomba watueleze vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kusema, kwamba huyu jamaa anayeshughulika na mbolea anastahili maua yake. Nimwombe sasa, Mheshimiwa Bashe ni rafiki yangu, nilimweleza kuwa kuna bonde kule *block farm* kubwa sana. Kwa nini hataki kwenda kutuchimbia kule mabwawa. *Block farm,* lakini si ni mkoa wake ule. Ninaomba, nina ramani hapa nitamrushia Mheshimiwa Bashe, atupelekee bwawa kule ili tulime Mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka kuwa pia walituahidi watatupelekea skimu hizo nane Nyasa; hazipo mpaka leo, hakuna mpaka leo; lakini watu wanafikiria Ruvuma hatuhitaji mabwawa kwa sababu kuna mvua na tulikuwa tunalima sana. Sasa hivi kutokana na hizi tabianchi kubadilika tunahitaji na sisi mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anipelekee bwawa Mdundualo kule. Aliniletea wataalam, ninamshukuru sana; waende Mdundualo ili lile bwawa sasa likafufuke. Sehemu inaitwa Likingu waende kule na sisi tuone mabwawa maana watu wanayasikia tu. Sisi tunayahitaji hayo mabwawa ili tuanze kulima kwa kutumia *Irrigation scheme*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndiyo nianze kuchangia. Nimshukuru sana Mheshimiwa Bashe, anapambana na bei za kahawa pamoja na korosho. Sasa ile bei waliyotuambia ya 4,000 kilo yaani ile ilikuwa mara moja na ndio ikazima. Asimamia palepale hawa wanunuzi wasishushe bei, korosho haiozi. Ile ya shilingi 4,000 tulifurahi sana, lakini ikashuka, ikashuka, hadi ikafika huko kwenye elfu mbili na ushee. Asimamie hizi bei zipande pale; tena awatishie kwamba, kama mnasema zipunguzwe siwauzii korosho, lakini korosho watazinunua tu. Kwa hiyo tunaomba ile bei ibaki shilingi 4,000 kwa kilo; ilifanyika mara moja tu, hiyo nimwambie na Mheshimiwa Bashe analijua hilo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, sasa nakuja kwenye utafiti. Niseme hivi, nipongeze sana kazi inayofanywa na *TARI* na hasa pale Naliendele. Kwenye hii fedha nyingi aliyoipata kwenye bajeti ya safari hii aipeleke bajeti nyingi kwenye utafiti. Wakafanye utafiti kwenye mbegu ili tusipate mbegu *fake*. Zile kampuni zinazouza mbegu *fake* zifungiwe; na kampuni zinazouza mbegu nzuri tutangaziwe ili wakulima wajue kuwa kampuni hii ina mbegu nzuri ya mahindi; zitangazwe zile mbegu nzuri zote na kampuni zao; lakini na wale matapeli watangazwe pia ili mkulima ajue kuwa, nikiona kampuni hii nisinunue mbegu yake. Asiwaonee huruma; mimi ninakwambia wakulima watafurahia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Dkt. Jeradina aliyeko kule Naliendele. Kuna mbegu kule ya karanga, nikasema hivi mbegu hii ya karanga ambayo na mimi nilipanda, je, kule Tabora Kaliua wanaijua? Nachingwea wanaijua? Ruvuma yote wanaijua? Kuna mbegu nzuri mno. Mimi mwenyewe nilishangaa, nimelima kaeneo kadogo tu. Kwa hiyo ile mbegu ninaomba Mheshimiwa Bashe awasambazie mikoa yote wanaolima karanga, watafurahi sana, ipelekwe kule. Vilevile kuna *SUA*, Nelson Mandela, *UD* na Tumbi; hizi ni *Centre* zinazofanya tafiti, hawa wameomba wasaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongea na mkuu wa chuo fulani akasema: *"Tunaomba watushirikishe sana katika tafiti."* Leo hii kuna huu utafiti wa *tissue culture* ya ndizi; hebu wasaidiwe hii *tissue culture* ya ndizi pale Nelson Mandela ili iweze kuwasaidia.

Kwanza wao Nelson watapata fedha na vilevile watasaidia ku-*train* na nchi nyingine na hivyo watapata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *tissue culture* ya ndizi ni biashara nzuri mno. Mheshimiwa Bashe aweke nguvu zake hapa, awasaidie *SUA*, awasaidie na wale Nelson Mandela na *UD* pamoja na Tumbi kwa kuwa wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa *RAS* Tabora, Tumbi kuna zinaitwa pingiri, aliniambia huyu Maige, sijui ni Kiswahili; zinaitwa pingiri, zile za mihogo. Tumbi wana mbegu nzuri za mihogo. Tunaomba; walianza *production* kidogo, lakini tunaomba, wataalam wanisikilize hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba zile mbegu Mheshimiwa Waziri azisambaze kwenye mikoa inayolima mihogo ili kuzuia ile *bleach*, sijui inaitwa *bleach* sijui inaitwa nini. Wanatoa mbegu ambayo ipo *very resistant to disease*. Tusaidieni Ruvuma tunalima mihogo, Tabora wanalima mihogo, hata Kyela kule wanalima mihogo. Kwa hiyo, ile *species* muisambaze. Mimi kuagiza mbegu kutoka kule kupeleka huko kusini ninaweza; lakini mkulima wa kawaida, ninaomba wasambaze hiyo mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka nimwambie Mheshimiwa Bashe, yeye ni rafiki yangu, lakini hili lazima nimwambie, Mheshimiwa Bashe nimemwambia mara nyingi zao la tumbaku linawafaa wakulima wakubwa. Wakulima wadogo kwanza wanachelewa kuwalipa, wakulima wadogo wanakopa sana wengine mpaka wanakimbia nyumba zao. Ninafurahi ananiangalia, anisikilize. Ameniambia kwamba wameweza kupata tani 160,000 sawa, wanapata sijui fedha za nje zinawasaidiaje wakulima wa chini Mheshimiwa Bashe? Nyumba zao mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie hivi, wakishapata zile hela waende wakatengeneze programu ya kuwasaidia wakulima wadogo. Wakulima wadogo afya zao mgogoro, hali zao na nyumba zao mgogoro unazing'ang'ania, amwachie Mheshimiwa Cherehani alime tumbaku, lakini

wakulima wadogo wawape mazao mengine mbona yapo Mheshimiwa Bashe, hili zao wanaling'ang'ania kwa nini? Mimi hapo kwa kweli wewe hautakuwa rafiki yangu, urafiki utapungua kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo basi mimi nikushukuru sana, lakini nimemwambia ukweli. Ninafikiri atakuja na majibu ya kuliondoa taratibu hilo zao la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamtaja mwingine ninaomba niwatangaze wageni ambao wapo Bungeni muda huu.

Tuna wageni ambao wamekaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika; Wageni wa Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo: Ndugu Abdulmajid Nsekela ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Chai, Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika na pia, Mtendaji Mkuu wa Benki ya *CRDB.* Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna ndugu Maregesi Shabani, Mkuu wa Kitengo cha Kilimo na Biashara Benki ya *CRDB;* ndugu Sarah Mabula, Meneja wa Mahusiano, Kilimo na Biashara Benki ya *CRDB.* na ndugu Gideon Mazara, Meneja Mahusiano Taasisi za Serikali Benki ya *CRDB*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo ndugu Chabu Mishwalo, Meneja wa Benki ya *CRDB* Kanda ya Kati; ndugu Imani Tasama, Msaidizi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya *CRDB.* Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Mohamed Bashe. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge: kuna wageni 72 wa Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, ambao ni wanafunzi 64 na Walimu nane wa Shule ya *High View* Kutoka Zanzibar. Karibuni sana, wanafunzi wetu kutoka *High View* Zanzibar. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: tuna wanafunzi 100 na Walimu watano kutoka Shule ya Msingi Feza iliyopo Jijini Dodoma. Karibuni sana wageni wetu. Katika wanafunzi hao 100 kuna mtoto wa Mheshimiwa Jesca Kishoa, anaitwa Darwin Kafulila, atupungie mkono tumwone. Huyo hapo mbele. Karibuni nyote katika Bunge letu kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 50 wa Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma kutoka Chuo Kikuu Dodoma *(UDOPSO)*. Karibuni sana. Karibuni wanafunzi wetu kutoka huko Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Tuna vijana 10 kutoka Taasisi ya *Embassy of Protocol* inayojihusisha na usimamizi wa itifaki na matukio ya kidiplomasia Mkoani Dodoma. Karibuni sana watu wetu hao kutoka huko *Embassy of Protocol. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, wajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kabla sijaendelea na mchango wangu ninaomba ni-*quote* maneno ya Baba wa Taifa, Baba wa Taifa anasema maeneo yafuatayo kwenye kilimo: "*Hatupaswi kusahau kwamba kilimo ni kazi ya heshima tunapaswa kuwathamini wakulima na kuwaunga mkono ili waweze kufanya kazi yao vizuri.*" Maneno ya Baba wa Taifa, Mwasisi wa Taifa hili ambaye aliamini na kuheshimu kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya ya Baba wa Taifa, ninaomba nitumie fursa hii adhimu kuipongeza na kuishukuru sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia ambaye ni Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi amekitendea haki chama chetu, amewatendea haki Watanzania kwa kuonesha na kuyaishi

maneno halisi ya Baba wa Taifa kwamba kilimo siyo kazi ya kudharaulika, kilimo ni kazi ya kuheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninaomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kuendelea kuwahudumia wakulima wote nchini kwetu na kwa kweli tumeona faraja kwa wakulima. Kipekee ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Bashe katika kipindi cha Uwaziri wake amebahatika kufanya ziara kwenye Jimbo langu la Momba, ninamshukuru sana. Kwa hiyo, katika haya nitakayokuwa ninashauri ninajua atakuwa na picha halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, nitakuwa na ushauri kidogo tu kwenye Wizara yetu hii pendwa ili waendelee kuwahudumia wakulima. Mheshimiwa Waziri, katika vipaumbele vyake alivyokuwa amevisoma pamoja na ile mikakati ombi langu la kwanza, nimwombe kama ambavyo ameanzisha *BBT* ninaomba aanzishe kampeni ya kutokomeza Watanzania kulima kwa kutumia jembe la mkono ili tuanze kulima kidigiti. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah! Kaka mimi nitaomba taarifa usome baadaye, nishauri kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani kuona hizo takwimu alizokuwa anazisoma za miaka minne, kwamba miaka minne tumetoka hapa, tumepanda hapa, tumezalisha tani hizi Mheshimiwa Waziri pamoja na jitihada zote hizo ambazo alizisoma hapo mbele zaidi ya Watanzania, 60% bado wanalima kwa kutumia jembe la mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania watakapoanza kulima kisasa watatumia akili kubwa, nguvu kidogo lakini watatumia eneo dogo na watazalisha kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo, ninatarajia tutakaporudi kwenye Bunge la Kumi na Tatu anasoma bajeti kama sasa kama Mungu ataendelea kumpa kwenye hiyo

nafasi au vinginevyo atapandishwa. Tunatamani atusomee takwimu kwamba alikuwa na Watanzania kadhaa ambao walikuwa wanatumia jembe la mkono na sasa hivi siyo tu kuwa wa pili kulima mahindi Afrika, tunatamani kuwa wa kwanza. Hiyo ni kampeni ambayo ninaomba Waziri aweke kwenye vile vipaumbele vyako Watanzania tutoke kulima kwenye jembe la mkono *as we are speaking now* hatuna hata matreka, hayawezi kufika 100 kwenye Jimbo la Momba, sijajua kwenye Majimbo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Mheshimiwa Waziri, mbegu, sitataka kuongea sana kwenye hiki kipengele kwenye suala la mbegu, lakini pamoja na jitihada zote ambazo wamefanya, ninataka nimwachie tu *homework*. Kwa nini, watu wa Nyanda za Juu Kusini bado wanalima na kutumia mbegu ya mahindi kutoka Zambia, kwa nini? Hususan kwenye Mkoa wangu wa Songwe, mbegu zote za mahindi tunachukua Zambia, Zambia wametuzidi kitu gani? Pamoja na mazuri yote ambayo umefanya kwenye mbolea hiyo ni *homework*. Tunapaswa kuzalisha mbegu zetu wenyewe, sisi ndiyo tuwauzie Zambia na Mataifa mengine na yenyewe hiyo itakuwa ni chanzo kizuri cha mapato kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbolea, Mheshimiwa Waziri ninakiri na hata alipotembelea Jimboni kwangu Momba aliona. Kwa kweli hali ya upatikanaji wa mbolea ilikuwa ni changamoto sana na Watanzania wengine ambao wameongeza kipato kwa kutupatia ruzuku za mbolea, lakini Mheshimiwa Waziri kaka yangu kule Wilayani kwetu, sisi tunatoka Wilaya ambayo ipo mpakani, tunakiri vyombo vya dola vimefanya kazi yake vizuri sana ila bado wapo ndani kwako huko kuna shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifumo ya mbolea iwekwe vizuri mbolea bado inatoroshwa kwenda Zambia. Mimi ninatoka Jimbo ambalo pia lipo mpakani pale Tunduma bado kuna shida. Kwa hiyo, ile ruzuku ambayo wametuwekea ili inawezekana sasa hivi mbolea isingekuwa nyingine imevuja huko inawezekana mpaka tunavyoongea. Sasa tungekuwa sisi tumeongoza, tumekuwa wa kwanza katika zao la mahindi, lakini bado ipo mianya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kwamba wapo baadhi Watanzania ambao wanalima upande wa Zambia. Kwa hiyo, wanachukua mbolea yetu wanaenda kulimia upande wa Zambia lakini mbona inapokuja mbegu mbona wenyewe Watanzania wanaenda kununua Zambia kwa pesa kwa nini na wenyewe wasifuate? Kama upo utaratibu wa kuwauzia mbolea kama nchi ili iende ikatumike kwao, lakini siyo mbolea yetu ya ruzuku ambayo Mheshimiwa Rais ameamua kutoa thamani ndiyo iende ikafanye Zambia. Bado kuna matobo, hukohuko ndani kwako, mwone namna ya kuangalia hili jambo lisiendelee tena, lakini nia ya Serikali na nia yako ilikuwa ni njema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikakati yake Mheshimiwa Waziri, vitu ambavyo vingine amevitaja kwamba ni kipaumbele ni pamoja na masoko kwa wananchi kuwatafutia masoko. Mheshimiwa Waziri mwaka jana tulikuwa tunaogopa hata kuonana usoni nikija unasema Condester, ninajua kule kwake changamoto ya stakabadhi ghala. Mimi kama Mbunge kijana nikaamua nichukue hili jukumu nikaenda na yule *DG* wa Waziri anaitwa Bangu, tukazunguka Jimbo zima la Momba kuwaelimisha wananchi umuhimu wa stakabadhi ghalani na kwa kauli yake amekuwa akisema stakabadhi ghalani mkulima anajipangia bei. Sasa Mheshimiwa Waziri Wanamomba wakaitika wakakubali na nikawaambia limeni poleni kwa changamoto ambazo zimewapata tukae kwenye muda wa kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Wanamomba wamelima sana ufuta na kwa bahati mbaya kwa sababu mvua zilikuwa ni kidogo mazao ambayo yanakubali mvua kama mpunga hatujapata, wakapata ufuta. Sasa Mheshimiwa Waziri ikiwa bei ya mwisho mwaka jana ilikuwa 4,000 tunapoongea sasa juzi kulikuwa kuna mnada 2,800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitaomba Waziri atakapokuja kuhitimisha leo jioni atuambie ile hamasa aliyotupa tukubali stakabadhi ghalani, nikaamua kubeba mzigo mwingine wa Waziri mwenye dhamana, ilibidi aje kutoa tamko Wanamomba wakaelewa, sasa hivi Wanamomba wanalia. Wanataka wauze huo ufuta ili waweze kununua mahindi, ili waweze kununua

mpunga bei zipo chini unatuambiaje? Wanamomba hawajui mambo ya *demand and supply* huko duniani, yeye ndiye Waziri mwenye dhamana anatusaidiaje bei za ufuta zipo chini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu skimu za uwagiliaji, ninakushukuru nimepitia taarifa yako yote kwenye mabondeni yote hapa ya kwetu. Bondeni la Kasinde amesema upembuzi umeshakamilika lina hekta 15,000 kwamba upo kwenye manunuzi, kwenye Bwawa la Kamsamba ambalo lina huo ujazo wa *cubic meter* 62,920, Bwawa la Kasinde pia *cubic meter* 88 umesema vyote hivi vimekamilika. Kwa dhati ya moyo wangu pamoja na Wanamomba tunakushukuru sana ukamilishaji huu unasema tupo kwenye manunuzi. Tunaomba kweli tuone kwenye vitendo, tunaomba kweli tuone kwenye vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazalisha; pamoja wanalima kwa kutumia jembe la mkono utakapotuletea mambo mazuri kama haya siyo tu kwetu sisi Wanamomba, lakini ni faida pia kwa Taifa. Nimwambie ukweli mpunga ambao anaona unaenda mwingi pale *DRC* na Zambia, mimi si nipo hapo maeneo Jirani, unalimwa na hawa wanaolima kwa jembe la mkono hapo Momba. Kwa hiyo, tunaomba hili jambo likamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaona Skimu ya Uwagiliaji Naming'ongo, Mheshimiwa Waziri alikuja pale tukamtembeza akapigwa na picha vizuri na Wanamomba akili yao bado inakukumbuka. Sasa hivi utekelezaji ametupa pesa 41%. Tunamwomba basi kaka atumalizie hii pesa maana yake ndiyo skimu ambayo kwa sasa hivi inategemewa hakuna skimu yoyote ya uwagiliaji kwenye Jimbo la Momba. Hii tu hizi nyingine zote ndiyo tunakusudia tuweze kuzifanya, umeona ni hii tu 41%. Kwa hiyo, sasa hivi ukiona mpunga ambao utakuwa umetoka Momba ni kwenye hii skimu hii hapa. Kwa hiyo, tunaomba tumaliziwe pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa umuhimu wake, Waziri mwenyewe akiendelea kusema anayaunga mkono maneno ya Mheshimiwa Rais kwamba sisi tunataka tujitosheleze ndani, lakini pia tuweze kuilisha Afrika. Mheshimiwa Waziri siyo makosa ya

Mheshimiwa Rais, siyo makosa ya Chama Cha Mapinduzi, siyo makosa ya Waziri, kulikuwa kuna mabadiliko ya tabianchi Tanzania kwingi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya maeneo ambayo yanategemea mazao yenye mvua wamekosa mazao. Mfano kule kwetu Momba hatujapata mpunga kwa sababu hata hii skimu yenyewe si haukutuletea pesa, sasa tungemwagiliaje? Maana yake skimu ni mbovu. Kwa hiyo, tulikuwa tunategemea mvua ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, yale mazao kama mpunga hatujapata. Ninataka kumwambia nini? Ninataka kukumbusha kule 2022 maana yake hatuna mazao ya kutosha ya chakula. Sasa kama jana Waziri ametusomea kwenye hizo taarifa zake kwamba sisi tumekuwa ni wazalishaji wa pili wa mahindi na Mheshimiwa Rais anasema tujitosheleze sisi nchini kwetu na tuweze kuwahudumia Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi tunaomba kuanzia angalau mwezi Julai watu wamalizie kuvuna, atakuwa ameshafanya tathmini, ameshapata. Tunaomba *NFRA* kwa atakavyojua kwa sababu wapo chini yake, waanze kuwauzia wananchi mahindi kwa sababu lengo la kupeleka ruzuku, lengo la kufanya mambo yote hayo, lengo la Wabunge sisi kuendelea kuishauri Serikali kwamba tuongeze bajeti ni kuona kwamba hatupaswi kununua chakula kwa bei ghali kwa sababu tumelima tuweze kujitosheleza sisi wenyewe na sisi tunalo ghala la *NFRA*. Kwa hiyo, tusingependa mahindi yanatoka, yanaeenda Zambia na *DRC* wakati sisi wenyewe tunalolitunza ghala na tumewa-*host* vizuri na kuna wakati *NFRA* wanachelewa kutulipa. Kwa hiyo, wakiwa wanachelewa kutulipa tunatunza mahindi yetu. Tunaomba tuanze kupata mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kuendelea kutukumbuka wakulima na sisi tunaamini watawatendea haki wakulima. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamtaja mchangiaji anayefuata, katika wanafunzi waliokuja kutoka Shule ya FEZA kuna mtoto pia wa Mheshimiwa Khadija Taya, anaitwa Yahya Jamal Juma, yupo wapi? Yupo kule pembeni mmemwona? Hongera sana Mheshimiwa Khadija. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi na Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, ajiandae.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kupata nafasi niweze kuchangia kwenye bajeti hii muhimu sana ambayo inawagusa Watanzania wengi, ambapo Watanzania wengi sana wanajihusisha na kilimo hasa kilimo kile kidogokidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yote ya Wizara kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya kuhakikisha kwamba kilimo cha nchi yetu kinaendelea kuwa mkombozi kwa Watanzania wetu, lakini kilimo hiki kinaendelea kuwakomboa kiuchumi sisi watu ambao tunatoka maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kupongeza kwa bajeti ambayo imeendelea kukua mwaka hadi mwaka. Tunafahamu kwamba tumetoka toka kwenye shilingi bilioni 294 mpaka shilingi trilioni 1.2 mwaka jana na mwaka huu imeendelea hivyo. Hii yote ni juhudi kubwa ambayo inafanywa na Wizara. Pia, tumpongeze mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuwa mkulima namba moja *champion* kuhakikisha kwamba anawajali wakulima, anakijali kilimo na kuhakikisha kwamba Watanzania waendelee kunufaika na kilimo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoenda kupongeza kwa kuongezeka kwa bajeti pia tu ninaendelea kupongeza kwa

mipango mizuri waliyokuwa nayo. Namna ambavyo sisi ambao tunatoka maeneo ya kilimo hasa ambacho tunatoka kwenye kilimo cha tumbaku mipango yao mizuri kwenye Wizara, mipango yao mizuri kuhakikisha kwamba kilimo hiki kinazidi kukua, tumeweza kuona namna ambavyo zao letu la tumbaku limeweza kukua kutoka 2021/2022. Sisi Mkoa wa kitumbaku wa Chunya tulikuwa tunazalisha tani 15,000,000, lakini mwaka huu tunategemea kuzalisha tani 25,000,000 Mkoa wa Kitumbaku wa Chunya. Haya ni mafanikio makubwa sana tunawapongeza kama Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaambie nitapingana kidogo na mama yangu Mheshimiwa Dkt. Thea, kwamba uchumi wa wakulima wa tumbaku umeweza kukua na umeongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Sisi leo wastani wa juu wa zao la tumbaku ni dola 3.4 hii haijawahi kutokea kwa kipindi kirefu sana toka mama Mheshimiwa Dkt. Samia ameweza kuingia. Haya kwetu ni mafanikio makubwa sana. Hivyo, pato la Halmashauri yangu ya Wilaya ya Chunya kupitia zao la tumbaku mwaka uliopita tulipata shilingi bilioni 3.8 ambayo imetokana na ruzuku kutoka zao la tumbaku. Kwa hiyo, sisi kwetu zao hili ni mkombozi kwa wakulima, lakini pia mkombozi kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri haya ambayo yamefanyika kwenye zao la tumbaku lakini bado tunaendelea kuishauri Serikali iweze kuona namna bora na nzuri ya kuhakikisha kwamba zao hili kadri linavyoendelea kukua tuendelee kutunza mazingira. Mazingira yetu mengi tunayolima maeneo ya tumbaku yanaharibiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua wakulima wanakatwa fedha kwa ajili ya kupanda miti, lakini hiyo miti haionekani. kwa hivyo tulishauri Serikali ione namna iliyokuwa nzuri ya kuhakikisha kwamba wakulima wa kwetu wanawekewa utaratibu mzuri ili hii miti isiweze kuharibiwa kwa kiasi kikubwa kama ambavyo inaendelea kutokea sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wakulima wetu hawa kwenye zao la tumbaku pamoja na kutumia nguvu kubwa sana

kulima, lakini changamoto ya majanga ya asili yameendelea kuwaletea hasara sana. Changamoto ya ukame kama mwaka huu ambavyo tumeona, mvua zimekuwa kidogo hivyo wakulima mazao yao yamekuwa machache. Pia kuna wakati mvua zinakuwa nyingi hasa mvua za mawe, majani yale yanaharibika na yakiharibika inakuwa ni hasara kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri kwamba tuone namna ya kusisitiza ile bima ya wakulima tuhakikishe tunaipa nguvu ili wakulima hawa wasiweze kupata hasara kama ambavyo wanapata sasa hivi. Wanafanya kazi kubwa shambani lakini majanga ya asili ikiwemo mvua za mawe pamoja na ukame au mvua inapokuwa imezidi imeendelea kuwarudisha nyuma wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ili tuendelee kutoa elimu kwa wakulima wetu juu ya mabani yaliyokuwa mazuri na kisasa, wakulima wanafanya kazi kubwa sana shambani lakini kazi kubwa ile inakuja kuathiriwa wakati wa ukaushaji wa hii tumbaku kupitia kwenye mabani. Mabani mengi yanayojengwa yanakuwa hayana ubora wa kisasa, siyo makubwa kulingana na uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kazi kubwa iliyofanywa na wanakulima inaelekea kupotea katika hatua ya ukaushaji wa tumbaku. Wakulima wanashindwa kupata kile walichotarajia, kwani mavuno yao hayazai matokeo kama walivyotarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne tuendelee kutoa elimu juu ya kalenda ya upandaji wa zao la tumbaku. Tukifuata kalenda vizuri, wataalam wetu wakiwasisitiza hawa wakulima tutaweza kupata mazao mazuri na wakulima wetu wataona tija ya zao la tumbaku na bei ambayo ipo sasa hivi itaweza kuwanufaisha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunafahamu kwamba Watanzania wengi wanategemea sana kilimo kuendesha maisha yao hasa kule vijijini na kilimo ambacho sasa hivi tunatakiwa twende nacho na kila mmoja akizungumze hapa

ni kilimo biashara. Kilimo biashara ndiyo mkombozi wa mkulima wetu wa Tanzania na soko letu la mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali iwekeze sana kwenye kilimo cha umwagiliaji. Tunajua inafanya kazi kubwa, inaendelea kuchimba mabwawa, inaagiza magari ya kuchimba visima lakini hii kasi iweze kuongezeka. Tukiongeza hii kasi tunaamini kwamba wakulima wetu wataenda kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Wilaya ya Chunya hasa Tarafa ile ya Kipembawe yamegundulika mabonde mazuri yanayofaa kwa kujenga *scheme* za umwagiliaji. Kata ya Kambi Katoto, Kata ya Mafyeko, Kata ya Luwalaje pamoja na Kata ya Rupa maeneo Riyesero. Haya yamegundulika kwamba yanafaa kupitia wataalam wetu wa ndani na wataalam kutoka Wizarani kupitia Tume ya Umwagiliaji. Waliweza kufika Wilaya yetu ya Chunya wakayaahirisha wakayaona na sisi tukaweza kuomba, tumeandika barua kuomba angalau tuweze kupata usanifu wa kina, takribani kama milioni zisizopungua 500 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha tukiweza kuzipata, ukafanyika usanifu wa kina angalau sasa tutaweza tukaanza kuyajenga maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji na sisi Wilaya ya Chunya tukapata skimu za umwagiliaji, hivyo kilimo chetu kitaweza kwenda mbele na wananchi wetu wa Tarafa ya Kipembawe wakanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei yake, kuna *scheme* ya umwagiliaji ambayo ilianza kujengwa muda mrefu sana toka 2012 ambayo inaitwa *scheme* ya Ifumbo. Tulipata zaidi ya bilioni moja, lakini ilijengwa ndani ya mwaka mmoja ikasimama, zile fedha ni kama zimepotea. Hivyo, kwa kuwa Serikali nia na lengo lake ni kuhakikisha kwamba eneo lile ambalo linafaa kwa kilimo cha umwagiliaji liendelee ili lengo lake liweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara, tunafahamu ilikuja lakini iweze kufanya usanifu upya kulingana na mazingira ya sasa hivi, tupate fedha, usanifu wa kina ufanyike, *scheme* ile pale iweze kujengwa ili wananchi wa Kata ya Ifumbo na Wilaya ya

Chunya tuweze kunufaika wakati hii tayari tunakuwa tumeshaanza nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya ambayo tumeweza kuyasema, mtakumbuka wizara ina mpango mzuri sana wa kesho iliyo bora maarufu kama *BBT*. Sisi Wilaya yetu ya Chunya tuna maeneo takribani hekta zisizopungua 600,000 ambayo Waziri alifika, tukayaainisha. Hata hivyo, tulitegemea kwamba angalau sasa hatua za mwanzo zile zilivyokuwa zisingeweza kuanza, pia mpaka sasa mradi huu bado haujaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, wananchi wangu wa Tarafa ya Kipembawe wanategemea yale mashamba pori wakiweza kuyaendeleza tutahakikisha kwamba uchumi wa wananchi wa Chunya kwa maana ya Tarafa ya Kipembawe utakua, ajira zitazalishwa, lakini kama nchi tutakuwa na uhakika wa chakula cha kutosha. Mlibebe hili ili pamoja na mradi unapokuwa unaendelea tuhakikishe kwamba na sisi Wilaya ya Chunya tunapewa kipaumbele pamoja na kwamba zao la tumbaku linaendelea, lakini na haya mazao mengine yaweze kwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi hii. Niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya yeye na wataalam wake, tunaamini kilimo siyo uti wa mgongo, kilimo ni biashara na kilimo ni fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile na Mheshimiwa Anathropia Theonest wajiandae.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami ili niweze kuchangia bajeti hii ya wakulima, bajeti hii ya wananchi. Nianze kwa kuunga mkono

hoja bajeti hii nzuri ambayo inakwenda kugusa maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipokuja Kigoma alisema anakwenda kuufungua Mkoa wa Kigoma, amekwenda kuufungua Mkoa wa Kigoma kwa kupitia kilimo ambapo wananchi sasa wa Jimbo la Muhambwe wanafurahia kufunguliwa kwa jimbo lao kwa kupelekewa mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote ni mashahidi, tumepata mbolea ya ruzuku ambayo imefikia wakulima kwa wakati na kwa urahisi. Hapa niwapongeze mawakala wetu ambao walijiongeza zaidi na kusogeza karibu zaidi huduma hii ya mbolea kwenye vijiji vyetu ili wananchi waweze kupata mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea hii ya ruzuku imeleta tija sana kwa wakulima wetu kwa sababu bei imepungua, lakini wanaipata kwa wakati na kwa urahisi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Bashe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri sana wanazozifanya katika Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tumeshuhudia tangu jana mapka leo tunawapa maua yao kwa kazi nzuri kwa sababu wote tunafahamu wamegusa maisha ya wananchi wengi huko kwenye jamii zetu. Wengi wamesema, wananchi sasa wanapenda kulima, lakini wameiamini Serikali, Wizara ya Kilimo kwa sababu imefanya mambo yanayoonekana. Hongera sana kaka yangu Mheshimiwa Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwenye Hotuba ya Waziri kwamba tunavyo viwanda vya ndani ambavyo vinahudumia nchi yetu, hivi vimerahisisha upatikanaji wa mbolea ikiwemo *Minjingu Phosphate* na *Itracom* hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa mbolea umerahisika kwa sababu ya viwanda hivi, sasa ninadhani ni muda muafaka sasa wa viwanda hivi kupelekewa ruzuku kwa ajili ya mbolea ili

mbolea itoke kule kiwandani ikiwa tayari ina ruzuku. Hii italeta *multiple effect*, kwa nini? Kwanza tutavijengea uwezo viwanda vya ndani kama ilivyo sera kwa nchi yetu kwamba tuwalinde watengenezaji wa ndani.

Mheshimiwa Mweyekiti, tutaongeza pia ajira kwa vijana wetu kwa sababu kama vitazalisha sana, vijana wetu wataajiriwa zaidi, pia viwanda hivi vitaweza kusafirisha mbolea nje ya nchi. Kwa hiyo, tutapata *export levy* kwa sababu, wakizalisha ndani zaidi mahitaji yakitosha watapeleka nchi jirani na nchi itajipatia mapato zaidi. Niombe Serikali ifikirie kuvipatia viwanda hivi ruzuku ili viweze kufanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umwagiliaji; kwanza niishukuru Serikali nimeona kupitia ukurasa wa 144 umeweka mikakati ya kuendelea kujenga miundombinu ya umwagiliaji. Hapa nimpongeze Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji kaka yangu Raymond alifika Jimbo la Muhambwe, alifika katika Skimu za Lumpungu, Nyendara, Kigina, Kumgondogondo na Kahambe. Wananchi wa Muhambwe wanamshukuru sana. Leo nimeona kwenye bajeti imeelezea jinsi gani wanakwenda kufanya ukarabati wa skimu zile za Jimbo la Muhambwe ili wananchi wa Muhambwe nao waweze kufaidika kwa kilimo cha umwagiliaji waweze kulima kwa mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, Serikali ipeleke pesa za kutosha Tume ya Umwagiliaji hizi skimu ziishe pia ambazo zimemalizika kufanyika upembuzi yakinifu ikiwemo za Jimbo la Muhambwe ziweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kipekee Tume ya Umwagiliaji kwa kujenga uzio kwenye Skimu ya Nyendara, kama nilivyoisema hapa Bungeni kuwa ilikuwa inasababisha maafa na mkandarasi sasa yupo *site*, wananchi wa Jimbo la Mhambwe wanaishukuru Serikali sana ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu sasa skimu ile italeta matokeo na haitaleta maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 107 imeongelewa jinsi gani tutakwenda kushirikiana na Serikali katika kuendeleza Skimu ya Lumpungu, wananchi wa Lumpungu wapo tayari, wanaisubiri kwa hamu, wamefurahia uwekezaji huo kwa sababu kipo kipengele ambacho wananchi watapata 20% na wao kuweza kufanya kazi, na tumeshaandaa hati ya pamoja kushirikiana na Serikali ili *scheme* hiyo ifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda muafaka wa kuhakikisha utekeleza hii mipango mizuri ambayo Wizara ya Kilimo imefanya, kwa Wizara ya Fedha kupeleka pesa za kutosha. Bila fedha hatutaweza kufanya haya mambo ambayo yamepangwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuja na mpango mzuri wa kujenga miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo kwa ajili ya wakulima katika halmashauri zetu. Nami nimetajwa pale kwenye ukurasa wa 107, Jimbo la Muhambwe tunalima muhogo na muhogo umeporomoka sana. Kufuatia kilio changu kwa Mheshimiwa Kaka Bashe ninashukuru sasa Serikali imetuona, inakwenda kujenga soko la muhogo, itakuwa *three in one*, tutakausha muhogo, tutauza muhogo, lakini tutaweka na maghala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaandaa eneo katika Kata ya Nyarioba, tulitakiwa hekta 50 lakini sisi tumeandaa 55 na wananchi wametoa eneo lile bila kuhitaji fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaiomba Serikali, soko hili la muhogo lina manufaa sana kwa wananchi wa Kibondo kwa sababu bei ya muhogo imeporomoka sana kutoka shilingi 800 mpaka shilingi 200, mabenki yamewapatia wafanyabiashara pesa lakini hawawezi kulipa kwa sababu soko la muhogo limeporomoka sana. Niiombe Serikali mpango huu ulioweka kwenye bajeti, basi pesa iletwe ili wananchi wa Jimbo la Muhambwe waweze kuuza huu muhogo kwenye masoko yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo imeona umuhimu wa kumkopesha mkulima wa Tanzania. Niyapongeze mabenki yote ambayo yanafanya kazi na wakulima, *CRDB*, *NMB*, *NBC,* lakini kipekee hapa niipongeze Benki ya Maendeleo ya Kilimo kupitia Mkurugenzi wake kaka yetu Frank, anafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunakumbuka mwaka jana 2024 wakati benki inaonekana haitaweza kufanya kazi vizuri, Serikali na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maamuzi ya dhati na ujasiri aliingiza pesa pale ili kuwaongezea mitaji. Benki hii kikubwa ilichofanya nimeona kwenye taarifa imetoa bilioni 137 kwa ajili ya wakulima wadogo. Niiombe Serikali iendelee kuiongezea benki hii pesa, lakini waendelee kushuka kwa mkulima mdogo wa Muhambwe wa Kijijini kule Kigina - Rugogwe ambaye hawezi kufika kwenye mabenki makubwa ili na yeye aweze kunifaika na huu mkopo wa *single digit. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo inafanya vizuri katika mazao mengi, tumeona tumbaku ya pili Afrika, tumeona mahindi, Mheshimiwa Bashe amefanya kazi nzuri na Serikali imefanya vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali, wapo mawakala wachache wanunuzi wa mazao kwa wakulima ambao ni wajanja wajanja na hapa nitamtaja *JESPAN* ni wakala aliyenunua tumbaku katika Jimbo la Muhambwe, *AMCOS* zangu za Jimbo la Muhambwe bado hawajalipa, mauzo ya mwaka 2020/2021. Ninamwomba kaka yangu Mheshimiwa Bashe, *JESPAN* awalipe wakulima hawa ambao wanalima kwa shida sana, wanalima kwa jembe la mkono, lakini wanauza tumbaku halafu mtu hawalipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Bashe wasaidie wakulima wa Jimbo la Muhambwe ambao walilima tumbaku lakini wakala wake *JESPAN* hajaweza kuwalipa. Hapa nimpongeze *DG* wa Mamlaka ya Tumbaku, kwa kweli amenipa ushirikiano sana kuhusiana na deni hili, wamelipwa kidogo lakini

sasa ni muda wa kumaliza hii pesa yote ili hawa wananchi waweze kupata pesa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Muhambwe wapo tayari kupiga kura, wakiangalia yale maghala aliyojenga Mheshimiwa Bashe kule Kagezi, Rubongwe, wananchi wa Muhambwe wapo tayari kwenda kupiga kura. Wananchi wa Muhambwe wapo tayari kupiga kura wakiangalia mbolea ambayo imewasaidia kuweza kupata mazao mengi, ikuvuna kwa kiasi kikubwa. Wanasema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hawana cha kumlipa zaidi ya kumpatia kura za kishindo za kutosha itakapofika mwezi wa kumi, kwa nini? Tulijiandaa kwa muda mrefu ndiyo maana sasa tupo tayari kwenda kupiga kura kumchagua Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Wizara ya Kilimo imefanya mambo mazuri makubwa sana, lakini kama Serikali haitaingiza hizi pesa, kama wenzangu wanavyosema, Azimio la Maputo hatujafikia hiyo 10%, hata hiyo asilimia tunayoipanga haiendi kwa wakati na haiendi kwa ukamilifu. Malengo haya mazuri ya Waziri Bashe, malengo haya mazuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hatutaweza kuyafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu ambao wamesisitiza kwamba tunaiomba Serikali ipeleke pesa za kutosha kwenye Wizara ya Kilimo ili wananchi wetu waweze kufaidika ili Skimu za Muhambwe ziweze kujengwa, soko la muhogo liweze kujengwa, mikopo kwa wananchi iweze kupelekwa na wananchi waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo niliyoyachangia, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja bajeti hii ya wakulima, ya Watanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi. Nilimtaja Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile,

Mheshimiwa Anathropia Theonest na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, ajiandae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Pia ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai, lakini niungane na Wabunge wenzangu kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba Mheshimiwa Rais ameonyesha kwa vitendo namna ambavyo anakwenda kufufua matumaini ya wakulima kote nchini. Tukiona tu hiyo bajeti ya mwaka 2021 na hii bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025, tunaona dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais kwenda kuinua kilimo cha Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili mwenye ubishi bila shaka ana matatizo na hapa hospitali ya afya ya akili ipo karibu Milembe, hawa watu tuwasaidie ili waone nia njema ya Mheshimiwa Rais namna Serikali ya Awamu ya Sita ilivyofanya kazi kuinua kilimo cha nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Hussein Bashe na Naibu wake Mheshimiwa Silinde, Katibu Mkuu na Watendaji wote. Wabunge wenzangu wametoa sifa nyingi kwa Mheshimiwa Waziri na Timu yake, lakini ipo sifa ya ziada nitaisema. Mheshimiwa Waziri huyu ni mcha Mungu lakini pia ni mkweli, zaidi ya hayo Waziri huyu hata ukimpigia simu hata saa nane ya usiku anapokea na tabia hiyo amekwenda kuiambukiza kwa Naibu wake, lakini kwa Katibu Mkuu na Watendaji wote. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri, tunaona kazi yake kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze kwenye mchango wangu kwenye maeneo kadhaa. La kwanza kwenye *scheme* ya umwagiliaji na hapa Mheshimiwa Waziri ninaomba kwa unyenyekevu mkubwa kabisa. Kwenye maswali yangu nilikuwa nimetoa maswali yanayohusu juu ya *scheme* hii ya umwagiliaji kwenye maeneo kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu yapo maeneo ambayo yana mabonde oevu, yapo mazuri kwa ajili ya kilimo hiki cha umwagiliaji. Na kwa kutambua maeneo haya ninaomba niyataje kwa ruhusa yako, yapo maeneo ya Namanga, Ruponda, Marambo, Chihola, Rupota, Mbondo na Matekwe. Haya maeneo ni mazuri na yana mabonde mazuri yaliyo oevu na kwenye majibu ya maswali niliyokuwa nayauliza walikuwa wanasema bado wanaendelea na utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri maeneo haya tukienda kuweka hizi *scheme* za umwagiliaji ni zaidi tunakwenda kupandisha sasa morali ya wakulima wetu na wataendelea kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Nachingwea lina Kata 36 na hapa nishukuru kata zote zinao Maafisa Ugani, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina vijiji 127 kwenye eneo hili, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, tunao Maafisa Ugani kwenye maeneo haya 16, maana yake tunao upungufu wa Maafisa Ugani 111 na kwa sababu tunaona nia ya dhati ya Serikali kuinua kilimo ni wazi sasa Maafisa Ugani wanahitajika zaidi. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anapata nafasi ya kuajiri hawa Maafisa Ugani, tukumbuke kule Nachingwea ili kazi iweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo, niipongeze Idara ya Kilimo Nachingwea inafanya kazi nzuri sana, hawa Maafisa Ugani kwa ngazi zote wamepata vyombo vya usafiri, lakini hapa nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, Afisa Kilimo Wilaya, hana usafiri, ili aweze kusimamia vizuri kilimo ni lazima awe na usafiri wa kufaa unaokidhi haja kuwafikia watendaji wetu kule ngazi ya kata na vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Afisa Kilimo wetu Wilaya ya Nachingwea anaitwa Rafael Yusuph Ajetu anafanya kazi nzuri sana, anachapa kazi kweli na ndiyo maana kilimo Nachingwea kinaendelea kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linguine, nimesikia Wabunge wenzangu hapa wanashukuru kwa sababu ya matrekta. Hapa nitazungumza kwa unyenyekevu mkubwa sana. Kule kwetu sisi asilimia ya wananchi wengi wanatumia kilimo cha jembe la mkono. Matrekta haya tafadhali na sisi tunayahitaji, kwa kufanya hivi kilimo tutaendelea kukiinua zaidi, maeneo hayo kwa sasa wananchi wamehamasika sana juu ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka iliyopita kilimo ilikuwa inaonekana ni kazi ya hovyo na ni kazi ambayo wanakwenda kuifanya watu ambao wameshindwa maisha, lakini sasa kilimo hata wananchi wetu wameshagundua sasa kwamba kilimo ndiyo uchumi, kwa hiyo kwa kutuletea haya matrekta, sisi tunakwenda kuimarisha kilimo chetu, siyo tu Nachingwea hata Lindi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri wakati anakuja kuhitimisha hapa, ni vizuri aseme neno kuhusu gari ya hisa kilimo kule Wilaya ya Nachingwea na matrekta haya kwenye maeneo haya tutapata lini ili basi kule kazi iendelee na wenzetu waendelee kujipanga kwamba kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu jana hapa wako Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia juu ya ufufuaji wa zao la soya na karanga kule Nachingwea. Mheshimiwa Waziri, zao hili ndiyo lilikuwa maarufu enzi za wakoloni na tulipata reli pale ambayo ilikuwa inatoa karanga na soya kutoka Nachingwea kwenda Bandari ya Mtwara. Kwa sababu ambazo kwa kweli siwezi kuzijadili sasa ile reli iliondolewa, lakini pia na lile zao lilikufa. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwenye mipango ya Wizara kufufua mazao ya kimkakati twende tujielekeze kwenye zao hili la soya na karanga kwenye Jimbo langu la Nachingwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hata leo hapa Mheshimiwa dada yangu Dkt. Thea Ntara amelizungumzia pia, Mheshimiwa mama yangu pale jana, Mheshimiwa Lulida

alilizungumzia. Kwa hiyo, ni jambo la muhimu, wakituletea hiyo basi tutaendelea kuongeza mazao ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Tawi la Kituo cha Utafiti Naliendele, kiko pale Nachingwea na hili ninalizungumza kwa unyenyekevu mkubwa, Mheshimiwa Waziri kile kituo kimechakaa. Kile kituo matrekta yote ni mabovu, wakati tunaendelea kuimarisha kilimo, twende tukifufue na kile kituo cha utafiti ili kiweze kufanya kazi kikiwa na zana za kisasa. Ninajua hilo Waziri analiweza, basi anaweza akasema neno hapa ili wataalam wangu kule waendelee kujua kwamba mambo yanakuja na kazi itaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anakuja ku-*present* hapa Mfumo wa Ununuzi wa Korosho *(TMX)* hatukumwelewa sana, lakini sasa tunamwelewa sana, tunamwelewa sana. Tunamwelewa sana Mheshimiwa Rais na nia yake njema na kwenye hili sisi kule Nachingwea, wananchi wangu wakati nawatembelea nakwenda kuwaambia nikaseme nini Dodoma? Waliniambia Mheshimiwa Mbunge ukipata nafasi mwambie Mheshimiwa Rais, wakati ukifika huku hana sababu ya kuja, sisi tumeshakubaliana, kura zote kwa Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo hata Liwale sauti ndiyo hiyo. Siyo tu Nachingwea na Liwale hata maeneo mengine ya Mkoa wa Lindi tumekubaliana kwamba, Mama Samia hata kama asije kuomba kura, sisi tumekubaliana kwa namna ambavyo ametufanyia mema kwenye Mkoa wetu wa Lindi, kule kazi inaendelea na sisi tutampa mitano tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ni vizuri nitambue kazi kubwa inayofanywa na Mkuu wangu wa Mkoa, Mama Zainab Telack, anafanya kazi kubwa sana ya kusimamia shughuli zinazoendelea ikiwemo kilimo, pia na Mkuu wangu wa Wilaya, Mheshimiwa Mohamed Moyo, naye anafanya kazi. Mkurugenzi wangu, *Engineer* Chionda Kawawa, wanafanya kazi ya kusimamia na kuona kwamba mambo yanakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niendelee kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amandus Chinguile. Nilimtaja Mheshimiwa Anatropia Theonest. Mheshimiwa Miraji Mtaturu na Mheshimiwa *Engineer* Dkt. Leonard Chamuriho, wajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Nisiwe asiyekuwa na fadhila, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa Ujenzi wa Masoko ya Kimkakati ya Kyerwa, Mlongo, lakini pia Mheshimiwa Esther Matiko ameomba pia niongelee Soko lake la Remagwa. Siyo kwamba yamekamilika, hapana hayajakamilika, lakini kuna ujenzi unaendelea. Kwa hiyo, ninaomba ni-*reserve* pia hizi shukrani mpaka yale masoko yakikamilika yakaanza kutumika. Hizo shukrani nitazileta rasmi kwa niaba ya wananchi wa Kyerwa na Tarime kama alivyoniongezea Mheshimiwa Esther. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika sana kwamba Bajeti ya Kilimo imekuwa haitoki yote. Tunakuja hapa tunafurahia sana, tunasherekea sana, tunachekelea sana, lakini fedha haziendi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukawaza mtu afanye maajabu, atafanya maajabu gani kama fedha haijaenda kwa wakati? Kwa hiyo, nitoe wito na niongeze kupaza sauti. Ninaomba turudi kwenye *commitment* yetu za Malabo *Protocol,* kwamba 10% ya bajeti itengwe kwa ajili ya kilimo na siyo kutengwa tu, itengwe na ipelekwe kwa ajili ya kilimo. Hivi vilio vyote mnavyovisikia Waheshimiwa Wabunge wanavitoa hapa vya kuhusu wakulima wetu kutumia jembe la mkono, linaweza kufikia mwisho. Hakuna fahari ya mtu kutumia jembe la mkono, hakuna utajiri kwenye kutumia jembe la mkono. Sisi tumelelewa tumekua wazazi wetu wanatumia majembe ya mkono mpaka leo bado ni maskini lakini ni watu ambao wanafanya kazi kwa bidii, wanajituma sana, lakini utaongeza tija gani kama ni jembe moja moja yaani unahesabu jembe moja moja, kwa hiyo, kwa siku kama ni jembe 1,000 imeishia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama tunataka tulete mabadiliko kwa 61%, Waziri ameeleza 61% ya Watanzania wameajiriwa kwenye kilimo, kama tunataka ku-*empower the 61%* ambao ni *majority* ni lazima tuboreshe kilimo kwa ku-*mechanised agriculture*. Ni lazima tuweke fedha za kutosha kwa ajili ya ku-*boost* uchumi wao. Vinginevyo itakuwa ni *mark time* tu na ndiyo maana tunaona mabadiliko hayaonekani kwa sababu ya wakulima wetu wengi bado ni maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mtu wa Kyerwa nikisimama hapa cha kuongelea ni kahawa tu. Kahawa kwetu ni uchumi, kahawa kwetu ni maisha, kahawa ndiyo kila kitu. Nilikuja Bungeni hapa ninakumbuka kipindi fulani Mheshimiwa Hasunga akiwa Waziri, nikaeleza umuhimu wa kutumia minada katika kununua kahawa. Nilitoa mifano niki-*cite* hata mikoa kadha wa kadha ambayo ununuzi au uuzaji wa kahawa ni minada. Wengi sana walipinga bila kuelewa nilikuwa nasema nini. Ninashukuru sana Mheshimiwa Bashe na Serikali iliyokuwepo ilielewa mantiki ya kwa nini tunapaswa kutumia minada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyotumia ushindani wa kiminada *at least* kuna unafuu wa bei tumeuona. Walienda mbali zaidi waliokuwa kwenye vyama vya ushirika, waliowahi kukutana na mimi wananitambia kwamba Anatropia kushinda uchaguzi hutatoboa kwa sababu tu nilisema ninataka minada na *KBC* waunde kampuni na wao washindane na wanunuzi wengine na hiki ndiyo kinafanyika na wakulima wetu wanafurahi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui hofu yao ilikuwa ni nini kama leo kwenye soko ni *win win situation*. Ninaomba nimwambie kitu kingine Mheshimiwa Waziri, pengine anakijua au hakijui. Kahawa zinazopita kwenye minada pengine ni robo kuliko nyingine zote ambazo haziingii kwenye minada, sijajua ni kwa kiwango gani atasaidia kudhibiti hiyo, lakini namna pekee ya kuwasaidia watu wa Kyerwa na mikoa inayozalisha kahawa kama Kagera na maeneo mengine ni kuhakikisha kila kahawa inayozalishwa inapita kwenye mnada na wanaonunua kwenye minada wanalipa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu shida tuliyonayo, wananchi wanaanza kuwaza kwamba tukwepeshe kahawa ili tuweze kupata hela kwa haraka, kitu ambacho kinawadidimiza. Mheshimiwa Waziri, tafadhali tusitengeneze na tusikubaliane na ma-*cartels* ambao wanahakikisha kwamba watu hawauzi kahawa zao kwenye mnada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali watazijuaje hizi tani? Leo Waziri anaeleza kwamba uzalishaji wa kahawa umepanda kutoka tani 58,000 mpaka 81,000, atajuaje kama hazipiti kwenye minada? Kwa hiyo ili tuweze kupata *correct record,* ili tuweze kupata *the right revenue* ili hata halmashauri zetu zikusanye *cess* ni lazima tu tupambane kahawa zetu zote zipite kwenye mnada, *full stop*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kabla sijaenda mbali zaidi, leo ninavyoongelea Kyerwa kuna wizi mkubwa wa kahawa. Watu wanavuna kahawa mbichi wasiokuwa waaminifu wanavuna kahawa mbichi, wanavuna mashambani usiku kucha wanawaibia wakulima maskini ya Mungu. Mtu amejiandaa zaidi ya miezi nane anasubiri kahawa, kahawa hazijaiva zimeshavunwa na watu wasiokuwa waaminifu. Unadhani wanauza wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu hana hata mti mmoja wa kahawa, hana shamba, hana mche, lakini anaenda kuuza kahawa, ni kwa nini tusiamini kwamba wafanyabiashara wanawashawishi watu wasiokuwa waaminifu kuvuna kahawa? Nninachotaka kusema hapa, ni lazima kila kahawa inayonunuliwa iwe na *source*. Wewe kama ni mkulima umeleta kahawa utuambie umezivuna wapi, hiyo ndiyo namna pekee ya kuzuia wizi unaoendelea leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninavyoongea, baba yangu wa zaidi ya miaka 80 amelazimika kutafuta watu wa kulinda kahawa zake na kama hawezi ku-*afford* kulinda kahawa anapaswa kujikongoja na yeye akalinde kahawa. *Do you think that is fair?* Siyo sawa. Ni lazima utaratibu utengenezwe, tuwe na *source,* umevuna wapi kahawa unazotaka kuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la kwanza lakini jambo la pili, tumekuwa kwa muda mrefu na habari ya butura. Ni kwa nini mnadhani watu wanauza butura? Ni kwa sababu hawana fedha ya kujikimu kipindi chote wanasubiri kahawa ziive. Leo Mheshimiwa Waziri nikuongezee sifa, tumezindua Benki ya Ushirika. Kazi ya Benki ya Ushirika iwe ni benki ya washirika kweli ya wananchi, waweze kunufaika na benki yao kwa maana waweze kukopa, tulegeze masharti. Wasi-*behave* kama *commercial banks* ambao wao kuweza kukopesha mkulima ni *story* nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki tuliyonayo leo ya ushirika iweze kukopesha wakulima wadogo wadogo kwa dhamana hata ya miti yao ya kahawa, kwa sababu wanajulikana. Wafungue *bank account*, mashamba yanajulikana, hiyo ndiyo namna pekee ya kuzuia wao kuuza kahawa kabla ya wakati, lakini ndiyo suluhisho la wao kula butura. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, hii benki iwepo kwa ajili yao, isiwe tu ni *cosmetic* kama benki zilivyo nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kwa kiwango gani tumeweza ku-*tap potential* ya kahawa? Nikiwa ninazunguka nimepata fursa ya kuzunguka maeneo mengi duniani, na nina-*feel* kwamba sisi watu wa Kyerwa tunawezaje kuendelea kuwa maskini tumezungukwa na rasilimali kubwa kama kahawa. Hivi ni kweli sisi kahawa yetu kitu pekee kinachofanya ni kuweza kunywa na kula? Nika-*google* lakini pia nimeona kuna matumizi mbalimbali ya kahawa duniani na huko jimboni nimekuwa nikiwaambia ninasema, leo ninyi ni maskini lakini mmelalia uchumi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaona kahawa inafanya vitu kadha wa kadha ukiachana na kunywa. Kahawa bado inaweza kutengeneza kiungo, kahawa bado ni mbolea, kahawa inaweza kutengeneza keki, kahawa inaweza kufanya vitu kama *cosmetics*. Ninyi wote tunajua kuna *scrub* ambazo leo kwenye mtandao *google scrub* ya kahawa, ni moja kati ya *scrub very expensive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, Waheshimiwa Wabunge, ambao wamefanikiwa kusafiri na Ethiopian Airways,

kuna kinywaji ambacho ni kizuri sana, kinaitwa *Bottega*, kiko kwenye ladha tofauti tofauti, hizo ni *products* zimetengenezwa na kahawa. Wao pia wana Amarula, *they have their own brand* wanaita Amarula *Coffee Drink*. Siyo hizo tu, ziko nyingi tu nitamtumia Waziri aone. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunawezaje ku-*add value* kwenye kahawa yetu? Tukaondoa, sisi kama wakulima wa mikoa ya kahawa tunachokiwaza ni kahawa zikiwa tayari, sisi tunakula, tunakausha tunakula kidogo, lakini baadaye tunawaza ku-*export*. Ni kwa kiwango gani tunaweza kuji-*squeeze* tuka-*attract* wawekezaji waka-*add value* kwenye kahawa, tukaondoka leo kuwa *market driven*, tukawa watu ambao tunaweza ku-*add value* na tukafaidika na kahawa yetu? Hayo ndiyo nilitaka niyaeleze *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, Kyerwa bado ina *potential* kubwa sana. Zao letu haliwezi kuwa kahawa tu. Wabunge wote wanajua Mkoa wa Kagera ni ndizi, lakini ni kwa kiwango gani tumefaidika na ndizi? Niliwahi kueleza hapa Bungeni kwamba nilifanikiwa kwenda nchi fulani Ulaya, nimekuta kuna ndizi ziko *imported* kutoka nchi jirani ya kwetu sisi. Sasa sisi ni kwa kiwango gani tunaweza tuka-*capitalize* katika hizi ndizi tunazozilima na *mind you,* sisi hatulimi kwa tija, ukienda kwenye shamba letu huko Kagera, hatulimi tena kwa tija. Migomba kwanza haina kiwango kizuri kwa sababu tulikuwa na changamoto ya mnyauko kama ilivyo kahawa, mazao yamekuwa ni kama ni kilimo cha zamani. Tunahitaji kilimo cha kisasa cha migomba ili tuweze ku-*add* tija na ku-*export*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, zao la *vanila*. Sisi eneo letu au Mkoa wetu una-*attract vanila*. Ninadhani Mheshimiwa Waziri unajua kesi ya *vanila*. Wakulima walishawishika kulima vanila, wakapambana kupata masoko. Waziri alieleza kwamba amefungua kiwanda, sijui kwa kiwango gani ameweza kuwasaidia ili waweze kuuza hayo mazao yao, lakini bado sisi eneo letu linaweza kuzalisha alizeti. Kwa hiyo, hayo ninaweza kueleza kwamba bado tuna *potential* ya kusaidia Mkoa wa Kagera. Bado tuna *potential* ya kuwafikia wakulima wetu ili

waweze kunufaika na zao la kahawa, lakini na *advantage* ya eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, hizi kahawa zimekuwa zikiwanyanyasa wananchi. Ninarudia, nimemwambia mara nyingi sana Mheshimiwa Bashe kwamba, ikifika msimu wa kahawa pamoja na wao kuwa na wizi wizi mdogo mdogo, kumekuwa pia na kunyanyasa wananchi kwa sababu eti wanavusha kahawa kwenda Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, kama bei yetu ni nzuri kama ilivyokuwa 5,000, 6,000, 7,000, anavusha Uganda ili iweje? Soko letu likiwa zuri, wakulima wetu wakalipwa kwa wakati, hakuna atakeyevusha kahawa, lakini hivi vyote vikikosa, utegemee kwamba watu *by nature* watatafuta faida, tutayaona hayo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, kumradhi. Nimeona Waziri ameandika kwenye kishikwambi kwamba "tutajenga Kituo cha Umahiri wa Maendeleo ya Kahawa Jijini Dodoma" inaitwa *The Coffee Centre of Excellence*. Hivi *what, where, when* Dodoma na kahawa wapi na wapi? Ninaomba m-*cancel* hiyo mipango yenu hii *centre of excellence* siyo lazima iletwe Kyerwa au kokote Kagera lakini ipelekwe kwenye mikoa ambayo ina-*reflect* uchumi unaotokea kwenye hilo eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anatropia Theonest. Nilimtaja Mheshimiwa Miraji. Mheshimiwa *Engineer* Dkt. Leonard Chamuriho, Mheshimiwa Bahati Ndingo na Mheshimiwa Subira Mgalu, wajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii muhimu, bajeti ya wananchi na bajeti ya wakulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na takwimu zilizopo ni kwamba, kilimo kinaajiri Watanzania wengi kuliko biashara au shughuli yoyote. Zaidi ya 75% ya Watanzania wanafanya kilimo, hata mtu akiwa mtumishi na yeye anafanya kilimo, kwa sababu kilimo ni sehemu ya majukumu ya kawaida. Kwa hiyo maana yake tukikiboresha kilimo basi tutakuwa tumegusa watu wengi zaidi. Ndiyo maana leo Serikali imeangalia kilimo katika umuhimu wake, imeweza kupandisha bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 294 mpaka shilingi trilioni moja na milioni mia mbili arobaini na mbili kama ambavyo tumesomewa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kama ambavyo wamesema wengine kwamba, Azimio la Maputo lilizielekeza nchi zilizopo kwenye ukanda huu kuhakikisha kwamba 10% ya bajeti yake inakuwa ni bajeti ya kilimo kwa sababu, kilimo ndiyo kinazalisha malighafi za viwanda, kilimo ndiyo kinachozalisha chakula kwa maana ya usalama wa chakula, lakini kilimo ndiyo kinachosababisha hata viwanda vifanye kazi. Kwa hiyo maana yake, kilimo kikizingatiwa kinaweza kuchochea shughuli za uchumi kwenye sekta zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo baada ya maneno haya ya mwanzo, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ambayo ameionesha wazi kwa utekelezaji mbalimbali wa bajeti na mipango ya Serikali kwenye sehemu ya kilimo. Amefanya kazi hii kubwa sana ambayo leo tunaona imepandisha na kuleta hata ruzuku ya mbegu, ruzuku ya mbolea, imeongeza hekta za umwagiliaji, lakini na afya ya udongo ambayo huko nyuma tulikuwa tunapigia kelele kama Bunge. Leo tumeanza kuona hata vifaa vya kuangalia afya ya udongo pia tumeongeza Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani hawa wamewezeshwa hata usafiri katika maeneo yetu. Kwenye hili eneo ninaomba tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya utekelezaji wa shughuli za kilimo. Zaidi nimpongeze sana Ndugu yangu Mohamed Hussein Bashe kwa namna ambavyo ameisimamia sekta hii. Kwa kweli tunamwona ana *passion* ya kilimo, anafanya kazi nzuri, wakulima wa nchi hii wana imani na

yeye na kwa hakika kile anachosema ndiyo anachotembea nacho. Amekuja mwaka huu ametupa tathmini na tunaona mwenendo mzuri wa kilimo. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na wenzake kwa maana ya Naibu Waziri Mheshimiwa Silinde, Katibu Mkuu Ndugu Mweli na wataalam wote walioko kwenye eneo hili, wanafanya kazi nzuri na Mungu aendelee kuwabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maeneo haya, ninapongeza kwa upande wa Ikungi. Ikungi, nilisimama mwaka wa fedha 2022/2023 nikasema kwamba, miongoni mwa maeneo ambayo hatujafanya vizuri ni kutuwekea hata ruzuku ya kilimo katika eneo la zao la alizeti. Tukasema kama tunavyoweza kupata ruzuku kwenye pamba, kama tunaweza tukapata ruzuku kwenye korosho, kwa nini isiwe alizeti ambalo ni zao muhimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahi kusema kwamba mwaka huu tunaoenda kuumaliza tumeweza kupata ruzuku ya mbegu ya alizeti tani 57.8, jambo hili ni kubwa ambalo sisi watu wa Ikungi tunashukuru sana. Kama haitoshi tumepata tani 710 ya mbolea ambayo imeenda kusaidia kuongeza uwezo wa uzalishaji wa mazao mbalimbali, tumeweza kupata hata mbegu ya mahindi ambayo huko nyuma ilikuwa haipo, tumepata tani 571 na hii jumla yake ilikuwa gharama ya shilingi trilioni mbili, bilioni mia nne thelathini na nane, mia tano sitini na nane. Katika hili Serikali imetuletea ruzuku ya shilingi trilioni moja, bilioni mia saba kumi na saba, sawa na 70%, Serikali imetuwekea fedha hii, tuseme nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa kutuwezesha kutuletea ruzuku hii ambayo leo imewawezesha wakulima zaidi ya 63,000 ambao wameweza kufanya kazi hii nzuri. Kwa hiyo, ninaomba nihakikishe kwamba, itatusaidia kuongeza sana uzalishaji. Kwenye eneo hili la alizeti, ninaiomba sana Serikali iongeze uwezo wa mbegu ili uweze kusaidia wakulima kuzalisha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; niweze kuchangia kwenye suala la mbolea. Tumekuwa na uwekezaji, wawekezaji

wamevutiwa sana, Mheshimiwa Rais amewavutia wawekezaji na wamewekeza kwenye Sekta ya Mbolea. Tuna kiwanda ambacho kipo hapa Dodoma, ambacho kimeweza kufanya kazi nzuri ya uzalishaji. Kiwanda hiki cha *ITRACOM* ambacho kinazalisha mbolea hizi za *FOMI*, ambazo ni mbolea nzuri na ni mbolea tofauti na mbolea nyingine ambapo inaweza kukuza mazao, lakini pia inaweza kuboresha afya ya udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana wenzetu hawa waliowekeza waweze kulipwa fedha ya ruzuku, ili waweze kutoa mbolea kwa wingi na walipwe fedha ambazo wanadai Serikali ili wawe na *muscles* ya kuendelea ku-*supply* mbolea. Tukiwezesha vizuri eneo hili, tutasadia kuongeza tija ya kilimo na tutaongeza mazao mengi na zaidi, tutaenda kuwasaidia ajira Watanzania hawa. Hapa Dodoma kiwanda kipo kinazalisha ajira nyingi, tunaomba wawajali, wawaonyeshe na waweze kuwavutia wawekezaji wengine waje wawekeze katika sekta mbalimbali ambazo Mheshimiwa Rais ameendelea kuwavutia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi niombe sana maeneo mawili: eneo la kwanza ni suala la umwagiliaji. Minara ya skimu yangu Mheshimiwa Bashe anaijua ya pale Mang'onyi. Ninajua Naibu Waziri naye pia anajua, lakini amenielekeza kwa wataalam kazi nzuri inafanyika. Niombe sana zile fedha zitoke, Mkandarasi apatikane ili ile Skimu ya Umwagiliaji ya Mang'onyi iweze kuanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana mabwawa pia yaweze kuchimbwa maeneo ya Lighwa pale Msule kwa maana ya Misughaa pamoja na hapa Choda eneo ambalo lina ardhi nzuri sana, ili wakulima wawe na mazao mbadala kwa ajili ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo mwaka huu kumekuwa na tatizo la hali ya hewa, tabianchi imebadilika na mvua hazikuwa nzuri. Niombe sana mazao yatashuka, hivyo kazi nzuri iliyofanyika na *NFRA* mwaka juzi, ndugu yangu Komba yuko pale ninaomba na mwaka huu watuangalie katika hifadhi waweze

kutuletea chakula kupunguza makali wakati tunaenda kujiandaa kwa ajili ya uvunaji upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ili tukafanye kazi ya wakulima wa nchi hii ambayo Mheshimiwa Rais amewajali sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Dkt. Leonard Chamuriho, Mheshimiwa Bahati Ndingo, Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla wajiandae.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu nichangie hoja hii ya bajeti hii muhimu, Bajeti ya Kilimo. Kwanza ningependa kutoa pongezi kwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutuongoza vizuri kwa falsafa zake za *4R* na vilevile, kwa kuhakikisha kwamba Wizara hii muhimu inapata bajeti ambayo inaashiria umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia bajeti hii ilivyopanda kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ilikuwa ni shilingi bilioni 294 hadi leo ambapo tunaongelea bajeti hii inayoombwa ya mwaka wa fedha 2025/2026 ya shilingi trilioni 1.24. Hiki ni kiashirio kizuri cha lengo thabiti cha bajeti hii inalenga nini katika kumkomboa Mtanzania. Kwa kazi hii nzuri ya Rais, zawadi nzuri ambayo tunaweza kumpatia ni katika muda muafaka mwezi Oktoba, tuhakikishe kwamba anapata mitano mingine tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kutoa pongezi kwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe, ambaye anafanya kazi nzuri ya kuiongoza hii Wizara na vilevile, kwa kuisimamia vizuri Wizara hii ambayo ni muhimu inayohitaji usimamizi mkubwa pamoja na kwa kutuletea bajeti ambayo ina matumaini kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kutoa pongezi kwa wasaidizi wa Waziri nikianza na Naibu Waziri wake Mheshimiwa David Silinde; Katibu Mkuu Gerald Mweli; na Naibu Makatibu Wakuu Dkt. Hussein Omar na Dkt. Stephen Nindi, ambapo inaonyesha wanatoa usaidizi mzuri kwa Waziri huyu ambaye ametuletea bajeti yenye kutia moyo. Ikiwezekana timu hii Mheshimiwa Waziri uitunze sana, kwani inaelekea inakusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa Mradi wa *BBT*. Mchango wangu karibu wote utajikita hapohapo kwenye huu Mradi wa *BBT* ambao kwangu mimi ninaona ni mpango mzuri sana, ambao umeazimia kutukomboa katika Sekta hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mradi huu umelenga katika kuongeza ajira kwa vijana na wanawake ambao wanaweza kuitumia ardhi yetu ambayo tunayo tele nchi hii, lakini vilevile, tuna wateja wa kutosha wa mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi hii. Tunampongeza kwa kugeuza kilimo, kwa ile dhana ya "Kilimo, Biashara". Kilimo kiwe ni biashara na biashara hii iweze kumfaidisha kila mtu kwa mafao yake kwamba siyo chakula tu, bali vilevile twende kukifanya kuwa ni biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuuelezea huu mpango wa *BBT* kwamba, jinsi ulivyo na ulivyo mkubwa, tutarajie matunda yake yaonekane kwa hatua. Yaani hayawezi kuwa matunda ya ghafla, kwani ni mpango mkubwa sana. Ningependa kuuita kama gogo twende taratibu kwamba: "Bandubandu Humaliza Gogo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuigawanya katika vipengele mbalimbali. Nilivyopitia randama yake pamoja na hotuba yake nimeona kuna *BBT* Ugani, ambayo imejigawa katika mambo fulani; kuna *BBT* Mitaji, ambayo imejikita katika kutoa uwezeshaji wa kifedha kwa hawa wahusika; ina *BBT* Miche, ambayo imetoa miche kwa ajili ya Wakulima hao; lakini kuna *BBT* Visima, ambayo imejikita katika miundombinu ya kusaidia umwagiliaji katika mpango huo; kuna

*BBT* Mashamba, ambayo imetoa mwelekeo mzuri katika upatikanaji wa ardhi ya hawa walimaji; lakini kuna *BBT* ya ngazi ya Halmashauri, ambayo inausogeza karibu zaidi mradi huu kwa wahusika wenyewe. Kwa hiyo ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa huo mpango wake wa "Bandubandu Humaliza Gogo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumshauri Mheshimiwa Waziri kitu kimoja kwamba, katika makundi haya ambayo amelenga ya vijana na wanawake, kuna kundi moja kubwa ambalo lipo linaweza likakusaidia sana katika kuboresha mradi huu. Hili ni kundi ambalo nitaliita ni kundi la walio tayari. Hili kundi la walio tayari ambao wengi wao ni *middle class* (watu wenye kipato cha kati) lipo, lakini lenyewe ukiliwekea mpango mahususi litaweza kusaidia sana katika mradi huu bila kumwongezea gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwa mfano katika ukurasa wa 80 na 81 wa randama ya Waziri. Ukurasa wa 80 umeongelea kuwezesha zana za kilimo, 81 umeongelea kuwezesha upatikanaji wa ardhi; lakini hawa walio tayari, tayari wana ardhi na wengine wao tayari wana mitaji. Kwa hiyo utajikuta sasa kwamba, kinachohitajika ni kuwasaidia vitu fulani fulani tu. Kwanza Waziri awasaidie miundombinu, ambapo awapelekee kule barabara na visima kwa ambao watakuwa tayari; lakini vilevile awapatie miche na ugani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba hawa, Waziri awawekee mfumo ambao utawawekea vivutio. Kwa mfano, anaweza kusema kwamba kama una ardhi tayari na una kitu hiki na mmejikusanya mpo 10 kwenye mashamba ya ukubwa huu, *then* nitawaletea barabara au mtakuwa *eligible* kupata visima. Kwa hiyo watajikuta kwa hawa watu ambao wana ardhi, wana mitaji yao, basi yeye awamsaidie kuwaongezea kama visima ili kumwagilia vizuri, awasaidie waweze kupata barabara ili waweze kufika katika ule mradi wao kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kulenga mradi mmoja wa *BBT* ambao Mheshimiwa Bashe akiulenga nao utatusaidia sana. Katika mpango wake nimeona kuna *BBT* Tanga,

(Korogwe au wapi) kuna *BBT* ambayo ameilenga kuwa ya mkonge ambayo iko Tanga. Ninapendekeza angekuwa ana *BBT* nyingine pale Butiama ingemsaidia katika ule mradi wa umwagiliaji Butiama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mradi ni mradi dada wa mradi wa Bugwema ambao ulikuwepo. Ninaufahamu vizuri kwa sababu nilianzia kazi pale ambapo tayari bwawa la kumwagilia lipo, shamba lipo na pale jirani kuna Chuo cha *Mwalimu Julius Nyerere University of Agriculture and Technology*. Kwa hiyo akiunganisha ile elimu ya pale ya kilimo na *BBT* pale shamba la umwagiliaji ninadhani atapata matokeo mazuri zaidi na kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona umeniwashia taa. Ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chamuriho, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Bahati Ndingo, Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla wajiandae.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa. Nami nianze kwa pongezi na kwa hakika wakati ninaingia humu ndani na leo ni siku yangu ya kuchangia nimepokea simu nyingi sana kutoka kwa Wanambarali hususani wakulima wa Mbarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamenituma nifikishe salamu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mapinduzi makubwa ya kilimo ndani ya ya Wilaya yetu ya Mbarali hayapigiwi mfano. Pia, wamenihakikishia kwamba, siku Mheshimiwa Rais atakapopita Mbarali tumemwandalia mpunga wa kutosha na ng'ombe wa kutosha kama shukrani kwa kazi kubwa aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haijaishia hapo. Wanambarali tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri kaka yangu Hussein Bashe na timu yako yote. Kaka yangu yeye ni mtu na nusu na ana utu, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanambarali wameniambia tutamtafutia kiwanja kaka Bashe Mbarali, ili ajenge pale Mbarali awe mkazi wa Mbarali. Hiyo yote ni shukrani kwa kazi kubwa ambayo ametufanyia Wanambarali. Akichelewa kujenga kaka Bashe, sisi Wanambarali tutaanza wenyewe kumjengea lakini haimaanishi aje agombee Ubunge Mbarali, hapana! Anakuwa tu mkazi wa Mbarali. Pia, anaye Naibu Waziri bingwa kabisa, ambaye anamsaidia kazi na sina shaka na wananchi wa Tunduma watampa mitano tena; sina shaka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imejipambanua vizuri sana. Kiukweli kabisa wanayo nia ya dhati ya kuwasaidia wakulima kwa sababu wao wenyewe timu ya Wizara wanapenda kilimo na wanawapenda wakulima wa Taifa hili na ndiyo maana wamekuwa wakihangaika kwa dhati kabisa na shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanambarali kwa muda mfupi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyokuwa madarakani, tumepata miradi mingi ya kilimo mpaka tunashangaa. Hivi ninavyokwambia, tuna miradi mitano inaendelea; wakandarasi wapo huko na mimi huwa ninapita mara kwa mara. Kwa dhati kabisa ana timu nzuri sana ya Tume ya Umwagiliaji, kaka yangu Mndolwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wasaidizi wake pale *Engineer* Banzi, wanafanya kazi nzuri sana; ninawapongeza. Leo ukienda pale mradi wa Chosi unaendelea; Mradi wa Matebete unaendelea; Mradi wa Utulo unaendelea; Mradi wa Mbuyuni unaendelea; Mradi wa Msesule unaendelea, zaidi ya shilingi bilioni 80 tumeshapokea miradi yote inaendelea, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametuongezea pia miradi miwili ya shilingi bilioni 60 Mbarali. Mradi wa Madibira *phase two* na *phase three* yote inaendelea na tunashukuru inaanza. Pia, mradi mwingine wa Njombe – Isitu ambao unaendelea, tunashukuru

sana. Kwa kweli, sisi kule hatuna shaka tunasema Mheshimiwa Dkt. Samia mitano tena, hatuna shaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi mingine minne ambayo nimeshukuru sana Tume ya Umwagiliaji walifika, walikutana na wadau na wamesainishana mikataba. Miradi ile ambayo itaenda kwenye *World Bank*, inayofadhiliwa na *World Bank* ya *P4R* minne. Pale tuna Gwiri; tuna Igomelo; tuna Mwendamtitu; na tuna Mradi mwingine wa Utulo. Kwa kweli sisi tunaiona Mbarali baada ya miradi hii kukamilika, Mbarali itakuwa ni kitu kingine eti, kabisa, kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la miradi ya mabwawa. Nilikuwa huko Mbarali, sasa hivi kuna Mkandarasi anafanya *study* ya mabwawa. Mbarali peke yake tuna mabwawa saba yanayoenda kuchimbwa. Jamani sisi tuseme nini Mbarali, zaidi ya kumsubiria huyu mama na kumpa mitano tena tuanze kazi hii, aimalizie vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Bwawa la Rwanyo, tayari Mkandarasi ameshafanya tathmini; Bwawa la Mto Chimala; Bwawa la Kimani; Bwawa la Mto Mbarali; Bwawa la Dudumizi; Bwawa la Mambi; na Bwawa la Mto Ndembela, yote hii ni kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais anajaribu kutusaidia Mbarali tuondokane na matatizo makubwa. Ninaamini kabisa matatizo makubwa ya Mbarali ya migogoro mikubwa, hii ndiyo suluhu yake. Baada ya miradi hii kukamilika, nina uhakika kabisa tunakwenda kuua baadhi ya migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninayo maombi machache. Mheshimiwa Waziri, kwanza tukushukuru sana na tukupongeze sana kupitia hotuba yako ya jana. Umeweza kulirudisha shamba la ekari elfu sita na, kwa wananchi, tunakushukuru sana na Wanambarali wanakupongeza sana. Mheshimiwa Waziri tuendelee kutafuta maeneo kwa ajili ya wakulima wetu wadogo na hili eneo lililopatikana tunaomba liwafikie walengwa waliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusione sasa wanaenda kumegeana watu wachache tukarudi kwenye matatizo yaleyale badala ya kwenda mbele zaidi. Nimwombe sana tusimamie kwa uadilifu mkubwa, wakulima wadogo wa Mbarali waweze kusaidiwa wapate maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali. Tunakwenda kutengeneza uwanja ule wa John Mwakangale pale Mbeya wa Nanenane, uwanja ambao utakuwa ni mkubwa *East Africa* hakuna mfano. Tunashukuru sana Serikali, kupitia maonesho yale ya Nanenane yatawasaidia wakulima wa mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini kuweza kuonyesha umahiri wao kwenye suala zima la mazao; tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Bashe ambalo ninamwomba Waziri kwa dhati kabisa. Nimeona kwenye hotuba yake, kwamba wanakwenda kufungua matawi ya Benki hii ya Ushirika manne na wametaja tawi moja linaenda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshamaliza muda?

**MWENYEKITI:** Malizia nusu dakika.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kiukweli. Nimeona matawi manne ambayo yako Tabora, Mtwara, Dodoma, na Kilimanjaro. Niwaombe kwa Nyanda za Juu Kusini watuwekee tawi pale Mbeya. Ni suala muhimu ambalo litatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru kwa kupata nafasi. Mungu awabariki, tunawaombea Wizara ya Kilimo warudi waendeleze kazi hii na tunawapenda sana na wakulima wanasema "Mitano Tena." Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati Ndingo, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi mchana wa leo kuchangia bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia afya njema. Pia, niende moja kwa moja kwamba, ninaiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nianze kwa kuwapongeza askari miavuli wa Wizara hii ya Kilimo kuanzia: Mheshimiwa Bashe; Naibu wako Mheshimiwa Silinde; Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa namna ambavyo wamemsaidia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuweka rekodi mpya kwenye Sekta ya Kilimo ndani ya miaka minne ya Utawala wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imeshuhudia kauli mbiu mbalimbali. Kulikuwa na masuala ya "Siasa ni Kilimo"; "Kilimo cha Kufa na Kupona"; na "Kilimo Kwanza", lakini ndani ya utawala wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ajenda ya *10/30* imeleta matumaini na imekifanya kilimo kwa watu wengi kuwa kwamba inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapochangia bajeti ya Wizara hii ya Kilimo, binafsi ni shuhuda wa mafanikio yaliyopatika kwenye Sekta hii hususan nikijielekeza kwenye pembejeo na viuatilifu hasa vya zao la korosho. Mheshimiwa Waziri kwanza, hotuba umeiandaa ya kimataifa, hotuba nzuri ambayo imeainisha mafanikio unayaona moja kwa moja, nikupongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyosema jina la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan litaandikwa kwa wino wa dhahabu kwa namna ambavyo ameimarisha kilimo, lakini wewe Mheshimiwa Waziri ni Waziri pekee kwenye Wizara hiyo ya Kilimo ambaye ameweka rekodi ambayo itakuwa kwenye vizazi na vizazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mimi ni shuhuda. Tumefanya ziara na UWT-Taifa chini ya uongozi wa mama Chatanda na mama Shomari kwenye Mikoa ya Njombe, Lindi, Mtwara, Ruvuma na Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo hayo, kupitia mikutano ya hadhara kwenye kata na vijiji, tumepokea salamu za shukrani kwa wakulima, hususani wanawake. Tumeona kwa kushuhudia namna pembejeo zilivyowafikia wananchi, namna viatilifu vilivyowafikia wananchi na tumeshuhudia mabwawa haya yanayoendelea kujengwa na Wizara yako, likiwemo Bwawa la Membe la hapa Dodoma; binafsi nimetembelea bwawa hili, nilipangiwa kutembelea Bwawa la Msagali, Wilaya ya Mpwapwa. Tumeona *block farming,* ambayo ipo hapa Kata ya Makambako, ni kazi kubwa iliyofanywa na Wizara, lakini nimpongeze pia ndugu yangu Raymond kwa kazi nzuri aliyofanya katika sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi, pamoja na ongezeko kubwa la bajeti kufikia shilingi *1.2 trillion* na mabwawa yanayoendelea katika Mkoa wetu wa Pwani, wamefanya upembuzi yakinifu kule Rufiji, Ngorongo pale na Kibiti na pia, wameshapata mkandarasi, ombi langu ni wazitazame hizi skimu, ya pale Ruvu, Chauru na Bagamoyo, ni ambazo miundombinu yake ni chakavu. Wakitenga pesa kidogo tu pale, tunataka ukarabati wa miundombinu, kutujengea tuta kwenye Skimu ya Bagamoyo, ili kuzuia mafuriko na vifaa, kama trekta na *power tiller,* kwa ajili ya wakulima wetu, lakini wanashukuru sana kwa mbolea ya pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwenye Skimu ya pale Chauru wameomba kuongeza eneo la umwagiliaji hekta kama 1,300 zinaweza kutosheleza. Tunashukuru kwa *BBT* ya Kisarawe, wametuweka kwenye mpango kwenye wilaya 20, ambapo pale Palaka eneo limejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kiwanda cha kubangua korosho cha kwanza, baada ya miaka mingi vile vingine vya Kibaha kufa, wanakijenga Wilaya ya Kisarawe. Hivi karibuni, kama

wiki mbili zilizopita, Mama Chatanda alikitembelea pale Mzenga na kazi inaendelea. Tunaomba tu usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea viatilifu vya korosho kutoka kwa ambao wanendelea kugawa mbegu katika maeneo yetu. Ninataka niseme, Mheshimiwa Bashe amepewa maua yake, siku ile ya kuzindua benki ya ushirika mimi binafsi nilikuwa kwenye Wilaya ya Nzega, kwenye mkutano wa ndani, Mambali pale, Mwamala na maeneo mengine; nimemsemea vizuri kwamba, Wilaya ya Nzega na Mkoa wa Tabora imetupatia kijana mpambanaji. Niwatakie kila la kheri na ninawaomba wawarudishe ninyi wote wawili na ikimpendeza Mwenyezi Mungu waendeleze hii ajenda ya 1030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, lakini kwa kweli, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweka rekodi ambayo itaishi vizazi na vizazi kwa kutuwezesha, hasa wanawake ambao ni 65% wanaojihusisha na kilimo, kupata pembejeo na bei nzuri ya mazao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Mgalu, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa *Dkt.* Hamisi Kigwangalla, Mheshimiwa *Eng.* Mwanaisha Ulenge, Mheshimiwa Regina Ndege na Mheshimiwa Cecilia Paresso ajiandae.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa ya kusema hapa Bungeni siku ya leo. Awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyejalia uhai na ametupa fursa ya kukutana tena kutimiza majukumu yetu hapa Bungeni siku ya leo. Pili, nitumie fursa hii, kwanza kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa utendaji wake uliotukuka na hususan kwa kuleta miradi mingi ya maendeleo kwenye Jimbo letu la Nzega, lakini pili nimshukuru kwa kuendelea kumwamini Waziri wetu wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, niwapongeze Mheshimiwa Rais, Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Waziri Hussein Bashe, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu ndugu Mweli na

watendaji wote wa Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kwenye sekta hii nyeti, ambayo ni uti wa mgongo wa maisha ya Watanzania, ni uchumi wa Watanzania. Bajeti ya kilimo ni bajeti ya watu na kwa namna ambavyo Mheshimiwa Rais na Waziri, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, wanafanya kazi kwenye Wizara hii ni wazi kabisa majina yao siyo tu yataandikwa kwa wino wa dhahabu, lakini pia, yatakuwa *casted* kwenye mwamba imara wa jiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, leo nimekusudia kuongelea jambo moja tu na ndilo ambalo kwa kweli, limeniinua niseme hapa Bungeni siku ya leo baada ya kuwa kimya kwa muda mrefu na lenyewe ni suala la umwagiliaji. Kama kuna jambo la busara, la hekima na la mapinduzi ambalo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, akiongozwa na utashi na mwongozo *(vision)* sahihi wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, litafanywa katika nchi yetu tayari, tumeanza kufanya kwa uchache wake na ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti hii unaona sasa tunaenda kimkakati na kwa ukubwa zaidi, basi ni suala la umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo litaenda kuleta mapinduzi makubwa kwenye maisha ya watu, ni jambo ambalo kiukweli sina maneno mazuri zaidi ya kuwapongeza, lakini binafsi kwa uelewa wangu mdogo wa uchumi wa mwaka 2050 unaokuja, naona litaenda kui-*position* Tanzania kwenye nafasi kubwa na ya kipekee sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo niwapongeze sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kuamua kuwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye eneo la umwagiliaji. Kwa nini nasema hivyo? Ukisoma Taarifa ya Idadi ya Watu Duniani, ambayo inatolewa na Shirika la Kiuchumi na Maendeleo ya Watu la Umoja wa Mataifa iliyotoka mwaka 2022, *World Population Prospects* ya mwaka 2022, unaona Dunia kufikia mwaka 2050 itafikisha idadi ya watu takribani bilioni 10, bilioni 9.7 Afrika, ambayo ndiyo itakuwa ina ukuaji wa hali ya juu wa idadi ya watu, itakuwa na mchango kwenye idadi hiyo wa takribani 25%. Katika nchi za Afrika ambazo zitakuwa zina ukuaji mkubwa

wa idadi ya watu Tanzania ipo kwenye *top four,* ikiwemo *DRC*, Nigeria na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, kutakuwa kuna changamoto kubwa sana ya uhakika wa chakula, *food security,* ifikapo Mwaka 2050, lakini Tanzania tuna bahati na fursa ya kipekee; tuna maziwa na mito ya maji baridi. Tunaweza tukawa *food exporters* kwa nchi za jirani na pia, kwa dunia kwa ujumla wake, lakini pia, Tanzania tutakuwa na changamoto ya kuwalisha takribani Watanzania milioni 140 ambao wanakadiriwa, kwenye ripoti hiyo, kuwa watakuwepo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mbali na uwepo wa idadi kubwa ya watu miaka 25 tu ijayo wengine humu, kama tutajaliwa kuwa hai, tutashuhudia. Tutakuwa tuna fursa ya kuwa na *food exporters* kwa nchi za jirani na nyinginezo, kwa hivyo, Mheshimiwa Bashe, endelea kuwekeza kwenye diplomasia ya chakula, *food diplomacy,* kama juzi hapa alivyofanya kwa wenzetu, ili tujenge soko imara kwenye uchumi unaokuja katika dunia, ambapo sisi tunakadiriwa kuwa ni miongoni mwa nchi ambazo zitakuwa zinakuwa kwa kasi zaidi kwa idadi ya watu na pia, kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo gani tufanye. Mheshimiwa Bashe kwenye ripoti yake ameanzisha mradi mkubwa sana kutoka Ziwa Victoria na pia, kutoka Ziwa Tanganyika, ambao utakuja mpaka huku ndani kabisa ya nchi yetu. Ninampongeza kwa wazo hilo, ninaamini mradi huu ukitekelezwa, kama ambavyo anaeleza kwenye ripoti yake, utakuwa umefanya jambo la kukumbukwa katika historia kama ambavyo Farao Amen Het wa kule Misri anakumbukwa kwa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji. Utakumbukwa kama wale wa Iraq ama Wambulu walivyofanya Skimu yao ya Umwagiliaji kule Engaruka miaka takribani 500 na 600 iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi unashangaa kwamba, sasa sisi watu wa leo tunashindwa akili na *ancestors* wetu wa miaka 500, 600 iliyopita? Kwamba, kwa nini tulikuwa hatuendi kwenye kilimo cha umwagiliaji wakati tuna historia ya kuwa na

skimu miaka 600 iliyopita kule eneo la Engaruka Katikati ya Mlima Oldonyo Lengai na Bonde la Ziwa Natroni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini leo hii hatuna kilimo cha umwagiliaji? Kwa nini Skimu ya Engaruka ilikufa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tukijifunza pale tu tunapata somo kubwa sana la kui-*position* Tanzania, kama *giant food manufacturers* na *food exporter* katika dunia inayokuja kwa hivyo, nikupongeze kwa kufikiria wazo hili. Mambo ya kuzingatia ya muhimu, kwa sababu ya muda; lazima skimu hii kubwa ambayo unaijenga, achilia mbali hizi nyingine mbalimbali ambazo mmeanza kuzijenga ikiwemo Skimu yangu ya kule Budushi, ya kule Manonga, Nehele na maeneo ya jirani, hii skimu kubwa ambayo inakuja, Waziri ahakikishe wanavyoi-*design* wawe wamei-*pair up*, wamei-*link up* vizuri, wameifungamanisha na wazalishaji kwa sababu, kwenye hiyo ripoti ya mwaka 2050 zaidi ya 50% ya Watanzania watakuwa wanaishi kwenye majiji. Maana yake ni wakulima hawa wa leo wa jembe la mkono hawatokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha wakati huo kitakuwa ni cha kibiashara, kitakuwa ni cha watu wakubwa zaidi, kwa hivyo kitatoa ajira nyingi, kitatusaidia kutatua tatizo la ajira ambalo linakusudiwa kuwa ni tatizo mama la mwaka 2050. Kwa hivyo, huu mkakati wanaoenda kuwekeza sasa hivi ni mkakati ambao utapunguza vurugu na *chaos* ambazo zinatarajiwa, kama tusipo tatua tatizo la kuwa na *young population* kwa zaidi ya 65% ifikapo mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lazima scheme hii iwe *designed* kufanya *Agro-industrialization*. Kuwe kuna viwanda pembeni ya skimu, kuwe kuna ushirika ambao unakuwa *linked* na ku-*manage* hizi skimu. Kuwe kuna ulinzi wa vyanzo vya maji, mito, mabonde na pia, kuwe kuna mkakati mzuri wa *GIS,* kutumia *better science*, kwa ajili ya ku-*manage* idadi ya watu katika Taifa letu na namna wanavyosambaa kwenda kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Skimu ya Engaruka ilikufa kwa sababu, Wamasai ambao ni wafugaji walienda kuwavamia Wambulu. Hata huko mbele hivyo hivyo wafugaji watavamia maeneo ya wakulima, kwa hivyo, ili kilimo kiwe salama ni lazima mikakati ya kulinda maeneo ya ardhi ya kilimo iwekwe vizuri; kuwe kuna upimaji, lakini pia, kuwe kuna ugawaji mzuri wa maeneo, ili ardhi ambayo ni *fertile* ya kilimo isipotee kwa sababu, hatujajipanga vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwe kuna uendelevu wa mradi huu ni lazima uanzishwe Mfuko wa Kilimo cha Umwagiliaji ambapo, kutakuwa kuna muda mrefu wa kutekeleza miradi ya umwagiliaji, kutakuwa kuna vyanzo vya uhakika vya fedha na hakutokuwa na athari, ambayo itasababishwa na mabadiliko ya viongozi kwenye hii Wizara. Hapa sasa hivi namwombea dua, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais asimwondoe kwenye Wizara hiyo mpaka miradi hiyo aimalize.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kigwangala.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima sasa mifumo iwekwe na Serikali, ambayo italinda kilimo cha umwagiliaji na miradi mikubwa kama hii kwa muda mrefu, kama tulivyofanya kwenye barabara na tunavyofanya sasa kwenye reli. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa *Eng.* Mwanaisha Ulenge, Mheshimiwa Regina Ndege na Mheshimiwa Cecilia Paresso, dakika tano tano tu.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini kipekee kabisa nichukue fursa hii kuishukuru sana Serikali kwa mageuzi makubwa katika Sekta ya Kilimo nchini kwetu, hakika tumeyaona kuanzia miaka ya 90 kwa majina mbalimbali, kama watangulizi wangu waliozungumza

wameweza kuyataja hapa, lakini *commitment* ya kweli ya yenye mikakati ya uhakika imetokea kufanyika wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweka *commitment* ya kibajeti na kwa kupitia watendaji mahiri, kama kaka yangu Mheshimiwa Bashe pamoja na wasaidizi wake kwenye Wizara hii ya kilimo wakiongozwa na kaka yangu ndugu Mweli. Hakika wameweka mikakati inayokwenda kuonesha taswira ya kweli ya tunakoelekea kwenye mageuzi ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani nyingi za dhati, hakika tunakoelekea tunaona taswira kubwa. Mioyo yetu inafarijika kwamba, leo Tanzania badala ya mkulima kuwa na hofu ya kutegemea mvua itanyesha lini, tunakwenda kukimbia mvua zisizokuwa na uhakika, mvua haribifu; unakwenda kuchimba na kuwa na uhakika wa kumwagilia, hakika haya ni mageuzi makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutuwezesha Mkoa wa Tanga shilingi bilioni 11, kwa ajili ya mashine zile za mkonge. Mheshimiwa Rais amesema tusiziite tena korona, tunawashukuru sana, wamewajali wananchi wa Mkoa wa Tanga na hakika Serikali imesimamia kwa dhati zao hili la mkonge kuendelea kuwa la biashara Kimataifa. Tunatoa shukrani zetu nyingi sana, kwa ajili ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika shilingi bilioni 11 zile zitasababisha kuzalisha mkonge wa *grade* ya juu kwa sababu, *the more we delay* kwa sababu ya kutopatikana mashine *the more product* inakuwa imepungua ubora wake. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa *commitment* hiyo ya fedha nyingi ndani ya Mkoa wetu wa Tanga, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia, nitoe shukrani zangu za dhati, kwa ajili ya kituo atamizi kilichopo pale Tanga Jiji, kwa ajili ya kuzalisha bidhaa zinazotokana na mkonge kwa kutumia

mikono yetu wanawake wa Mkoa wa Tanga. Vijana wa Mkoa wa Tanga na hata watu wenye ulemavu wametengenezewa kituo kile na Serikali imeweka *commitment* ya shilingi milioni 600, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunaishukuru Bodi hii ya Mkonge ya Tanga, hakika inafanya kazi nzuri sana kwenye kituo hiki, nimekitembelea, nimeona. Ninaomba sana Serikali ijitahidi kuhakikisha shilingi milioni 600 hizi walizoziweka kwenye kituo atamizi zinafika pale, ili wakufunzi wale waweze kulipwa ipasanyo, ili mashine zile ambazo bado hazipo pale ziweze kuwepo, ili mafunzo yale yaweze kuleta tija kwa haraka. Shilingi milioni 600 zile tunaziomba kwa haraka ipasavyo, ziende kuongeza nguvu katika kituo kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo atamizi cha Mkoa wa Tanga matamanio yetu siyo tu kuzalisha bidhaa zinazotokana na mikono ziuzwe ndani ya Tanzania, tunatamani kuona zile *trade centers* zilizopo nchi mbalimbali, kwa ajili ya mazao ya mkonge na *products* za mkonge zinakwenda kurudi. Mheshimiwa Bashe, historia inaonesha kulikuwa na *trade centers* katika nchi mbalimbali, ambapo *products* za mazao ya mkonge zilikuwa zinafika kule na watu wananunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye balozi zetu mbalimbali tulikuwa tunakuta bidhaa za mkonge kule. Sasa hivi ukienda kwenye balozi zetu zote utakuta kahawa ya Kilimanjaro, lakini bidhaa zile za mkonge za Tanga sasa hivi hazipo, tunaomba warudishe *trade centers* zile kwa kuanzia na vituo atamizi kama hivi, ili tufanye biashara za Kimataifa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kukukwaza, dada yangu. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha. Nilimtaja Mheshimiwa Regina Ndege, Mheshimiwa *Regina* Paresso atamalizia.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, bajeti ya wananchi. Ili kuweza kuongoza nchi kwa utulivu ni lazima kuangalia usalama wa chakula na hili Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema ameweza kwa sababu, ni kwa kipindi chake amekwenda kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo kutoka shilingi bilioni 294 hadi shilingi trilioni 1.2. Hii siyo kazi rahisi, Mheshimiwa Rais ameonesha kwa vitendo dhamira yake njema kuhakikisha Watanzania walio wengi wanakwenda kufanya mapinduzi makubwa kwenye kilimo hii Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ameendelea kutupigania Watanzania. Ninashukuru na ninampongeza sana Waziri wa Kilimo, ndugu yetu Mheshimiwa Hussein Bashe, msaidizi wake Naibu Waziri, Mheshimiwa Silinde, Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Kilimo pamoja na watumishi wote kwa namna ambavyo wanasimamia kwa vitendo dhamira njema ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kilimo cha Tanzania kinakuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kuongelea suala la kilimo cha umwagiliaji. Tumekuwa tukiongelea suala la umwagiliaji kwa muda mrefu, lakini tumeona kipindi hiki cha Awamu ya Sita, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekwenda kufanya mapinduzi makubwa kuhakikisha ameanzisha skimu za umwagiliaji katika maeneo mbalimbali. Katika Mkoa wetu wa Manyara tumepata skimu nyingi; tumepata Skimu ya Bashay, Kiru Six, Matufa, Kisangaji, Gichameda, Tlawi na maeneo mengine. Maeneo haya kwa sasa yanazalisha vitunguu, mpunga na viazi. Tunaona ni kwa namna gani wananchi wetu wamekwenda kujikomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kushauri; kwa sababu, kilimo tulichonacho cha umwagiliaji kwa sasa ni kwa njia ya mifereji, ninapendekeza, Mheshimiwa Waziri, tuangalie namna ya kuweka umwagiliaji kwa njia ya matone ili tuweze kumwagilia maeneo makubwa zaidi. Kwa sababu kwenye umwagiliaji wa

mifereji tunaweza kumwagilia. Kwa mfano mtu analima heka moja, lakini tukipeleka kwa njia ya umwagiliaji wa matone *(drip irrigation)* tunakwenda kumwagilia maeneo makubwa zaidi badala ya heka moja mtu unamwagilia hadi heka nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninapenda nipendekeze hili ili Wizara ione namna gani ya kwenda kusaidia wananchi wetu ambao tayari wamejihusisha na kilimo cha umwagiliaji wakamwagilie maeneo makubwa na kuzalisha mazao ya kutosha katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze kwa kuanzishwa kwa maabara ya kuanzisha miche. Hili linakwenda kuleta mapinduzi makubwa kabisa kwa sababu tutapata miche iliyo bora, miche ambayo inaweza ikastawi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kwamba *pilot* ianzie katika Mikoa ya Manyara, Arusha na Kilmanjaro; kwa maana ya kwamba tutakwenda kuzalisha zaidi kulingana na mazingira yetu. Kwa hali ya hewa iliyo katika maeneo yetu tupate miche ya kutosha ili wananchi wetu wakazalishe mazao ya kutosha. Pia Mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro ni wazalishaji wazuri pia wa zao la ndizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara itafute namna ili tuwekeze kwa kiwango kikubwa katika mikoa hii niliyoitaja uzalishaji wa ndizi ili tuzalishe zaidi na kwenda kufanya *export* ya mazao yetu na kupata fedha za kutosha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kuomba Serikali isogeze huduma ya kifedha ya Benki ya Kilimo pamoja na ule Mfuko wa Pembejeo. Benki hizi ziko kikanda, kwa hiyo niombe sasa Serikali itafute namna ya kuwasogezea wananchi katika maeneo yao ili mtu anapohitaji kukopa iwe rahisi kupata mikopo badala ya kusubiri watu kutoka maeneo ya kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze uboreshaji wa *TARI* na *ASA* katika kuboresha uboreshaji uliyofanyika. Niendelee kuomba, kwamba sasa Serikali itafute namna ya kuboresha miundombinu,

iboreshe vifaa, iwaboreshee wataalam wetu na kuwapatia ujuzi wa kutosha ili waweze kwenda na kasi iliyopo pamoja na kwenda na mazingira tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiagiza baadhi ya matunda katika nchi yetu kutoka nje; kwa mfano, mapeasi na matunda kama ma-*apple*. Niombe Serikali itafute namna ya kwenda kuzalisha mazao haya au matunda haya katika maeneo yetu. Mfano mdogo tu, kwamba tunayo maeneo ambayo tunaweza kuzalisha matunda kama peasi, *apple,* mfano, Babati, Manyara, Mbulu, tuna uwezo wa kuzalisha matunda haya. Kwa hiyo niombe matunda haya yawekewe msisitizo ili tuweze kuzalisha hapa nchini badala ya kuagiza nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na niwatakie sana Wizara ya Kilimo utendaji mwema. Ninaunga mkono bajeti hii ya Wizara ya Kilimo kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Regina Ndege. Nilimtaja Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Kilimo. Pia niungane na Waheshimiwa Wabunge kwanza kwa dhati kabisa kumpongeza Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hasan kwa kuhakikisha kuwa mapinduzi makubwa kwenye sekta ya kilimo yanafanyika; na hii ni sambamba na kuongeza bajeti ya kilimo kwa 324.49%. Niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu maono ya Rais wetu wao wanayasimamia na tunaona mabadiliko. Tunawapongeza sana na hongera sana kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ukuaji wa sekta ya kilimo umeongezeka, tunaona na tunashuhudia. Kwa hiyo tunatarajia na ni matumaini ya Watanzania kwamba mapinduzi haya yako mengine ambayo matunda yake hatuwezi kuyaona moja kwa moja leo, lakini tunatarajia miaka kadhaa ya mbele

tuweze kuona haya mapinduzi yanawasaidia Watanzania ambao asilimia kubwa ni wakulima katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nizungumzie wananchi wangu wa Karatu, hasa katika Bonde la Eyasi ambao ni wakulima wa vitunguu. Wakulima hawa; tunafahamu na tunaishukuru Serikali kuna mradi mkubwa pale wa umwagiliaji unaendelea wa shilingi bilioni 21.5; ninatambua kwamba kazi hii inaendelea japo imesuasua kidogo, lakini angalau kuna kazi inaonekana. Kwa hiyo ni matarajio yetu kwamba kazi hii kwa mujibu wa bajeti iliyotengwa itakamilika ili wananchi katika bonde hili la Eyasi waweze kupata uhakika wa kilimo chao; kwa sababu miundombinu yao ya umwagiliaji itakuwa imeimarika kulingana na bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo wana changamoto moja. Ninafahamu kuwa si ya Wizara ya Mheshimiwa Waziri moja kwa moja, lakini kwa sababu yeye ni msimamizi wa wakulima nina imani atasaidiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kusimamia hoja ya vifungashio vya hao wakulima wa vitunguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hawa wamekuwa wanatumia vifungashio vya kila aina; wana vifungashio vyenye majina tofauti. Kuna kifungashio kinaitwa *Net* ya Magufuli ambayo ina ujazo wa debe 7.5, kuna *Net* ya Samia ina ujazo wa debe 8.5 na kuna *Net* ya Mkenya yenye ujazo wa debe 15. Sasa wananchi wamekuwa wakichanganywa mno; na kila mnunuzi anayekuja na *net* yake ananunua kwa mahitaji yake, si uhitaji wa soko wakati huo ukoje. Kwa hiyo, imekuwa ikiwaumiza wakulima kwa kiwango kikubwa sana

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Wizara kuwe na vifungashio sahihi vyenye ama ujazo sahihi au turudi kwenye ule utaratibu wa kutumia kipimo cha kilo kwa sababu ninadhani hii ndiyo *standard.* Kilo moja inapimwa, tunajua mwananchi huyu kwenye kilo moja akichukua ile *net* inakuwa imeingia kiasi gani cha kilo kwenye *net* husika. Kwa hiyo, imekuwa ni changamoto ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, tuwasaidie wakulima wetu, hasa hawa wa Bonde la Eyasi. Ukifika pale Bonde la Eyasi anayepanga bei tuna Wakenya kule wamejaa, ndiyo wanaopanga bei, ndiyo wanaoamua soko na ndiyo wanaokwenda mashambani. Kwa namna yoyote; pale na madalali hapo katikati; wanawapangia wakulima. Yaani wanachukua kwa bei wanayotaka wao. Unajua zao la vitunguu linavyolima, yaani linabembelezwa kama mtoto. Ukikosea tu *stage* moja umeharibu na uwekezaji wake ni mkubwa kwa sababu unahitaji uangalizi wa karibu. Tunaomba sana kwa dhati wakulima hawa wasimamiwe, huu utaratibu wa wanunuzi kwenda mpaka mashambani ukomeshwe, watu wanunue kwa mujibu wa bei iliyopo sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ni suala la lumbesa, suala la lumbesa pia, tunaomba wakulima wasaidiwe, wasimamie suala la lumbesa kwa nchi nzima. Tukiweka mkazo upande mmoja wa Bonde la Eyasi kwa wakulima hawa, wanunuzi hawa wanakimbilia upande mwingine. Kwa hiyo ninaomba sana washirikiane na Wizara nyingine ya Kisekta ili wasimamie kukomesha suala la lumbesa kwenye mazao yetu, hasa zao hili la vitunguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna skimu nyingine muhimu sana ya umwagiliaji, ninadhani hii haifahamiki sana, tunaifahamu zaidi hii ya Bonde la Eyasi, lakini tuna skimu nyingine kwenye Kijiji cha Chemchem katika Kata ya Rhotia, Wilayani Karatu; ni bonde zuri sana. Tunaomba nalo lifikiriwe kutengenezewa miundombinu ya umwagiliaji na skimu bora. Tunajua itawasaidia watu wengi sana kwenye eneo lile kuhakikisha wanazalisha, hasa wanaozalisha mbogamboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kuwa eneo letu la Karatu ni eneo la kitalii, tuna hoteli nyingi. Tukiwasaidia akinamama hawa na wananchi wa pale, tukawa na skimu watazalisha mboga za kila aina na siyo utaratibu wa sasa kuchukua mboga mbalimbali kutoka Arusha ilihali tuna ardhi inayotosheleza na tuna maeneo. Watusaidie ili tupate skimu ya umwagiliaji katika eneo hili ili kuwakwamua wananchi katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la muhimu. Wilaya ya Karatu pia tuna wakulima wa ngano. Kumekuwa na changamoto ya mbegu za ngano. Mbegu hizi wakati mwingine wananchi wanaletewa na kampuni kubwa kubwa. Kuna hawa wa *Breweries* wa Serengeti, kila kampuni inaleta mbegu yake, wanakwenda kwa wakulima, wakulima wamepata changamoto mbegu si bora na hazioti kwa wakati. Tunaomba Wizara wasimamie suala hili la ubora wa mbegu ya zao la ngano katika eneo letu la Karatu na katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni kuhusu mbegu ya ruzuku. Tunaipongeza na kuishukuru Serikali kwa utaratibu mpya wa kuweka ruzuku kwenye mbegu zetu za mahindi. Tunaomba; tuimeshuhudia mwaka huu kulikuwa na utaratibu ambao kwa namna moja au nyingine ama wananchi hawakuufahamu au kwa sababu ni utaratibu mpya umekuwa na changamoto. Tunaomba waboreshe zaidi ili hii mbegu ya ruzuku ambayo tunaamini ni nia njema ya Serikali kupitia Mama Samia iweze kunufaisha wananchi wote ambao wana uhitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso. Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa kipindi hiki cha asubuhi.

Kabla sijasitisha shughuli zetu za Bunge nitawataja Waheshimiwa watatu ambao wataanza kuchangia jioni. Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mheshimiwa Selemani Kakoso na Mheshimiwa Mariam Nyoka na wengine watafuatia baadaye.

Baada ya kusema hayo, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.08 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa, majadiliano yanaendelea. Tunaanza majina yaliyokwishatangazwa. Tunaanza na Mheshimiwa Justin Nyamoga, ajiandae Mheshimiwa Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Nyoka, Mheshimiwa Yustina na Mheshimiwa Godwin Kunambi.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Wizara hii muhimu ya Kilimo. Nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati na pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na kubwa katika uboreshaji wa masuala mazima ya kilimo katika nchi yetu, na pia katika Jimbo la Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengi sana ambayo yamefanyika ambayo Wanakilolo wanashukuru. Wanakilolo wanashukuru sana kwa ruzuku ya mbolea ambayo inaendelea kutolewa na Serikali hii ambayo imeendelea kupaisha kilimo katika Wilaya ya Kilolo. Pia, tunayo shukurani kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais, pia kwa Mheshimiwa Waziri Bashe, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Wizara nzima kwa ujumla kwa uhusiano mzuri na ushirikiano ambao mimi kama Mbunge wa Jimbo la Kilolo nimeupata wakati wa kufuatilia mambo magumu ambayo

yalikuwepo, lakini Wizara hii ikaweza kuyatatua katika kipindi hiki. Siwezi kutaja mengi, lakini nitaje machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, Mheshimiwa Waziri atakumbuka alipokuwa Naibu Waziri, alifika Kilolo pale kwenye Kiwanda cha Chai na kwenye mashamba ambayo yalikuwa yametelekezwa kwa miaka 30. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, baada ya ziara ile ilikuwa ni mwanzo wa safari ya ukombozi kwa Wanakilolo kwenye mustakabali mzima wa masuala ya chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyozungumza, yule mwekezaji ambaye ni kampuni ya kutoka China ameshakamilisha ujenzi wa kiwanda, kimekamilika, na kiko kwenye majaribio. Kazi kubwa iliyopo ni Mheshimiwa Waziri mwenyewe na *delegation* yake, pia na viongozi wengine kufika pale kwa ajili ya uzinduzi wa kiwanda kile kwa ajili ya kazi sasa kuanza kuendelea kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya kiwanda kile kazi ndogo iliyobaki kwanza ni ya kuhakikisha kilimo cha chai kinafanyika kwenye eneo lile la hekta 3000 ambazo zipo, zimetengwa baadhi kwa ajili ya *BBT,* ili kukuza upandaji wa chai ambayo italisha kiwanda kile ili kutosheleza kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri uliopo kwa kiwanda kile, mwekezaji ni kampuni ya kutoka China. China ni soko kubwa la chai, kwa hiyo, kwa vyovyote vile hatutakuwa na ugumu wa kupata soko kwa sababu mzalishaji mwenyewe ana soko kwenye nchi yake. Najua huo ni mlango hata kwa ajili ya viwanda vingine kwenye nchi hii. Kwa hiyo, ni vizuri kuweka jicho pale kuona pia *performance* ya hiyo kampuni kwa sababu, nchi yake ina soko kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuona *performance* yake ili kuangalia soko la chai kwenye nchi kwa ujumla, tunaweza kunufaika vipi na soko ambalo watakuwa wamelianzisha wao? Kwa hiyo, pia kuna haja ya uzalishaji wa chai ile kuwa bora

kwamba inaweza kuvutia wale wateja kwenye nchi hiyo na hapo tutakuwa tumefanya jambo la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulizungumzia. Mheshimiwa Waziri atakumbuka, nimezungumza naye kuhusu *horticulture* hasa kwenye kilimo cha matunda na mbogamboga. Ili uchumi wa nchi uweze kukua, lazima ipunguze sana *import* na iongeze *export*. Sasa sisi tuna-*import* sana matunda, tuna-*import apple*, *pears, peaches,* lakini matunda hayo yote niliyokutajia yanaweza kuzalishwa vizuri sana kwenye baadhi ya maeneo ya nchi yetu, hasa Kilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ilikuwa kwamba badala ya kuendelea kutumia miche iliyopo ambayo imezeeka sana ambayo ni ya tangu wakati wa ukoloni ndiyo imepandwa, tuna haja ya kuanza kuleta miche bora kwa ajili ya matunda, na pia kuweka viwanda vya matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa matunda tu, uzalishaji wa *apple* tu, uzalishaji wa *peaches* tu, uzalishaji wa *peas* tu, ungeweza kutosheleza mahitaji na hata wakati ambapo inatokea hao watu wanakuwa wakorofi na kufungwa masoko hayo, bado ndani ya nchi tungeweza kujitosheleza. Najua tuna nafasi bado ya kuendelea kuhakikisha kwamba tunakuza soko la *horticulture* kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba ili tuweze kufanya vizuri kwenye kilimo, tunahitaji *integrated programing,* yaani kuhakikisha kwamba kilimo kinaambatana na yale mahitaji muhimu. *AGRI-CONNECT* ambao ulikuwa ni mradi ambao unahusisha kilimo na miundombinu ulifanikiwa sana hata Kilolo kwa mfano kwa sababu mazao yanayozalishwa yanatakiwa yasafirishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama miradi ya kilimo itaambatana na *component* za usafirishaji, tunakuwa tumefanya jambo la muhimu sana. Kwa kuwa kulikuwa na *project* ya *AGRI-CONNECT* ambayo imejenga barabara kwa mfano kutoka

Kidabaga kwenda Boma la Ng'ombe na inaendelea ina kilometa saba, lakini ile *project* ya *AGRI-CONNECT* inaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba ni vizuri kufanya mazungumzo na wale watu ambao wamefanya *project* ya *AGRI-CONNECT* kuona namna tunavyoweza kuendeleza miundombinu ya barabara ili wakulima wa maeneo ya pembezoni waendelee kupata mindombinu mizuri ya barabara. *AGRI-CONNECT* iliimarisha zaidi ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, lakini yako maeneo ambayo yanahitaji madaraja tu, na yako maeneo ambayo yanahitaji barabara nzuri kwa kiwango cha changarawe tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hoja yangu ni kwamba ni vizuri Wizara ikafanya mazungumzo na *AGRI-CONNECT* kufanya uendelevu wa ujenzi wa miundombinu ya barabara hasa kwenye maeneo yenye fursa za kilimo kama ambavyo ilifanyika ili huu mradi usiishie pale. Kama utaishia pale, basi kuna maeneo mengi, kwa mfano, Wilaya ya Kilolo ambayo yana fursa kubwa sana za kilimo, lakini kinachotatiza usafirishaji wa mazao, ni barabara ambapo sasa inashusha bei na wakulima wanakosa kupata bei nzuri na kwa hiyo, uendelevu wake unakuwa mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kama *AGRI-CONNECT* au mazungumzo yatafanyika ili kuwa na mradi mwingine wa *programming* kama ile, hata kama ni wa fedha za ndani, au fedha za nje, ni miradi mizuri sana ambayo itawakuza wakulima kwa sababu hatuwezi kuangalia jambo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni kuhusu umwagiliaji. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake pamoja na Katibu Mkuu kwamba skimu zote kubwa za umwagiliaji za Kilolo zinapata fedha. Skimu ya Ruaha Mbuyuni ameipa shilingi bilioni nne na ujenzi unaendelea, Skimu ya Mgambalenga ameipa fedha japo ujenzi ulisimama, lakini nimetaarifiwa kwamba fedha zimepatikana. Kwa hiyo, wataendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Skimu ya Nyanzwa wameifanyia usanifu na nimeona kwamba iko kwenye bajeti, itapata fedha kwa ajili ya kuendelezwa. Naomba sana, haya mabonde yaangaliwe kwni yangeweza kusababisha pia uzalishaji wa mazao mbalimbali kukua na wananchi wale kujikomboa kiuchumi hasa kwenye maeneo ya Ruaha Mbuyuni, na Nyanzwa kwa sababu yale ni maeneo makavu, yanahitaji sana kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika kwamba kwenye uwekezaji wa umwagiliaji, kama hayo yatafanyika, basi tutakuwa tumefanya jambo kubwa sana litakalowezesha uzalishaji wa mazao haya uweze kusababisha kufanikiwa kwenye sekta nzima ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi skimu nilizozitaja hasa ile ya Ruaha Mbuyuni ina-*accommodate* wakulima wengi sana, zaidi ya wakulima 10,000, na hao ni wakulima wengi ambao wote wanategemea kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, kutolewa fedha zile shilingi bilioni nne sasa, ni msukumo tu wa yule mkandarasi kuhakikisha kwamba anamaliza kwa wakati, lakini nafahamu, Naibu Waziri anafahamu, pia namshukuru sana Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji pia anafahamu na anafuatilia kwa ukaribu, na hilo ni jambo la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu kilimo cha parachichi. Kwanza naishukuru sana Wizara kwa kujenga kiwanda kwenye Mkoa wa Iringa. Najua kinajengwa Nyororo, lakini ni muhimu sana kwetu Wanakilolo kwa sababu sisi wote pia ndipo tutakapopeleka mazao. Ombi langu ni kwamba ujenzi wa kiwanda kile iende kwa kasi ili Wanakilolo wapate soko zuri, maana kukiwa kuna kiwanda kutakuwa kuna jambo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nimkumbushe Waziri, yeye mwenyewe alifuatilia sana uanzishaji wa kitalu cha miche ya parachichi Kilolo, na *TARI* walianza kufanya hiyo kazi, na walifanya vizuri sana mwanzoni, lakini baadaye kukawa na kusuasua kidogo. Kile kitalu tukifanya tathmini, kufanikiwa kwake kumekuwa kwa asilimia ndogo. Sasa huku tunakoendelea, *issue* kubwa ni

suala zima la miche. Kwa hiyo, naomba sana na hilo pia tuendelee kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana, Mwenyezi Mungu akubariki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa sasa namwita Mheshimiwa Kakoso.

Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda dakika tano tano kwa kuwa wachangiaji ni wengi na Waziri ana majibu mazuri. Kwa hiyo, tutakuwa na dakika tano tano, nendeni *specific* kwenye *issues* zile ambazo unafikiri ni muhimu katika eneo lako.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nami nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kufanya maboresho makubwa sana kwenye sekta ya kilimo. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, na Watendaji wote wa Wizara kwa juhudi kubwa ambazo wamezifanya hasa katika kukuza masoko kwenye maeneo ya mazao ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona ufanisi mkubwa umefanyika kwenye zao la tumbaku, na saa hizi kuna ongezeko la uzalishaji mkubwa sana kutoka tani 117,000 mpaka kufika 160,000. Ni maendeleo makubwa sana ya zao ukiangalia lilipokuwa huko chini. Ilishuka sana, lakini tunafurahishwa sana na bei ya zao kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya zao kwa wakulima walio wengi wanafurahia uhalisia wa kile wanachokipata. Vilevile, tunaipongeza Serikali kwenye maeneo ya kuleta pembejeo. Tumepokea pembejeo ambazo zina ruzuku ya Serikali zinazokaribia shilingi bilioni 7.6. Haya ni maendeleo makubwa sana kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo napenda kuishauri Serikali ni kwenye miradi ya umwagiliaji. Kwenye eneo hili bado hatujafaulu, jimboni kwangu mimi nina Mradi wa Skimu ya Karema

na Serikali iliahidi kutoa shilingi bilioni 30 ili ule mradi uweze kukamilika. Eneo lile tunaomba Serikali itoe fedha ili skimu ile iweze kukaa vizuri na iwasaidie wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tunaishauri Serikali ni kwenye suala la mazao ya chakula. Mheshimiwa Bashe kabla hajawa Waziri alikuwa mpambanaji sana wa kuwatetea wakulima ambao walikuwa wanalima mazao yao na wanapangiwa na Serikali, na hili leo hii umepewa dhamana. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri waachieni wakulima wazalishe na wanapozalisha wakipata kuuza sokoni bila kupangiwa, mazao yao yatapanda na tunawapa motisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mazao ya mahindi na mpunga. Kumekuwa na tabia Serikali inaangalia kwamba kuna uwezekano wa kuwa na njaa, wale wakulima tunawavunja moyo. Tunafunga mipaka, hili halijakaa vizuri. Naishauri Serikali iangalie na iwaachie wakulima wanapopata fursa wazitumie ili ziweze kuwaendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuishauri Serikali kwenye eneo la umwagiliaji. Tuna Ziwa Tanganyika ambalo halijatumika ipasavyo, Ziwa Tanganyika lina maji mengi na lina kina kirefu, ndiyo ziwa linaloongoza kuwa na maji mengi na safi lakini kwa bahati mbaya Serikali haijatumia rasilimali hiyo kwa sababu tunayategemea sana kwa ajili ya kunywa tu yale maji, lakini tungeishauri Serikali tuyatumie kwa ajili ya mfumo wa umwagiliaji, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso ahsante. Mheshimiwa Mariam Nyoka nilishakuita, jiandae Mheshimiwa Rahhi.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii adhimu ya kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu ya kilimo. Kwanza nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoipambania Wizara hii ya Kilimo pamoja na wasaidizi wake wote wakiambatana na Waziri wa Kilimo, Naibu

Waziri pamoja na Makatibu Wakuu wao na wasaidizi wao wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niende kwenye eneo la mafanikio ya Wizara hii ya Kilimo Fungu 43. Mafanikio ya fungu hili ni pamoja na ongezeko la bajeti kutoka shilingi bilioni 294 mwaka 2021/2022 hadi shilingi trilioni 1.2 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la 324.4%.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni mafanikio ya kusambaza vitendea kazi kwa maafisa wetu ambao ni maafisa ugani ikiwa ni pamoja na magari, pikipiki, vipima udongo, na mengineyo mengi. Kwenye eneo hili naomba niende kwenye namna ya kuwashauri Maafisa Ugani wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Ugani wetu hawa tunaamini wamepewa vitendea kazi ili wakafanye kazi, lakini nitashauri kwenye maeneo kadhaa. Naomba sasa kwa namna walivyopatiwa usafiri huu, waende vijijini na mashambani wakawasajili wakulima kuliko kukaa madukani kusubiri kuuzia pembejeo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine wakatoe elimu ya kilimo chenye tija. Eneo lingine waende wakapime afya ya udongo ili waweze kuwashauri wakulima ni zao gani linafaa kwa ardhi hiyo? Eneo lingine waende wakatoe elimu ya mazao kwa namna ya upandaji wenye tija. Pia, waende wakatoe elimu ya uwekaji mbolea kwa wakati sahihi kuliko ilivyo sasa hivi wakulima wanahangaika, kila mkulima anafanya anavyojua yeye, anahangaika ili mradi tu apate mavuno aweze kupata mazao ambayo yataweza kukidhi kibiashara pamoja na familia yake yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini ya kwamba kama Maafisa Ugani wetu wataenda vijijini, wataenda mashambani na wakitoa elimu hii ninaamini sasa wakulima wetu wataweza kupata mazao mengi, mazao yenye tija ili nao waweze kufikia haja ya mioyo yao. Siyo hivyo tu, naomba nishauri ya kwamba kwa sababu Maafisa Ugani wetu tumewapatia vitendea kazi

kama pikipiki, naomba basi watengewe bajeti angalau wawe wanapatiwa mafuta hata kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Maafisa Ugani hawa wanavyo vitendea kazi vyao, lakini wana-*park* majumbani na wengine wanazunguka navyo, kama bodaboda kwa sababu wanatafuta hela ya kuweka mafuta, hii siyo sawa. Tunaomba tuangalie Maafisa Ugani wetu ili wakaweze kufanya kazi zao kama tulivyokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu lingine nitaenda kwenye suala la mbegu bora. Nitaongelea suala la mbegu za alizeti. Tunaona kuna mbegu za alizeti tofauti tofauti zipo, lakini wakulima wengi hasa wa maeneo ya Kiteto wanapendekeza mbegu ya *record* ambayo inatokea Makutopora ni bora zaidi ukilinganisha na mbegu ambazo zinaitwa *Sun Bloom* na K-Kwanza. Hizi tunaomba zifanyiwe utafiti zaidi kwani wakulima wengi wamelima kwa kutumia mbegu hizi lakini hakuna walichopata ukilinganisha na *record* ambayo inapatikana Makutopora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye eneo lingine ambalo ni mafanikio namba nane ya kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kutoka tani 363,599 mwaka 2021/2022 hadi tani 848,884 mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa niwapongeze Wizara hii ya Kilimo kwa kuwa Mkoani kwetu Ruvuma kulikuwa kuna changamoto sana ya namna ya kuifikia hii mbolea kutoka kwa wakulima walioko mashambani na vijijini kwetu, lakini kwa sasa hivi mawakala wamesogea mpaka kule vijijini, mbolea inapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Wizara hii kwa namna wanavyofanya kazi kwa ushirikiano wao mkubwa; Mawaziri pamoja na Makatibu Wakuu wao pamoja na wasaidizi wao wote. Yote kwa yote, nawapongeza niwatakie kila la heri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Rahhi, jiandae Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti ya kilimo. Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, Naibu Waziri na watendaji wote wa wizara hii. Kama kuna kipindi ambacho kilimo kinavutia, ndiyo kipindi hiki cha sasa hivi. Kilimo kilikuwa kimebaki kwa wazee, lakini kupitia *BBT* na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika kilimo, sasa kilimo kinavutia vijana, kinavutia wawekezaji, wasomi wako huko na matajiri. Kwa hiyo, hongereni sana watendaji wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba tu mchango wangu moja kwa moja niuelekeze kwenye zile changamoto chache zilizobaki kwa wakulima. Wakulima wadogo ambao ni 90% ya wakulima wote wa nchi hii na ndiyo wazalishaji wakubwa wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima kama mkulima vitu ambavyo viko karibu naye ni pembejeo za kilimo na masoko ya mazao yake. Kwenye pembejeo ya kilimo kwa maana ya mbegu, mbolea na viuatilifu, changamoto ni upatikanaji wa pembejeo, bei pamoja na ubora, kwa sababu wakulima bado sehemu nyingine wanakutana na pembejeo feki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upatikanaji wa pembejeo za kilimo, tunaishukuru Serikali, kwa kweli wameliona hilo, wameweka ruzuku kwenye pembejeo za kilimo. Tulianza na mbolea muda uliopita na mbolea tumefanya vizuri. Msimu uliopita ruzuku imewekwa kwenye mbegu, sasa hili jambo bado limeleta changamoto kwa wakulima kwa sababu upatikanaji ndiyo umezidi kuwa mgumu kwa sababu ya *bureaucracy* ya makampuni fulani ambayo mbegu hizi za ruzuku wanatoa kwa mawakala wachache sana pale wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utashangaa kwamba kwenye wilaya moja pembejeo za ruzuku zitapatikana kwa wakala mmoja, watakaa kwenye foleni. Mahali pengine mtandao unasumbua. Hii imeleta adha kubwa sana kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, yote makubwa ameyaweza; hili nalo analiweza. Naomba pembejeo za kilimo ziende kwa mawakala wale wa chini kabisa ambao wako karibu na wakulima. Tena zipatikane kabla ya muda wa msimu wa kilimo, lakini kwa changamoto ya bei kubwa, tunazalisha sasa hivi mbegu kwa 60%. Nami naiomba kabisa Serikali yangu sikivu, tuendelee kuongeza bajeti kwenye uzalishaji wa mbegu ili sasa tujitosheleze kwa uzalishaji wa mbegu na ziada, tuweze kuziuza nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kwenye maghala. Maghala haya kwa utaratibu wa stakabadhi wa mazao ghalani, kama kuna sehemu wakulima wamepata bei nzuri kidogo ya mazao yao, ni kupitia stakabadhi ya mazao ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni walikuwa hawajaelewa, lakini toka wameelewa Stakabadhi ya Mazao Ghalani imesaidia sana wakulima mazao yao yamepata bei nzuri, lakini wamepata taarifa za masoko. Sasa haya maghala yajengwe vijijini na kwenye kata; na kuna maghala ambayo yalishakuwepo yakarabatiwe ili sasa Stakabadhi ya Mazao Ghalani na mazao yote yaingie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona sehemu nyingine watu binafsi wana maghala yao na wananunua mazao ya wakulima kupitia Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Jambo hili ni jema liendelee kuwepo kila sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu huduma za ugani, tumeomba sana upatikane uwakala wa Maafisa Ugani. Vinginevyo uwekezaji mkubwa sana tunaoweka kwenye kilimo utakuwa hauna maana kama

tutashindwa kuboresha hali ya Maafisa Ugani; na katika kuboresha tumeomba wawe na wakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji huu mkubwa tunaoweka, kwa mfano kwenye miradi ya umwagiliaji, kama kwenye skimu hapatakuwepo Afisa Kilimo atakayeshauri kuzalisha kwa utaalamu, na atakayeangalia miundombinu ikiwepo mifuko ya ukarabaki, basi kipato pale kitakuwa kidogo na uwekezaji huu mkubwa utakuwa hauna sababu. Sasa ili Maafisa Kilimo waweze kufanya vizuri, tunaomba Serikali iharakishe upatikanaji wa Maafisa Ugani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango mwingine ni kuhusu *centre* hizi za *Agro mechanisation.* Naipongeza Serikali, wamenunua trekta za kutosha pamoja na *power tiller.* Sasa hivi ni kipindi cha kutoka kwenye kilimo cha jembe la mkono. Zilikuwepo *power tiller* ambapo watu walikopa kipindi kile cha Kilimo Kwanza, kwa sababu teknolojia hii ni mpya, zimekufa, hawajui pakupata *spare parts,* na hawana taaluma za kuendesha. Kwa hiyo, tutakavyokuwa na hizi *Agro mechanisation centre* angalau kubwa kwa kila wilaya, na kule kwenye kata, tuendelee kuboresha *world resource centre* sehemu ambazo watu watapata taaluma kwa urahisi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, hii iende ili kilimo chetu kiendelee kuwa bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine, naipongeza Serikali kwa kuanzisha Benki ya Ushirika, hongera sana. Hii benki inaweza ikawa mkombozi kwa wakulima. Hii benki sasa ipewe fedha. Kama inapewa fedha na Benki Kuu, ikopeshe wakulima kwa sababu wakulima ni kikundi ambacho walikuwa hawakopesheki.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Rahhi, nawe ni mkulima mzuri.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ushauri wako utapokelewa vizuri. Mheshimiwa Kunambi, halafu jiandae Mheshimiwa Kawawa na Mheshimiwa Festo.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa dhati kabisa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nina kila sababu ya kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu kuu moja ya utashi wake wa kisiasa kuwekeza fedha nyingi kwenye sekta hii muhimu ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona ongezeko la bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 bajeti ilikuwa shilingi bilioni 294, lakini kwa mwaka wa fedha 2024/2025 bajeti imekua na kufika shilingi trilioni 1.248. Jambo hili ni kubwa na ndiyo maana nikasema nampongeza Mheshimiwa Rais anavyowekeza fedha nyingi kwenye sekta ya kilimo, sekta pekee inayotoa ajira kwa Watanzania walio wengi. Maana yake ni nini? Anawagusa kwa asilimia kubwa Watanzania, watu wazima, vijana na itoshe tu kusema sasa hivi wamesema wengine, vijana wamehamasika sana na kilimo kwa sababu wameona kina tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Mheshimiwa Waziri, Bashe na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Hapa nirejee mafundisho ya hadithi muhimu ya Mtume Muhamad, anasema haya kwa Waislam, *"Hubra twani minal iman"* maana yake nini? Anasisitiza habari ya uzalendo. Anasema, "Kuipenda nchi yako ni sehemu ya Imani."

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika Mheshimiwa Bashe ni mzalendo na anafuata mawaidha ya Mtume Muhamad. Kwa hilo tu, itoshe kusema Mungu atambariki. Nasi vijana, wadogo zake tunamuunga mkono kwa kuwa tumeona ana maono na

hatutamwangusha. Tunajua nia yake ni njema na uwezo wake tunaujua. Apige kazi, sisi tupo tutamuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi nijielekeze kwenye eneo la kilimo cha umwagiliaji. Kama kuna mambo ambayo Taifa letu na Mheshimiwa Bashe utaweka alama na unaenda kutengeneza na Mheshimiwa Rais anakwenda kutengeneza historia katika Taifa letu, kwa muda mrefu sana Watanzania tunasema tunazalisha, lakini bado kilimo chetu tunatumia kilimo cha kutegemea mvua ambacho siyo kilimo cha uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona fedha nyingi zinakwenda kuwekezwa kwenye kilimo cha umwagiliaji, mathalani, pale Mlimba nimeona utashi wa Serikali kuwekeza kwenye umwagiliaji katika Bonde la Mto Kilombero, hekta takribani 53,000 usanifu unaambiwa umekamilika, lakini katika hili nadhani tumechelewa na siyo Mheshimiwa bash, yeye ameikuta Wizara katikati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme tu kwamba kama kuna eneo ambalo linakwenda kulisha Taifa letu, ni Mkoa wa Morogoro. Labda nitoe mfano pale Mlimba sisi tunazalisha mchele kwa mwaka tani 400,000; na nchi nzima sasa hivi mchele unazalishwa *metric tone* milioni 3.046. Maana yake 400,000 zinatoka Mlimba kwa kilimo cha kutegemea mvua. Hatuna umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uwekezaji wa kilimo cha umwagiliaji Mlimba, maana yake nini? Tutakwenda kuleta tija kubwa kwenye zao hili la nini? La mchele. Labda niseme tu, duniani kote, katika idadi ya watu duniani takribani bilioni nane, bilioni 3.5 wanakula mchele na chakula cha kwanza duniani kwa kuliwa watu walio wengi ni ngano, na cha pili ni mchele. Tuwekeze kwenye zao la mchele. Nami nasema tu, tukiwa na *surplus* tutapata fedha za kigeni kupitia mchele.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee eneo lingine la Mradi wa *BBT*. Mwanzoni ilikuwa kama sielewielewi hivi, lakini sasa nimejifunza mengi. Kaka yangu Mheshimiwa Bashe mwanzoni

ilinipa shida kidogo lakini nikueleze kwa dhati, sasa nimeona dhamira yako ilivyo njema, lakini nikuombe sasa nataka nifanye *polishing* tu kidogo. Sasa hivi nikuombe njoo pale Mlimba nenda kwa wale vijana kule wanaofanya kazi ya kilimo. Usiishie tu kwenye maeneo haya, maeneo yote siyo tu Mlimba, uende Mbeya, uende Iringa, uende Njombe na najua mpango huo unao, lakini nataka tu uende haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, twende pale Mlimba tukapate takwimu ya vijana wanaofanya kilimo cha zao la mpunga. Tujue wako wangapi pale? Tuwaulize changamoto zao ni nini? Watakwambia, "Eneo langu mimi ni dogo, ukinipa ekari 10 nitaongeza kipato", atakwambia, "Mimi pembejeo ni changamoto", na atakwambia, "Mimi pembejeo na masoko." Sasa haya yote utayapata kule na kwa sababu wewe una *passion,* uwekezaji wako ni mdogo sana kama kumsukuma mlevi kwenye mteremko.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nihitimishe kwa kusema, zao la *Cocoa* Mheshimiwa Bashe tusaidie, Kata ya Michenga na Kata ya Mbingu wewe unafanya jitihada kubwa kuhakikisha unahamasisha zao la *Cocoa* lakini wenzako wanakata mi-*cocoa*, na hili naomba ulitolee maelezo hapa. Tuna changamoto Michenga na tuna changamoto pale Mbingu Fuatiwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamejenga ule upande wa *Cocoa* lakini zinafyekwa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi ahsante. Mheshimiwa Bashe, *cocoa* ya Tanzania inapendwa kwa sababu ni *organic*. Hongereni watu wa Morogoro kwa *Cocoa* nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kawawa, jiandaeni Mheshimiwa Festo na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdullah.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naomba niungane na wenzangu kumshukuru Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya katika eneo hili la kilimo. Nitaanza kwa eneo hili la ruzuku. Kwa upande wa ruzuku tunashukuru sana. Hili neno ruzuku ni *terminology,* lakini maana yake kubwa kwa wakulima ni kwamba Serikali anayoiongoza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inamlipia bei mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mbolea kabla ya ruzuku ilifika shilingi 130,000 lakini leo tunanunua mfuko shilingi 53,000. Tumelipiwa karibu shilingi 77 Serikali imelipia wananchi. Maana yake ni nini? Tunapozungumza uchumi umekua, basi rasilimali fedha tunazozipata za ukuaji wa uchumi, Mheshimiwa Rais Samia aliridhia zigawanywe kwa wananchi wa kawaida kuwalipia mbolea kwenye mfumo huu wa ruzuku. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunamshukuru sana kwa kufungua masoko. Alipokuwa anasema anaifungua nchi, vilevile alikuwa anafungua masoko ya kilimo. Leo hii ametufungulia masoko ya kilimo. Kwa ajili ya muda, nitatolea mfano moja tu, zao la mbaazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaazi sisi kwetu kule ilikuwa ni mboga, ilikuwa ilifikia mpaka kuuzwa shilingi 100 kwa kilo moja. Kilo 130, lile gunia kubwa lile lumbesa au sisi kwetu tunaliita mbandanga lenye kilo 130 lilikuwa linauzwa shilingi 13,000 ambayo hata bati moja ulikuwa hupati, lakini leo hii gunia hilo linauzwa mpaka shilingi 222,000. Una uwezo wa kununua bati 10. Kilo moja, shilingi 1,710 tuliuza mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao hili la mbaazi tunaposema kwamba limefanya vizuri, na Wizara ya Kilimo mmelisimamia vizuri, ndipo tunapomsifia Mheshimiwa Bashe amefanya vizuri. Hatumsifii, kwa sababu leo kuna mahali nimesikia kwamba wanasema Wabunge kazi yao kumsifia tu Mheshimiwa Bashe kwenye hotuba hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie, hatumsifii Mheshimiwa Bashe kwa sababu ya uzuri wa suti yake aliyoivaa, wala hatumsifii Mheshimiwa Bashe kwa sababu ya urefu wake au u-*handsome* wake, tunamsifia kwa sababu ya uwezo wake alionao anaosimamia sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo katika sekta hii, eneo hili moja la mbaazi sisi tulikuwa tunauza. Mwaka 2022 tulizalisha tani 3,000 tukauza shilingi 2,536,000,000 lakini mwaka 2023 tukazalisha tani 4,000 tukauza shilingi 9,267,000,000; hizi zilikuwa *take home* walipata wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024 tuliuza tani 8,000 kwa shilingi 15,345,000,000. Kwa hiyo, maana yake ni nini? Mmeisimamia sekta hii vizuri sana na mmeisimamia Wizara hii vizuri sana katika eneo hili la mbaazi katika huu Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie wenzangu wenye wasiwasi na huu Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, mfumo huu umefanya kazi vizuri sana; na kupanda kwa uzalishaji na bei kwa wakulima wetu kule Namtumbo kumetokana na huu Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na hasa pia mfumo mliouweka wa *TMX*. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wizara nzima na taasisi zenu mnazozisimamia katika eneo letu hili la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye eneo la umwagiliaji kutokana na muda. Sisi Namtumbo tuna hekta 17,322 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini tunachoweza sasa hivi, kulima ni hekta 1,680 na katika maeneo haya mengi hayana mfumo sahihi au ni kama tumejengewa mfumo wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Waziri, nitaomba kupitia Wizara yako mtusaidie, tuna mradi pale wa kienyeji katika Mto Nahange Mtakuja, ambao una hekta 300, lakini hauna mifumo na miundombinu ya umwagiliaji maji. Tuna Mwangaza Limamu hekta 250.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa ahsante.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sana mtusaidie ili tuweze kufanya katika eneo hili la umwagiliaji, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, Mheshimiwa Hamida na Mheshimiwa Ally Anyingulile Jumbe jiandaeni.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Jambo la kwanza niunge mkono hoja iliyoko Mezani ya Mheshimiwa Bashe kaka yangu, lakini jambo la pili nampongeza kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kuhakikisha kwamba sekta ya kilimo inasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache. Jambo la kwanza nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Makete kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu amekuwa na utaratibu wa takribani miaka mitatu kutupatia mbegu ya ngano, na kwa kweli kwa niaba ya wananchi mimi kama mwakilishi wao nakuja kumshukuru sana lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu mbegu ile inatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye soko mbegu ya ngano inauzwa zaidi ya shilingi 180,000 mpaka shilingi 200,000 kwa mfuko, lakini sisi mnatupatia bure. Wananchi wa Wilaya ya Makete wanapongeza sana. Pia hapo naomba tu angalizo kwamba ngano tumelima, lakini tumevuna, na kuna malipo baadhi bado hayajalipwa. Kwa hiyo, tunatamani watu wetu wa *ASA* waweze kutusaidia kutulipa mapema ili wakulima waingie tena kwenye msimu mwingine na iweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; kwanza, tumefanya kitu kikubwa kwenye kilimo kwa maana ya kupandisha bajeti yake kutoka shilingi milioni 200 hadi shilingi trilioni 1.2 sasa ambazo tunakwenda.

Pili, tu-*appreciate* jitihada ambazo Serikali inafanya katika suala la ruzuku na maeneo mengine kuhakikisha kwamba kilimo kinakua, hususan Mheshimiwa Waziri amekuwa ni *champion* kuhamasisha umwagiliaji kwenye nchi yetu, kwamba bila umwagiliaji kilimo hakiwezi kwenda mbele. Tumeona *transformation* kwenye hilo, kwani mmeweka fedha nyingi kwenye umwagiliaji. Mheshimiwa Waziri *I really appreciate* kwa niaba ya vijana wa Taifa hili, na kwa niaba ya wakulima wote wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo machache ninatamani kumshauri Mheshimiwa Bashe. La kwanza, ni kweli mkulima tunampa ruzuku ya mbegu, lakini tumemsaidia mkulima anapima udongo. Ukiangalia kwa sisi Makete udongo tulikuwa tukienda kupima Uyole ni zaidi ya shilingi 140,000 lakini tunapima kwa *free* kwa sababu Maafisa Ugani wamewezeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, ana ajenda ya *BBT,* ameimarisha Benki ya Ushirika, sasa tunaiona, na ni kitu kizuri kama Taifa, lakini mkulima ameenda kwenye *single digit* kwenye suala la mikopo. Mkulima huyu ukisoma kwenye *page* ya 189 kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema, "Hatuwezi kuondoa umasikini kama hatuwezi kuwaondoa wakulima wadogo kwenye umasikini." Hoja yake ni kubwa na ni nzito kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama haya yote tumeyafanya ambayo nimeyataja, yeye kama Waziri anamsaidia vipi mkulima huyu asiibiwe mazao yake? Leo ninapozungumza, mkulima wa Makete analima kiazi na ngano, hadi afike sokoni na hadi apambane na soko, kwa kweli ameumia kwa kiwango kikubwa sana. *So, with all the efforts* ambazo tumeziweka kwenye mkulima ku-*support* ruzuku na kufanya nini, Mheshimiwa Waziri

lazima aje na jibu la kumsaidia mkulima huyu ili ile nguvu aliyoiwekeza isiwe *for nothing,* iwe ni yenye tija kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunakuwa na mkulima kutoka Taifa lingine, anakuwa na *access* ya kwenda kufika Makete nyumbani kwangu kwa mkulima akapata zao, akanunua kitu bila kupitia kwa mfumo halali ambao unatakiwa. Nashauri kama Wizara hilo mtengeneze. Hatutamani tuone wanunuzi wanatoka moja kwa moja nje kuja kum-*access* mkulima, wakati sisi Tanzania hatuwezi kuingia kwenye hizo nchi kwenda kumkuta mkulima na tukanunua mazao. Sasa Mheshimiwa Waziri madalali hawa wanawaumiza wakulima kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza lumbesa *is not a case* kwa kiwango kikubwa, lakini tunachotamani kukiona ni Waziri kutengeneza mazingira kwamba, *effort* zote walizoziweka za mikopo, ruzuku, mbegu ziende kuwa na tija kwa mkulima; akishalima, basi aweze kunufaika na tuone mkulima huyu anatoka kwenye umaskini kama alivyosema na kama ambavyo Serikali imekusudia, naomba sana kwa niaba ya wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamezungumza kuhusu kitunguu na soko holela. Tunatamani soko holela liondoke kwenye nchi yetu, tutengeneze mfumo ambao unaweza kudhibiti madalali ambao wamekuwa wakiwasumbua wakulima, wameweza kudhibiti kwamba Mataifa mengine yaende kuwa na *access* na mkulima moja kwa moja kwa kununua mazao na hatimaye kuondokana na soko holela ambalo linawaumiza wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, jitihada hizi ziwe ni jitihada zenye tija kwa ajili ya kumwinua mkulima maskini kama ambavyo amesema amenuia, na kweli Serikali imefanya kazi kubwa na hii ndiyo inatufanya sisi pia Wanamakete tukaichagua Serikali mwaka 2020 kwa kazi kubwa ambayo umeifanya, kwa sababu asilimia zaidi ya 90 wananchi wa Makete ni wakulima na *we really appreciate* kwenye *effort* ambazo amezifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo natamani kushauri ni kwenye suala la Bodi za Mazao. Mheshimiwa Waziri unafahamu na ninadhani unafanya *study* nyingi, unazisoma. Ukisoma *study* za India kwenye *rubber, coffee* na *tea,* ukiangalia Bodi za Mazao zinavyofanya kazi, angalia Ivory Coast, angalia Ghana, wenzetu wameweka u-*serious* mkubwa sana kwenye hizi Bodi za Mazao ili kuhakikisha kwanza, wana-*monitor* kwenye bei ili kusiwepo na bei holela. Pili, kuhakikisha kwamba, kunakuwepo na tathmini ya zao lenyewe katika ukuaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunatamani kama Wizara ya Kilimo, imarisheni angalau hata bodi nne au tano, yaani iwe ndiyo *foundation* ambayo Waziri ameitengeneza yeye kwenye nchi hii, kwamba bodi hii inatupa matokeo chanya kwa ajili ya mazao fulani, kuliko kipindi hiki unakuta pia kunakuwepo na changamoto ya bodi nyingine ambazo aidha, zimechelewa kuteuliwa au kuna…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kengele ya kwanza.

**NAIBU SPIKA:** *No,* ni dakika tano tu.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hamida Mohamed, jiandae Mheshimiwa Ally Jumbe na Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Bashe, Naibu wake na timu yake ya Wizara ya Kilimo kwa kutuletea bajeti ambayo kwa kweli inakwenda kutuletea mapinduzi makubwa katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mwanamapinduzi wa kweli katika kuhakikisha kwamba, anakwenda kuimarisha sekta ya kilimo kwa kwenda kuleta matokeo chanya katika nchi yetu. Tuendelee kumtakia heri na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza ndugu zetu wa *TARI* kwa kazi nzuri wanayotufanyia ya kuhakikisha kwamba, wanaendelea kufanya tafiti, lakini tuwashukuru wale wanaoendelea kutuzalishia mbegu ambazo zinakwenda kutuletea matokeo chanya ya uzalishaji uliokuwa bora na hatimaye kuleta ustawi wa wananchi wetu kwa maana ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Bashe nakushukuru sana, ulitusimamia kwa sababu nilikueleza changamoto kubwa ya kilimo cha minazi ambayo ilipatwa na ugonjwa na kuendelea kuathirika, na sasa umetuletea mbegu mpya ya minazi na tumepokea, wakulima wa Lindi Mjini wamepata miche ya minazi bure na tunaendeleza zao la minazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana pamoja na kwamba, bado mgao utaendelea awamu ya pili na ya tatu, tunataka kuondoa mashamba pori yote ili tuhakikishe kwamba tunaiendeleza minazi katika eneo letu la Lindi Mjini. Kwa asilimia kubwa eneo lile tunalima sana minazi, kwa hiyo, kiwango cha ulimaji wa mikorosho ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri wetu kwa kuhakikisha kwamba changamoto nyingi za wakulima wa korosho amesimamia na zimepungua. Wakulima wa korosho kila siku tukikutana kwenye vikao mbalimbali wanatamani arudi tena na awe Waziri wa Kilimo, auendelee kusimamia sekta ya kilimo kuhakikisha kwamba tunaendelea kukuza sekta ya kilimo. Kwa hakika ameitendea haki Wizara hii ya Kilimo. Tunaendelea kumwombea kila la heri, Mungu amrudishe tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana *SWISS Aid,* wametupa mafunzo mbalimbali pale Lindi. Pia tunashukuru kwamba, tumefungua benki ya kuhifadhi mbegu za asili na kuendeleza kilimo cha asili ambacho tumekirithi. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri, tuhakikishe kwamba tunawapa *support* kubwa kwa sababu kazi wanayoifanya ni nzuri, inatuletea matokeo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, nimempelekea mwekezaji katika Wizara yake. Mwekezaji huyo anakuja kuwekeza Lindi katika kilimo cha *agrihood*. Sisi wananchi wa Lindi tunaomba Waziri ampokee na ampe *support* kubwa kwa sababu anakuja kubadilisha maisha ya wananchi wa Lindi kuelekea kukuza uchumi katika eneo letu la Lindi Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kumtakia kila la heri, Mheshimiwa Waziri. Pia naomba Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba wanatoa fedha kama ambavyo bajeti inasema katika Wizara hii ya Kilimo kwa sababu kuna mambo mengi mazuri ambayo tunayategemea kwamba yataleta mabadiliko makubwa ya kimaendeleo katika nchi yetu. Kubwa ni kuhakikisha kwamba, fedha zilizotengwa zinakwenda kwa wakati ili Mheshimiwa Waziri Bashe pamoja na wenzake waweze kutekeleza mipango ambayo wametuletea katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Ally Jumbe, Mheshimiwa Msongozi na Mheshimiwa Kapinga Benaya wajiandae.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Nami niendelee kuwashukuru na kuwapongeza sana viongozi wetu ambao wanatuongoza kwenye sekta hii, Waziri Mheshimiwa Bashe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote wanaoshiriki. Kwa kweli tunawapongeza sana, lakini tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu ameweka kipaumbele kwenye kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nizungumze kidogo kwenye maneno yako uliyoyazungumza wakati amemaliza Mheshimiwa Kunambi juu ya zao la kokoa. Ni kweli zao la kokoa na hasa kokoa ya Kyela ni zao ambalo linapendwa sana duniani na ni zao ambalo ni *organic* na kwa Kyela unaambiwa ile ndiyo kokoa bora duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumefikia mahali pazuri, tunaenda vizuri, lakini bado nina wasiwasi sana. Wasiwasi wangu ni juu ya uendelezaji wa zao hili katika kuhakikisha haya mazao yetu yanakuwa endelevu na hasa kwa jambo la *quality* na *quantity* kwa sababu maeneo yetu ni madogo, lakini pamoja na kwamba maeneo yetu ni madogo, bado hakuna mkakati maalum wa kuliendeleza hili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara na Serikali ianzishe mkakati maalum wa kuendeleza zao hili pale Kyela. Naishauri Serikali, tuko na vijana wazuri sana pale Kyela ambao wamesoma, wanaelewa lile zao toka wako watoto mpaka sasa na wana uwezo wa kuisaidia Serikali kuhakikisha *Extension Officers* wanafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo nyuma kabla ya kuja Stakabadhi Ghalani, zao letu lilikuwa linaendeshwa na makampuni. Haya makampuni yaliweza kusaidia sana kuleta wataalam wazuri ambao walisaidia sana uendelevu wa zao hili, lakini bado tuna tatizo kwa sababu imeshatokea sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili zao linakimbiliwa na imekuwa ni biashara. Uvundikaji wa zao hili kwenye *quality,* nataka niseme tutafika wakati tutapoteza hii sifa tuliyonayo. Naomba sana tulisimamie hili, nami najua Serikali ni sikivu na tuko na Mawaziri ambao ni wasikivu, tutafanya vizuri katika hili, sina wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, maeneo yetu ni madogo sana Tanzania, pamoja na kwamba yapo maeneo ambayo ni makubwa, lakini maeneo ambayo yanaweza yakatoa zao la mpunga ambalo ni bora ni Kyela. Kyela tuna maeneo machache na ni eneo dogo. Pamoja na kwamba, ni eneo dogo

tumesema hapa sasa hivi tunachokiangalia ni kuzalisha kwenye eneo dogo mazao mengi, na ili ufikie hapo ni lazima tuingie kwenye *irrigation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri atakapomaliza ile skimu yangu ya bilioni 21 ya Makware ambayo Serikali imewekeza fedha nyingi, naipongeza na nampongeza Mheshimiwa Rais. Naomba sana, hebu tuziangalie skimu nyingine ambazo zipo. Kwa mfano, tuna Skimu ya Ngana, kuna Skimu ya Kingiri, yaani hayo ni mabonde ambayo yanafaa kumwagilia. Kuna Ikumbilo, Mwaigoga, Mabunga, Ikama, Kabanga, Katumbasongwe, Tenende na Mwambuzye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, tukiweka skimu kwenye maeneo haya, tutajuta ni kwa nini hatukufanya mapema. Naipongeza Serikali na ninawapongeza viongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Msongozi na Mheshimiwa Kapinga ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa. Leo tarehe 22 Mei, 2025 katika Wizara hii ya Kilimo naomba nami niwe miongoni mwa wachangiaji kwenye bajeti hii, ambayo kimsingi inagharimu pesa za Kitanzania, kwa makadirio yake ni shilingi trilioni 1.2 na ushee. Naomba nitumie nafasi hii kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ya kutukuka katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri mwenye dhamana kwa kazi nzuri anayoifanya, yeye pamoja na Naibu Waziri wake na *delegation* yake yote. Taasisi zote ambazo zina Wakurugenzi, kongole nyingi sana kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niseme, Mheshimiwa Bashe mimi huwa nataka nikufananishe na mtu mmoja ambaye ni kiongozi mahiri sana, mzalendo, kiongozi kijana, naye sio mwingine ni Kepteni Ibrahim Traore, Rais wa Burkina Faso. Traore ni Rais ambaye amefanya mageuzi makubwa sana katika nchi yake. Nataka nikwambie Mheshimiwa Bashe, utaenda mbali kwa sababu una uwezo mkubwa, una uwezo wa kufanya maamuzi, na huyo Naibu Waziri wako pia ninamfananisha kwamba angekuwa Naibu wako kama alivyo Rais Traore wewe ninavyokufananisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii sasa kuzungumza kwenye suala la mahindi. Mheshimiwa Bashe unafanya kazi nzuri sana, nawe umekuwa kipenzi cha wakulima, lakini naomba kwenye suala la zao la mahindi bado kila mwaka unatuwekea pesa shilingi 700 katika kitengo cha *NFRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Bashe, uzalishaji wa mahindi kila mwaka unaongezeka, gharama zinaongezeka, gharama za kulima, gharama za kupalilia, gharama za kutia mbolea, gharama za kila kitu zinaongezeka, lakini iweje ni mfululizo wa miaka mitatu sasa bei ameweka ni shilingi 700 tu? Kila mwaka shilingi 700, kila mwaka shilingi 700! Tunaomba sasa kwa sifa hizo tunazompa, na kwa upendo wake kwa wakulima, aje alete bei nyingine. Ungeniambia leo nipendekeze bei gani? Ningekwambia lete bei ya shilingi 900 kwa wakulima wangu wa Mkoa wa Ruvuma kwa kilo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Bashe inawezekana, kwa sababu wewe una uwezo mkubwa na una mapenzi na mahaba makubwa sana kwa wakulima wetu wa mazao haya ya nafaka ambayo yanalimwa sana katika Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nafahamu Mheshimiwa Bashe ni mbunifu sana amefanya vitu vingi, lakini naangalia kwenye suala la majanga na mabadiliko ya tabianchi wamejipangaje Wizara kwa ajili ya kuweka mkakati mzuri dhidi ya suala la kumkomboa mkulima pindi inapotokea majanga? Kwa mfano, mwaka huu, chupuchupu tukose mazao. Tumepata

mazao kidogo kutokana na hali ya mabadiliko ya tabianchi, mvua zimenyesha kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati fulani ilitokea jua linawaka sana baadhi ya mashamba yamekauka, je, mmetoa elimu kwa wakulima ili waweze kutambua umuhimu wa bima katika kilimo chao ili waweze kukata bima? Naomba sasa Wizara yako iende na mkakati wa kwamba, wakulima waende wakapate elimu ili waweze kupata bima kwa ajili ya mazao yao, ili pindi inapotokea majanga, basi wasijikute wanyonge, waweze kupata fidia kupitia bima ya mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la Hazina. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nakuomba sana, peleka pesa kama mvua kwenye Wizara ya Kilimo ili miujiza hii tuendelee kuitunza; miujiza hii ambayo inaendelea kutokea katika sekta ya kilimo. Ni sekta muhimu sana na kwa sababu tuna malengo ya kulisha dunia hii, bila kupeleka fedha hakuna muujiza wowote utakaotokea. Peleka fedha Mheshimiwa Bashe a-*relax,* afanye kazi vizuri. Ongeza mazao katika nchi yetu na tupeleke mazao mpaka nje ya nchi huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la kiwanda. Tumekuwa wazalishaji katika Mkoa wa Ruvuma zaidi ya miongo mitano, tunashika nafasi ya kwanza katika uzalishaji wa mazao ya nafaka. Kwa hiyo, tunapofanya vizuri namna hiyo, tunastahili kupata zawadi ya kujengewa kiwanda cha mbolea pale, kwa sababu sisi ndio wazalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Mheshimiwa Bashe hakuna anachokishindwa, tena ananikonyeza hapa anachekelea kabisa, inawezekana Mheshimiwa Bashe. Tuwekee kiwanda cha mbolea pale ili sisi kazi yetu iwe ni kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo, inawezekana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni suala la kilimo mseto.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo mesto…, namalizia wewe ni rafiki yangu sana. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo mseto…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msongozi tunakwenda kwa *time,* ukichukua *time* na leo mko wengi sana humu ndani na wote ni wakulima, na kila mtu anataka kuchangia, nikuombe tu ukae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga, jiandae Mheshimiwa Asenga na Mheshimiwa Samweli Hhayuma.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kuunga mkono hoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa mpango huu wa ruzuku. Hapa kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwani amekuwa mshauri mzuri wa Rais kwa kuendelea kumshauri vizuri mpango huu wa ruzuku na sasa ni miaka mitatu mfululizo imeendelea kutolewa ruzuku ya mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mbinga bila mbolea hatuvuni. Kwa maana hiyo, bei ya mbolea ilipokuwa juu tulikuwa tuna mashaka sana ya namna ya kilimo chetu, lakini nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, umekuwa na mikakati mizuri na ushauri mzuri kwa Mheshimiwa Rais, juu ya mbolea hizi za ruzuku na sasa

mbolea inapatikana vizuri Mbinga. Wananchi wa Mbinga wanapata mbolea, wanalima na wanavuna vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale katikati kidogo tulipata shida ya mbolea, lakini nashukuru kupitia kiwanda cha ndani ambao ulikuwa mkakati wa Mheshimiwa Waziri wa kufanya Tanzania tuwe na kiwanda cha ndani cha mbolea. Tunacho kiwanda hiki hapa cha *ITRACOM,* kina mbolea zile za otesha, pandisha, za aina karibu tatu, nne hivi; zilitusaidia sana zile mbolea pale ambapo mbolea nyingine zile za chumvichumvi zilipoonekana kupungua, tuliziweka zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, shida iliyopo ni uelewa wa watu kwa sababu mbolea ni zile zile. Sifa ya hii mbolea, tunaambiwa, pamoja na kunenepesha mmea, lakini inaenda pia mpaka kwenye nini? Kwenye udongo. Kwa hiyo, elimu ikitolewa kwa wananchi, huko watakuwa wanunuzi wazuri wa mbolea hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaambiwa sasa hivi hiki kiwanda kina uwezo mkubwa, kina uwezo wa kuzalisha hadi tani 600,000 na kina uwezo mkubwa zaidi ya tani 600,000 na sisi matumizi yetu sasa hivi ndio yamefika 800,000 mpaka 900,000 hapo. Kwa hiyo, kumbe tuna uwezo mkubwa. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, amefanya kazi nzuri na leo hii wananchi wa Mbinga wanakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimeambiwa hapa kuna madeni kwenye hiki kiwanda, sasa naomba kilipe. Tunajua taasisi nyingi hapo katikati zilipata shida. Zilianza vizuri kwa nguvu nzuri lakini mwisho wa siku zikadidimia kwa sababu ya madeni. Sasa hivi hiki kiwanda kinadai zaidi ya bilioni 11. Kwa kweli kilipeni kiende kufanya kazi nzuri, wananchi wetu wasipate shida tena ya mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ambalo nampongeza Mheshimiwa Waziri, ni suala la ujenzi wa maghala. Mwaka 2024 Mheshimiwa Waziri alifanya ziara Wilayani Mbinga, akakuta ukusanyaji mkubwa wa mazao, na mazao yametapakaa karibu

kila kona. Alituahidi ataenda kujenga maghala. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nimepata taarifa zaidi ya shilingi milioni 109 zimeshatolewa, eneo limenunuliwa na tayari maandalizi yako vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri aje atuambie, ni lini anaenda kujenga yale maghala? Wananchi wale wangependa mwaka huu 2025 au mwakani 2026 waanze kutumia yale maghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna Mheshimiwa Waziri alivyosema, najua atayajenga mapema iwezekanavyo, ikiwemo pia na wale wananchi wa kiwanda kile cha kukoboa kahawa na wenyewe walikuja wakamwona, najua amewapa ahadi nzuri kwamba ujenzi wa maghala ya kahawa utaenda sambamba na ujenzi ule wa maghala ya mahindi. Kwa hiyo, tunamshukuru na tunaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita, ikitamka inatekeleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024 huo huo Mheshimiwa Waziri alituma timu pale Jimboni kupokea matatizo na changamoto za wakulima wa kahawa. Walikaa pale zaidi ya mwezi mmoja wakaja wakampatia andiko Mheshimiwa Waziri na akaitisha kikao cha wadau wa kahawa. Kwenye kikao kile Waziri alitoa maelekezo kuwaambia wadau wa kahawa wakae wajipange kisaikolojia. Anaenda kufanya *reform* kubwa ya kahawa ya namna ya mfumo wenyewe wa kahawa wa mauzo na mambo mengine yote yanayohusiana na kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, amefanya vizuri sana kwenye korosho na amefanya vizuri sana kwenye kahawa huko upande wa robusta, wakulima sasa hivi hawana kelele. Mheshimiwa Waziri alipofanya ziara pale Jimboni kuna maelekezo pia alitoa na hata hapa wakati anawasilisha bajeti yake kuna maelekezo alitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, yuko mtu mmoja kule sasa hivi anapita na uongo mdomoni, anazurura pale Jimboni anapita na uongo mdomoni anasema uongo, anatamka maneno kwamba

umeyasema wewe. Maneno umeyatoa wewe kama Serikali kurekebisha mfumo wa malipo ya kahawa, kurekebisha mfumo wa zao la kahawa na watu namna gani wanaenda kukopa mbolea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga, ahsante kwa mchango mzuri, mengine mwandikie Mheshimiwa Waziri.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, tolea ufafanuzi hilo. Ni nini mlichokifanya? Nini ulichoelekeza; na nini kinachofanyika pale Mbinga Vijijini? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wageni waliokuwepo Bungeni jioni hii ni Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Mgeni wa Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Ndugu Juma Jota, mtoto wake kutoka Bukombe Mkoa wa Geita; karibu. *(Makofi)*

Tuna mgeni mwingine alishatambulishwa asubuhi, lakini kwa umuhimu na mapenzi yake kwa Taifa Ndugu Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya *CRDB.* Huyu ni mdau mkubwa sana wa kilimo na maendeleo kwenye Taifa letu. Nimekupa heshima kukutambulisha mara ya pili. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Asenga, wajiandae Mheshimiwa Samweli na Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, na ni bahati iliyo njema kupata hizi dakika tano za kuchangia Wizara nyeti ya Kilimo na huwezi kuzungumza kilimo bila kuzungumza Mkoa wa Morogoro. Mheshimiwa Naibu Spika umefika kwetu, umefika kwenye kiwanda cha sukari na umejionea sisi tulivyokuwa wakulima wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yote yaliyosemwa na Wizara hapa yapo katika namna mbili; kusaidia nchi yetu

kujitegemea kwa chakula ambapo sasa hivi tunajitegemea kwa 130% na pili tuuze mazao ya mwisho nje ya nchi yetu tuweze kupata fedha za kigeni. Mimi ni Mswahili, na Waswahili wanasema, njia rahisi ya kuleta umaskini ni kuuza malighafi badala ya kuuza ile *final product. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza kwa namna mbili; kwa furaha na kupendezwa kwa maana Kiswahili ni chata na tamwa, na pia nitazungumza kwa chona na kibubuti (kwa masikitiko) kule mwishoni endapo muda wangu utafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa furaha nataka kusema wazi kwamba nina furaha isiyo kifani kwa viongozi wote wa hii Wizara na Wakurugenzi wote. Ningetaja taasisi zote, lakini muda hautoshi.

Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na viongozi wenzako wote na Mheshimiwa Rais amempongeza mpaka Katibu Mkuu wako kwamba alikuwa anaonekana kama kijana kijana, akipiga suti yake hivi, unaweza ukamdharau ukasema kijana wa mjini, lakini Katibu Mkuu ni mtu muhimu sana katika Wizara yenu, na ni *engine* kubwa ya Wizara. Mkurugenzi wa *COPRA,* nimeona *COPRA* imeshaanza kuwasiliana wasiliana na sisi kuhusu mpunga ili tuuze mazao kidigitali, na tunaomba zao la mpunga ikibidi baadaye liende katika mambo ya kidigitali ya Stakabadhi Ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika*, TFRA* imesajili wakulima 4,500,000 na wakulima wangu wamepewa vishikwambi, ninashukuru sana. Kiwanda kipya cha sukari Mheshimiwa Waziri amekiona tunakushukuru sana, pia tunashukuru kwa kikao chake cha *AMCOS,* tunashukuru kwa upembuzi yakinifu wa Bonde, amesema pia Mheshimiwa Kunambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Kilombero litatusaidia mabwawa manne ambayo yatasaidia ku-*control* mafuriko. Tunashukuru kwa mbolea za ruzuku na tunashukuru kwa kitalu cha mbegu *KATRIN*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri Chuo cha *KATRIN* kwa maana ya *Kilombero Agricultural Training and Research Institute* kibaki kama chuo wakati mambo mengine yanaendelea kwa sababu sisi kwenye bonde tuna mkakati mkubwa. Serikali imeshawekeza mabweni pale wanafunzi walale pale. Sasa tukibadilisha, tukifanya kikiwa ni sehemu ya kuahirisha teknolojia, itakuwa tumeondoa nafasi kubwa ambayo wenzetu waliyaona huko nyuma. Naomba katika vyuo vitano vilivyobaki uongeze na hicho cha *KATRIN* kama cha sita kibaki kama chuo.

Mheshimiwa Waziri Bashe mimi nilikuwa ninakuona wakati unasoma Hotuba hapa umesimama, unainama, umesimama; nikasema hee, sasa nikajiuliza, siku moja ukiwa haupo kwenye hii Wizara itakuwa namna gani? Mheshimiwa Bashe andika kitabu, rekodini *Youtube,* elezeni mipango na idara zote zinazowakabili. Katika dunia ya sasa hivi, tuone kuna leo na kesho katika mambo haya. Tunakuomba sana, andika vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika kuandika kitabu ni kugoma kufa hata baada ya kufariki. Namwomba Mheshimiwa Waziri jambo la kwanza tunataka kufanya semina kwa wakulima wetu, tusaidiwe; pili, yale matrekta tuletewe mgao; na ya tatu, tusaidiwe haya mabwawa haraka ili tuweze kupata mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkurugenzi wa Umwagiliaji amekuja kule kwetu mara kadhaa, tunaomba sana atusaidie katika mambo ya umwagiliaji kwa sababu kama mvua zisingechelewa mwaka huu kwenye mpunga, tungepata hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atembelee Kiwanda cha *Mang'ula Machine Tools,* kina majengo, kina hekta 200, kimekaa pale zaidi ya miaka 20, kinakufa na watu wa viwanda wameshindwa kukifufua. Naomba aweke mwekezaji pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa ufupi, naongea kwa chonda na kibubuti (sikitiko) mambo mawili. Kwanza la miwa, kwa

sababu wakulima wangu wako hapa sasa hivi wananitazama. Suala la 10% nimempatia Mheshimiwa Waziri. Nimempelekea barua kwamba juzi *AMCOS* zote 17 ziligoma kuendeleza kwenye kikao cha Kiwanda cha Ilovu kwa sababu walikatwa pesa zao 10% na hawajapewa pesa zao. Mheshimiwa Waziri, ninakuomba nitaunga mkono hoja kwa masikitiko lakini naomba ulisemee jambo hili, kwani wanaangalia *television* huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima anapouza mua anakatwa pesa. Wakati msimu unaanza, wanataka kuchukua ile 10%, anaambiwa hawezi kupewa. Ni balaa huko sasa hivi ninavyokwambia, wako kwenye *TV* wanasubiria kuona hali hii. Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana nisaidie sana chonde chonde nisaidie. Prof. Bengesi ukimtazama unaona anapenda kilimo cha mua, lakini kuna saa anaona kama mambo magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Prof. Bengesi alikuja kule wakati mua unaungua moto, tukaenda mpaka porini. Ni mtu mzuri sana na mtu anayetusaidia sana, lakini naomba majibu ya 10% hii ili mwishoni nipate nafasi ya kuweza kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema *rendement* ikiwa chini ya 10, wakulima wanapata hasara, 10% yenyewe hawapewi. Kwa hiyo, hawatafanya chochote, hawatavuna mua mpaka wapewe hii 10%. Nimesikia Mheshimiwa Venant na Mheshimiwa Prof. Muhongo hawataki kilimo cha mua. Sisi tunakitaka; Mheshimiwa Waziri leta pesa, leta ruzuku, lipa wakulima wangu waendelee kulima kilimo cha mua tuendelee kujitosheleza kwa sukari. Tunalima, sasa hivi tunavuna sukari tani 480,000 na tunataka tani 700,000. Lete mambo hayo Kilombero sisi tunataka kilimo cha mua, wao hawataki. Kwa hiyo, sisi tupatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niongelee kokoa, amesema Mheshimiwa Kunambi nami ninataka kusisitiza. Kokoa kule kwetu inanawiri. Sasa lipo eneo linasemekana na wakulima na ni watu wazima; na kama hawa wakulima wamenidanganya wamekuja mpaka hapa, nimeenda mpaka kule, wanasema wana heka zaidi ya 200 zimezuiliwa na hifadhi, wamepigwa

viboko. Naomba Mheshimiwa Waziri twende tukaone kama hawa wakulima wakweli ama sisi ni wakweli.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, ahsante.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mzigo halmashauri, tunaomba Mheshimiwa Waziri ausaidie Msitu wa Kiogosi, Hifadhi ya Shamba la Kiogosi la Halmashauri ya Ifakara alisaidie liweze kulima kokoa…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, ahsante.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Samweli, halafu Mheshimiwa Mafuwe na Mheshimiwa Nollo wajiandae

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara ya Watanzania (Wizara ya Kilimo). Nataka tu nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, kwamba wakati nachangia bajeti ya 2023/2024 niliongea maeneo mahususi ambayo yanafaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji Wilaya ya Hanang. Nilitaja eneo la Duru pale Masakta, nikataja eneo la Getasam, Endagaw, Endasiwold, Qutesh, Nyamurah ambayo ipo katikati ya Bassotughang na Mara, nikataja Bwawa la Bassotughang, nikataja maeneo ya Endasak, eneo la Balang'dalalu ambapo maji yapo karibu lakini eneo la Mogitu ambalo lina maji mengi chini, nikataja na Ziwa Bassotu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili nimesema haya maeneo kwa maana ya kukumbushia yale niliyokuwa nimeyasema. Nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri ametuma wataalamu, wametembelea maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini utaharakisha uwekezaji wa mifumo ya umwagiliaji kwenye maeneo hayo ili Wanahanang ambao kwa sasa sehemu kubwa wanategemea mvua ya Mwenyezi Mungu ili waweze kulima, waweze kutegemea umwagiliaji na waweze kulima zaidi ya mara moja kwa msimu kwa sababu ardhi ya Hanang sasa imekuwa finyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, ameanza kazi vizuri, naye na timu yake wanajitahidi na wanafanya kazi sawasawa. Yale ambayo nimewaomba wamefanya sehemu kubwa, namwomba sana aongeze kasi, Wanahanang wanamsubiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni alishawahi kuahidi yale mashamba ambayo yako kwa wawekezaji ekari 30,000 angewarejeshea wananchi. Wanahanang wanasubiri hiyo ahadi.

Mheshimiwa Waziri, pia, Wanahanang wanakusubiri uwatembelee uende ukaongee nao. Wawekezaji waliowekeza kwenye ekari zaidi ya 42,000 mara nyingi wanakuja kwako wakileta siasa nyingi. Mwaka huu mashamba yao yamelimwa na wananchi wa Hanang na wamezalisha. Peleka jicho lako ukaone jinsi Wanahanang wanavyoweza kuzalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo Shamba la Bassotu *Plantation* ambalo liko chini ya usimamizi wa halmashauri. Shamba lile likabidhi kwa halmashauri wawekeze pamoja na wananchi. Wakiwekeza pamoja na halmashauri, matunda utayaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanahanang ni wachapakazi na wanajituma. Mheshimiwa Waziri, kete wataalamu tuzalishe kadri unavyotaka ili hatimaye Wanahanang tuzalishe. Pia, yale mashamba ya wawekezaji angalia namna ambavyo wale wawekezaji wanaweza kushirikiana na halmashauri ili yale maeneo yaweze kutumika vizuri. Tembelea Hanang, Wanahanang wanakusubiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninataka niseme ni suala la kilimo cha ngano. Wakati Mheshimiwa Rais anafungua Bunge hili la Kumi na Mbili, alionyesha kwamba tunayo nakisi ya zaidi ya milioni moja. Mheshimiwa Waziri nimeangalia kwenye vitabu vyako kwamba 2022/2023 tulikuwa tumefikia tani 86,000 lakini 2023/2024 tani laki moja na zaidi, bado tuko chini sana.

Mheshimiwa Waziri, ninachoomba, ile kasi uliyokuja nayo Jimboni Hanang mwaka 2020, hebu uirudie ile ile angalau tuweze kuzalisha ngano zaidi ili wakulima wetu waweze kulisha nchi yetu badala ya kutegemea kuagiza ngano kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamsubiri Mheshimiwa Waziri Hanang. Naomba wakati anahitimisha angalau atenge muda kidogo aseme kwamba wananchi wa Hanang, wakulima wa Hanang wanamsubiri akaseme nao, wana *issue* naye kwenye suala la Stakabadhi Ghalani na wanapenda sana Stakabadhi Ghalani.

Mheshimiwa Waziri, nafahamu ulikuwa unatarajia nitasema hili, lakini nalisema kwa sababu sasa hivi ni wakati ambapo watu wanaandaa mazao. Watu ule mvuto wa fedha haujaja, nenda kaongee nao sasa. Peleka timu yako ya *COPRA*, peleka timu ya *CPB* wakawaelimishe wananchi mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ule wa fedha, kila mtu alichanganyikiwa na fedha, hakuna mtu anamsikiliza mwenzie. Twende tukaongee sasa ambapo fedha hazijawa karibu. Wanakushukuru wananchi wa Hanang…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Samweli, ahsante.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mafuwe, Mheshimiwa Nollo na Mheshimiwa Mpakate, wajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Mheshimiwa Waziri utakumbuka miaka ya nyuma kidogo nilikuwa nikichangia hapa ninakuwa mkali sana, na wewe unajua sababu ya ukali wangu wakati huo, lakini leo nachangia hapa nikiwa na furaha kwamba mambo mengi ambayo nilikuwa nikiyasema umeyawezesha. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Waziri, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kweli kwa kukupatia jukumu hili na kwa miradi mingi aliyotuletea katika Wilaya yetu ya Hai. Mheshimiwa Bashe, nakupongeza sana kwa ujenzi wa Soko la Mula. Pale Mula najua tayari mkandarasi ameshapatikana na wako kwenye hatua za kuanza ujenzi. Kwa hiyo, niwaambie wananchi wanaotumia Soko la Mula, kuweni wapole Mheshimiwa Rais ameshatupatia fedha, Soko la Mula linaenda kujengwa soko la kisasa kabisa, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Silinde. Kule Hai wanamwita Mzee wa Makeresho. Namshukuru sana Mzazi kwa kazi kubwa aliyoifanya kuhakikisha Wilaya ya Hai inapata miradi mikubwa. Leo ninavyozungumza tuna mradi wa shilingi bilioni 19 kwenye Skimu ya Mtambo; tayari Bwawa la Bolutu, Makeresho, Metromu vinafanyiwa *feasibility study;* Kiladedea A tayari wanafanya *feasibility study* ili waweze kujenga. Nawashukuru sana kwa kazi hii kubwa mliyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, sasa haya ninayokwambia ni machache sana, nami najua watu wa Nzega wanakupenda sana. Kwa hiyo, nina hakika Bunge lijalo uko hapa nami watu wa Hai wameshaniambia mimi hapa narudi, na Mungu ameshanipa kibali. Kwa hiyo, mimi na wewe Bunge linalokuja tutakutana hapa. Sasa haya yafuatayo naomba uyaweke vizuri ili tuelewane, urafiki huu tuliouanza Bunge hili la mwishoni mwishoni, hilo Bunge linalokuja tuanze vizuri tusianze vibaya kama tulivyoanza Bunge lililopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Bwawa la Mto Mbuguni pale, nilikwambia linatoa maji kuja kuhudumia Kawaya, Longoi, na Mkalama. Haya maji yakipatikana, Mheshimiwa Waziri nimeona kwenye hotuba yako umeeleza kuna changamoto. Hizi changamoto zilizopo pale, hii inaenda kutibu. Wewe unajua watu wa Hai huwa tunafanya kilimo cha biashara, nasi ndio walimu wazuri. Kwa hiyo, tupate haya maji pamoja na maji ya pale kwenye Bwawa la Kibashukeni iliyoko kwenye eneo la Lyamungo, Kilanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukipata Bwawa la Kwa Tito, hili ni Bwawa muhimu sana. Tukilipata litatusaidia. Urara pale kuna bwawa la muda mrefu, limeharibika, limetelekezwa. Hili Bwawa la Urara na lenyewe litatusaidia, lakini najua Mheshimiwa Waziri wewe mtu bingwa mmeshanunua magari. Nakuomba haya magari yako hebu yaanzie Mkoa wa Kilimanjaro na yaweke kambi pale Hai yapige kazi pale kama miezi miwili halafu ndiyo yaende.

Mheshimiwa Waziri, kule Kiyeri niliongea na wewe ukaniambia nenda kwa watu wa Kiyeri kawaahidi kwamba utawachimbia visima vya umwagiliaji. Nakuomba, magari haya yazinduliwe pale, nami ninakuandalia sherehe na ndafu nzuri, magari yaende yakazinduliwe pale Hai, baadaye ndiyo yaelekee kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine hili, Mheshimiwa Waziri unisikilize kwa utulivu kabisa. Tuna mashamba ya Ushirika, haya mashamba yapo 17. Umenisaidia, tumepunguza changamoto japo hazijaisha, lakini naomba nikushauri. Kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, kuna shida gani kama tukiamua sehemu ya ardhi kwenye mashamba yale mazuri, kwa mfano, lile Shamba la Kikafu Mrososangu pale anapokaa James kwenye makazi yake, tukachukua pale ekari mbili tu tukajenga hoteli za kitalii?

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani ekari mbili hizi hazina madhara yoyote. Tutaendelea kulima kahawa, tutaendelea kufanya shughuli nyingine ili angalau kuwe na *package* kidogo ya

kuongeza fedha. Mheshimiwa Waziri sisi kule kwetu ardhi imekwisha. Tukipata fedha inayotokana na uwekezaji kwenye hoteli za kitalii zitatusaidia kwenda kule Nzega kununua maeneo angalau na sisi tuanze kusogea huko taratibu kwa sababu, ardhi yetu imekwisha. Nakuomba sana, hili Mheshimiwa Waziri linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimezungumza na Kamishna wa *PPP,* inawezekana. Tunafanya *valuation* ya zile ekari mbili tu au hata ekari moja bila kuathiri shughuli zozote za kilimo. Mheshimiwa Waziri, nikuhakikishie, kama ukinipatia wataalamu wako nikakaa nao, nimeshazungumza na Katibu wa Maliasili amekubali jambo hili. Wilaya ya Hai ardhi imekwisha, kwa hiyo, lazima tutafute *alternative* ya kuweza kuhakikisha Wilaya yetu inapata uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine Mheshimiwa Waziri alituahidi hapa Barabara ya Kwasadala kwenda Longoi kupitia mpango ule wa kilimo kwenda kwenye Soko la Kwasadala. Kumbuka Mheshimiwa Rais ameshatutengea shilingi bilioni 11.6; kwa utaratibu wako tumeongea asubuhi, naomba sana, endelea kuliweka kwenye kumbukumbu zako.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, leo sitaki kugongewa kengele. *TARI* wapeni fedha ya kutosha. Imewekwa kwenye bajeti, ndiyo, lakini hampeleki hizi fedha. Naomba *TARI* wapewe fedha ya kutosha ili wafanye kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naounga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Nollo, Mheshimiwa Mpakate na Mheshimiwa Kamonga, wajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kuunga mkono hoja bajeti hii ambayo iko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunaamini na hata mimi bado ninaamini kwamba nchi yetu ni nchi ya ujamaa, na ujamaa halisi unaweza kuuona katika maisha ya wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama ni haki na kama ni kuitendea haki Sekta ya Kilimo, amefanya vya kutosha. Kwa hiyo, kama ukitaka kumwelezea Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, huyu ni mjamaa katika vitendo katika kuwainua wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii vilevile nimpongeze Waziri wa Kilimo, ndugu yangu Bashe. Kwanza, ni mtu mbunifu, lakini ni mtu anayejaribu. Tatizo kubwa la uongozi katika nchi yetu ni kwamba watu hawawezi kujaribu kufanya mambo na kutokuwa na maamuzi, lakini Mheshimiwa Bashe ni mtu anayejua kutumia madaraka katika kuamua. Kwa hiyo, jambo hili mimi nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona ubunifu mkubwa uliofanyika katika Wizara hii, lakini tumeona namna ambavyo Sekta ya Kilimo imekua kwa kiasi kikubwa. Tangu mwaka 2021 mpaka leo tumekuwa na miradi 780 ya umwagiliaji. Haya ni mapinduzi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja ya kwanza kwenye suala zima la mbolea na pembejeo. 60% ya wananchi wa Taifa letu ni vijana na kwa maana hiyo vijana wengi inatakiwa waingie kwenye kilimo, lakini hawawezi kuingia kwenye kilimo kwa kutumia jembe la mkono. Jembe la mkono ni *corporal punishment*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ipo haja ya kuangalia tutoke kwenye jembe la mkono, tuingie kwenye *mechanization,* hasa katika jembe la kukokotwa na ng'ombe. Mimi ninamshauri Waziri, jembe la ng'ombe sasa linauzwa shilingi 150,000, Serikali inaweza ikaweka ruzuku kule, ikaondoa kodi, tukaweza kununua hata kwa shilingi 50,000 ili wananchi wengi waweze kulima, waachane na jembe la mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuhusu uzalishaji, wenzangu wamesema kwenye bustani *(horticulture),* kilimo ambacho kinavutia vijana wengi, lakini kinatengeneza fedha kwa muda mfupi. Tunazo mashine za *pump,* zile za *man maker,* ambazo hutumii umeme, unatumia nguvu zako mkulima katika ku-*pump,* kwa sasa inauzwa shilingi 500,000; wakulima na wananchi wa vijijini wengi hawawezi kununua.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, zile *pump* za *man maker* ziondolewe kwanza kodi na vilevile kutoka shilingi 500,000 walau ziuzwe shilingi 200,000. Tukifanya hivyo, tutaweza kuajiri vijana wengi katika umwagiliaji. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo mmenunua magari kwa ajili ya kuchimba visima. Jambo hili ni kubwa, sisi bado tunaiogopa sana rasilimali ya maji.

Mheshimiwa Waziri mimi ninakushukuru sana, katika Wilaya yangu ya Bahi umeweza kunipa miradi ya umwagiliaji mikubwa. Mradi ule wa Kongogo pale Babayu, Mradi wa Kukarabati Skimu ya Umwagiliaji ya Bahi na mingine, juzi mitano nimeipata katika Bonde la Lukali pale Mtitaa na wanakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa na mkutano pale na pia, pale Mkakatika. Mheshimiwa Waziri kwa kweli, mimi nakushukuru katika suala zima la kutaka kunyanyua kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la mbolea. Mheshimiwa Waziri kwenye mbolea uzalishaji wetu wa viwanda vya ndani ni kama 158,000, lakini mahitaji ni makubwa, kama 1,500,000 sasa bado inatakiwa tuweke umadhubuti katika kuongeza uzalishaji wa mbolea. Bahati mbaya mbolea nyingi tunaitoa nje, lakini Kiwanda kama cha *INTRACOM* kimeonesha mbolea hii na wakulima wameikubali; kwanza inatumia Samadi, ambayo tunanunua kwa wafugaji, inatumia *dolomite* na *gypsum,* ni *material* ambayo yanapatikana hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Mheshimiwa Mpakate, atafuatiwa na Mheshimiwa Kamonga, na Mheshimiwa Kungu ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye hoja ya kilimo, ambayo ni uti wa mgongo wa nchi yetu. Mimi nitakuwa na *section* mbili. Kwanza, tunaishukuru Serikali na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia vitu vifuatavyo; kutoa pembejeo za mikorosho bure kwa wakulima wetu; pili, kutoa ruzuku kwenye mbolea; na tatu, kusimamia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani vizuri, pamoja na *TMX,* ambao unawafanya wakulima waneemeke kwa kupata fedha nyingi na bei nzuri kutokana na mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashauri kwenye mambo yafuatayo: Ushauri wangu wa kwanza, naomba Mheshimiwa Bashe anisikilize kwa makini sana kwa sababu, mimi ni mkulima ambaye natoka kijijini. Mfumo wa ugawaji pembejeo una kasoro kidogo, ni kwamba, hakuna uwazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamefanya vizuri, wameandikisha wakulima, kila mmoja anajua analima kiasi gani? Ila wakati wa kugawa, mkulima anaenda pale ghalani, hajui anapata kiasi gani? Hili linasababisha wakati mwingine malalamiko kuwa mengi kwamba, wamepunjwa. Kwa hiyo, naomba sana, kwa sababu, tayari tumeshawaandikisha hawa wakulima, basi ni vizuri tukabandike yale yaliyotoka kwenye *research* yetu, ili kila mmoja ajue anapata mifuko mingapi na kwa wakati gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kugawa huku, kuna kalenda ya uzalishaji wa korosho, namna ya kuhudumia. Tufuate kalenda jinsi inavyotaka, ili hizi dawa zinapokwenda zikahudumie mazao yetu vizuri. Tofauti na hivyo, unapeleka *Sulphur* wakati inahitajika dawa ya maji, kwa kweli, tunayumbisha uzalishaji wa zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwenye hili la ugawaji wa pembejeo, ni suala la kuangalia *ratio*. Sasa hivi jinsi wanavyogawa inaonekana kwamba, mfuko mmoja unahudumia mikorosho 100, kitu ambacho siyo jambo la kawaida. Kwa hiyo, naomba wakati wanagawa ile *Sulphur,* watuoneshe mgao wa kwanza utapata mifuko kadhaa na mgao wa pili utapata mifuko kadhaa, ili mkulima naye aweze kufanya *adjustment* ya namna ya kupulizia shamba lake, na kama kuna haja ya kuongeza mifuko mingine, basi aongeze ili aweze kuhudumia mashamba yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye ugawaji ni suala la kuangalia wakati na muda maalum wa kugawa. Mara nyingi umbali kutoka kwenye ghala unasababisha wengine wakose hizo pembejeo. Basi tujiahidi maghala yaliyo mazuri ya vyama vya msingi na vijiji yatumike yote ili mkulima asiende mwendo mrefu kufuata hizi pembejeo, jambo ambalo linamkatisha tamaa wakati mwingine kufuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, lingine ambalo namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hii ni mara ya pili naliongea, kuna kero kubwa sana ya wakulima kuhusu akaunti zao kwenye benki zetu za biashara. Niliomba mwaka 2024 kwamba, Wizara ya Kilimo ikae na Wizara ya Fedha warekebishe Sheria ya Fedha inayohusiana na akaunti za wakulima kuwa *dormant* ndani ya miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo linasumbua sana wakulima, kila mwaka wanakuwa kama wanaenda kufungua akaunti mpya. Mkulima ameuza korosho zake, hana habari, hapati *message*, anakaa mnada wa kwanza, wa pili, wa tatu, kumbe hela imeshaenda benki, imegonga ukuta kwa sababu akaunti yake imekuwa *dormant*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana, hebu wasaidieni hawa wakulima waondokane na hii kero kwa sababu, ipo ndani ya Sheria ya Fedha. Basi mjitahidi *BoT* warekebishe kuhakikisha kwamba akaunti za wakulima zisiwe na muda maalum wa kuzifunga kabla hawajaanza kufanya operesheni. Hili jambo litatusaidia sana kupunguza kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la maghala. Naomba kila siku, ubora wa korosho unatokana na ubora wa maghala. Stakabadhi Ghalani pamoja na *TMX,* kama hakuna ubora wa zao, kwa kweli inakuwa ni shida. Tunaomba sana tutengeneze programu maalum ya kujenga maghala kwenye vijiji vyetu, ili vyama vya msingi vitumie maghala maalum, badala ya nyumba za watu ambazo hazina ubora ule unaotakiwa kwa ajili ya kutunza mazao yetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate, ahsante.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Kungu na Mheshimiwa Hasunga ajindae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia mjadala wa hii Bajeti ya Kilimo. Mimi ni Mbunge ambaye natoka Jimbo la Ludewa ambalo wakulima ni wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuthamini sekta ya kilimo. Napongeza pia Kiti chako na Bunge lote kwa kuidhinisha bajeti kubwa kwa miaka zaidi ya mitatu mfululizo kwenye Wizara ya Kilimo. Hali kadhalika, nampongeza sana Mheshimiwa Hussein Bashe kwa uthubutu, vilevile kufanya maamuzi mengi kwa kutumia takwimu na kuzingatia teknolojia kwenye kilimo. Hii kwa kweli, inatuvutia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nashukuru sana kwa ruzuku ya mbolea. Kwa kweli, wananchi wa Ludewa, hasa wakulima, wameweza kuongeza mavuno. Tangu muanze kutoa hii ruzuku mavuno yameongezeka na wakulima wamepata fedha nyingi, wamelipa ada za watoto na kujenga nyumba za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu 2025 Ludewa tuna mahindi mengi sana. Kwa hiyo, wanaiomba Serikali, kupitia *NFRA,* iweze kujipanga. *NFRA,* kupitia Mkurugenzi Komba, mwaka 2024 walifanya kazi nzuri; walinunua mahindi kwenye vituo vingi Ludewa, wananchi walifurahi sana na mwaka huu pia, wanaomba ajipange. Namshukuru pia, ameweza kumlipa Mkurugenzi, zile *SES* zimeweza kusaidia sana kukwamua miradi ya wananchi ambayo ilikuwa imekwama. Kwa hayo, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lile ombi letu wananchi wa Ludewa kuweza kuwa na *godown* kwa ajili ya kuhifadhi, hasa mahindi, tuweze kufikiriwa na Serikali. Pale Ludewa Kijijini kulikuwa na *godown,* sasa limechakaa, lilikuwa linahudumia wakulima kutoka Kimelembe, Ibumi, Kata ya Ludewa na lilikuwa na uwezo wa kuhifadhi tani nyingi sana. Kwa hiyo, mwaka 2024 walishindwa kununua zaidi, kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mlangali kuna *godown* ambalo linahitaji tu ukarabati wa ile sehemu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kupitia *SCR,* Watu wa *NFRA* waweze kwenda kukarabati hilo eneo kupunguza tope na vumbi, ili mazao yale yanunuliwe katika mazingira ya usafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kuna Kituo kingine kile cha Amani, wale wanachoomba tu ni ule mradi ambao mlikuwa mnashirikiana na watu wa TAMISEMI, ninadhani ni *RISE,* ambao ulikuwa unaboresha barabara za vijijini kwenda kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa. Ludewa, ule mradi bado tunauhitaji kwa sababu tuna uzalishaji mkubwa sana. Unavyozungumzia Kata ya Ibumi, mkulima mmoja anapata magunia 8,000 ya mahindi. Kwa hiyo, kule ukisema lori la tani 10 liende ni kuwapa hasara wakulima, kuwaingizia gharama na kuwakimbizia masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba ule mradi ambao ulikuwa unashirikiana na watu wa *TARURA* kuboresha barabara za vijijini. Kule tuna uhitaji wa barabara inayoanzia pale

Madope kwenda Madilu – Ilininda mpaka Kata ya Mundindi. Ile barabara ina uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba pia, kule kuna wakulima wa viazi, kuna zao wanalima ule msimu wa umwagiliaji, wanaita kipalila. Wale wananchi wanahangaika wenyewe kwa teknolojia ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana, Mheshimiwa Waziri, atume wataalam kutoka umwagiliaji waweze kwenda kujifunza, kile kilimo kinaitwa kipalila, kwenye Kata ya Madilu, Milo, Lupanga na Mlangali, ili waweze kuwasaidia kuboresha ile teknolojia ya umwagiliaji kwa sababu, vile viazi vinawawezesha sana kiuchumi. Naomba sana watu wa umwagiliaji waweze kuwatembelea kuboresha kile kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, barabara nyingine ambayo ni ya ukanda wa uzalishaji mkubwa inaanzia Kigasi, inakwenda Milo – Ludende mpaka Kata ya Mundindi, kupitia Amani. Kwa hiyo, ule mradi wa *RISE* utusaidie, hata kama hawataweka lami, waweze kuweka changarawe ambayo malori mpaka ya tani 30 yatapita msimu wote na ile barabara inayoanzia Ludewa kwenda Ibumi kuja kuunganisha Mundindi. Huu ni ukanda wa uzalishaji mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba ule mradi ufuatiliwe uweze kutusaidia kwenye barabara za ukanda wa uzalishaji. Kama mkulima analima mazao, anashindwa kuyafikisha kwenye masoko kwenda kwa walaji, sekta ya kilimo tutachelewa kuweza kupunguza umaskini kwa sababu, hadi sasa sekta ya kilimo imechangia 26% ya pato la Taifa na kuajiri zaidi ya 65% ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kile kitendo cha Waziri wa Kilimo kugawa minazi bure, ule ni uwezeshaji mkubwa sana wa kiuchumi kwa wananchi unaofanywa. Wale wakulima wakianza kuvuna zile nazi watapata mapato mengi sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nashukuru kwa Miradi ya Umwagiliaji Lihuu na Ivumi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kungu, jiandae Mheshimiwa Hasunga na Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie hii Wizara ya Kilimo. Nianze kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuleta suluhu ya changamoto kubwa iliyokuwa inawakumba wakulima; changamoto ya pembejeo pamoja na viuatilifu. Kwa nini nasema ameleta suluhu ya changamoto hiyo ya pembejeo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu katika jimbo langu kwa miaka mitatu mfululizo, 2022/2023, zao la korosho tulipata tani 15 peke yake. Mwaka 2024/2025 tumevuna takribani tani 31 na zaidi. Hii yote imeletwa na wakulima wale kupewa pembejeo, kwanza kwa wakati; na pili, bure kabisa. Kwa hiyo, utagundua mwanzoni tulikuwa tunapata uzalishaji mdogo kwa sababu ya kukosa *Sulphur* na viuatilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Naomba nimshukuru Waziri, Mheshimiwa Bashe, yeye na Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jambo langu la pili Wilaya ya Tunduru, sisi uchumi wetu unachagizwa na kilimo. Kama unachagizwa na kilimo, mazao yale ili tuweze kupata tija ni lazima yaongezewe thamani. Tunayaongezaje thamani? Maana yake ni korosho zile zinazovunwa zinapaswa kubanguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunduru tuna Kiwanda cha Ubanguaji Korosho. Kiwanda kile kilikuwa kinafanya kazi vizuri sana kwa ufanisi mkubwa. Pia, kilikuwa kinatoa ajira kwa akina mama zaidi ya 600 na vijana zaidi ya 200, ambapo walikuwa wanafanya kazi ya vibarua pale, wanapokea posho ama mishahara yao kwa

kila mwezi. Sasa ninavyosema hivi sasa, kiwanda kile kimesimama kwa muda mrefu sana, hakifanyi kazi. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba ajira zile za akina mama na vijana zimekwenda kuyeyuka, na kwa bahati mbaya sana wakati kiwanda kile kinasimama, kilisimama na madeni ya wale vibarua. Wale wamama na vijana wanadai fedha nyingi, wamejaribu kufuatilia na mpaka hivi sasa hawajalipwa fedha zao. Kwa hiyo, Serikali ilikuwa ina nia njema sana ya kujaribu kutafuta wawekezaji ambao watawekeza viwanda vile ili waweze kuviendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi, mwekezaji wa kiwanda kile pale Tunduru tunaona kabisa ameshindwa kukiendeleza, kwa lugha nyepesi, hana uwezo wa kukiendeleza kiwanda kile. Kwa hiyo, naomba niishauri Serikali ione namna ya kuweza kukirejesha Serikalini na hatimaye apewe mwekezaji mwingine mwenye uwezo, ili sasa kiweze kufanya kazi, wakulima na wananchi wa Tunduru wanufaike; akina mama zaidi ya 600 pamoja na vijana wale waendelee kupata ajira ya muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwenye Jimbo langu tulipata Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji ambao una thamani ya shilingi bilioni 6.4, lakini yule mkandarasi wa skimu ile mpaka sasa tunavyozungumza, ilipaswa awe ametekeleza mradi ule kwa zaidi ya 50%, lakini ametekeleza kwa 18%. Kwa hiyo, tunaona *speed* yake ni ndogo. Tunaomba *speed* iongezeke na kama kuna tatizo lolote, basi Wizara ikae chini ione namna ya kuweza kutatua mradi ule uweze kuendelea kwa sababu, Tunduru tunategemea sana Kilimo cha Mpunga na kilimo kile kinalimwa msimu hadi msimu. Mradi ule wa skimu ya umwagiliaji ukikamilika tunakwenda kulima bila kutegemea msimu na hatimaye tutaendelea kulisha mchele Lindi, Ruangwa, Nachingwea na Mtwara pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la tatu ni ukomo wa uongozi wa Bodi za Vyama Vikuu. Mheshimiwa Waziri viongozi wale wa vyama vikuu, muda wao wa uongozi ni miaka mitatu. Kama ni miaka mitatu, tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri yake ni kwamba, baada ya mwaka mmoja atafanya kazi, lakini mwaka wa pili ataanza maandalizi tena, kwa maana hiyo atakosa ufanisi. Kama alikuwa ni kiongozi bora, kiongozi mzuri, ataishia njiani kwa maana muda mwingi anakwenda kuandaa uchaguzi na hatimaye anashindwa kuboresha kazi yake. Kwa hiyo, nashauri muda huu uweze kuongezwa, badala ya miaka mitatu, iwe mitano. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiri kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hassan, muda wako tayari umeisha.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, halafu Mheshimiwa Mchungahela na Mheshimiwa Tabasam jiandaeni.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja ya Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, ambaye kwa kweli, amekuwa na maono makubwa na msikivu. Tulimshauri kwa muda mrefu kwamba, aongeze uwekezaji kwenye sekta za uzalishaji, na kwa kweli, amedhihirisha kwa namna alivyowekeza na ambavyo bajeti imeongezeka. Hongera sana. Pia nampongeza, kwa kutoa usafiri kwa Maafisa Ugani na zaidi ya hapo kwa kutenga fedha, kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa na kuongeza sekta ya umwagiliaji. Ametenga fedha nyingi, ambayo kwa kweli, haijawahi kutokea, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naipongeza sana Wizara. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wote walioko katika Wizara yake. Kwa kweli, sisi tumedhihirisha leo kwamba, wanasema mzigo mzito mpatie Mnyamwezi, na kweli, haya yamejidhihirisha kwa namna

ambavyo mmesimamia vizuri sana Wizara ya Kilimo. Tunaona jinsi ambavyo mnachacharika na tunaamini, hata wananchi wale, wapigakura wenu kwa kweli, watawarudisha katika nafasi zenu ili muweze kuendelea kuongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, nawapongeza sana kwa kuanzisha Benki ya Ushirika. Benki muhimu sana ambayo tunaamini itatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu nampongeza, kwanza kupitia Bodi ya Kahawa kwa kutuchimbia visima kwa ajili ya umwagiliaji wa mashamba ya kahawa. Kwa kweli tunakupongeza sana, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri ambayo wameifanya, lipo jambo ambalo tunalo kama ombi. Tunajua wamefanya mengi na wanaendelea kuyafanya, lakini pale Mbozi tulikuwa na yale maghala ambayo yalianza kujengwa tangu mwaka 2017. Yale maghala ambayo tunaita vihenge, vilikuwa ni vihenge vizuri sana, na mpaka sasa hivi, tangu viliposimama mpaka leo wananchi wanasubiria vile vihenge vikamilike ili viweze kutoa mchango mkubwa katika kutunza mazao yetu ya nafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vihenge tunaomba vipewe uzito. Tunaelewa kwamba zilikuwa ni fedha za mkopo kutoka huko nchi ya *Poland,* sasa tumeanza kulipa mkopo, lakini bado yale maghala hayajakamilika. Ni vizuri wakiyasimamia, yakiweza kukamilika itakuwa vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tunawapongeza kwa bei nzuri ya upande wa kahawa na namna ambavyo wamefanya. Kwa kweli kahawa sasa hivi bei mwaka huu imekuwa ni nzuri sana. Sasa tunaomba *BBT* ambayo wanayo, ambayo inakwenda kwenye halmashauri, wale vijana na watu wengine wahamasishwe kwenda kuwekeza kwenye zao la kahawa ambalo ni muhimu sana katika maendeleo ya wilaya yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, tumepata changamoto sana mwaka huu kuhusu soko la mazao ya parachichi. Parachichi tumepata changamoto kubwa sana. Tulihamasisha wananchi wakalima parachichi kwa wingi, wakazalisha kwa wingi, lakini soko mwaka huu baada ya kuyumba kwa kweli wamekosa mahali pa kwenda kuuza. Tunaombeni msaada tusaidiwe ili kutafuta masoko zaidi tuweze kulima zaidi tuweze kuongeza kwenye maembe na maeneo mengine. Hii tunaamini kwamba itatoa mchango mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne, soko la nje kuhusu mahindi na mazao mengine, tunaomba, tunajua sasa hivi kuna changamoto ya mahusiano ya Zambia, Malawi, na maeneo mengine; tunaomba yaimarike ili masoko yale yafunguliwe na wananchi wa maeneo yale waweze kuuza. Tuuze kama ni mahindi tuweze kuuza kule, kama ni kuuza mbegu tuweze kuuza, kama tunapata mbegu kutoka kwao, basi ziweze kutusaidia; na hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo nilitaka kulisemea ni kuhusu kiwanda cha kuongeza thamani. Tunacho kiwanda cha kahawa pale Mlowo. Tungeomba kile kiwanda sasa kipige hatua zaidi kianze kutengeneza kahawa mpaka hatua ya mwisho badala ya kuongeza tu thamani ile. Sasa tutengeneze kahawa ambayo inatengenezwa *instant coffee* kutoka kule Mbozi. Hiyo itakuwa kwa kweli ni msaada mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Waziri ameifanya katika Wizara, tunaamini sisi; na bado naendelea kuimba na wao nimesikia kwamba wanaimba wimbo huo, kwamba kilimo ni chakula, ni viwanda, ajira, uchumi, na fedha. Hili sisi tutaendelea kulisimamia, tutaendelea kuhamasisha kuungana na juhudi za Wizara ili mambo yaendelee kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ni kuhusu lile bwawa la pale Msia. Bwawa lile tulitengewa fedha mwaka juzi, lakini hazikuweza kwenda. Naliomba lile bwawa basi mwaka huu fedha zingeenda pale ili bwawa lile liweze kukamilishwa, na ili

wananchi wa Wilaya ya Mbozi na wa eneo la Msia waweze kumwagilia. Hii itatusaidia sana katika kuweza kuchangia uchumi mkubwa wa eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, nawapongeza timu nzima, wamefanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mchungahela, wajiandae Mheshimiwa Tabasam, Mheshimiwa Manyinyi na Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Tunayo mengi sana ya kuzungumza kuhusu kilimo, na hii ni kutokana na jinsi kilimo kilivyopiga hatua. Baada ya ujio wa Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kumekuwa na mabadiliko makubwa sana au mapinduzi makubwa sana ya kilimo. Kama ilivyokuwa utaratibu wake, ameamua kupeleka fedha za bure kabisa moja kwa moja kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona nia hii akiwa anaifanya tangu alipoingia. Kwanza tuliona alivyopeleka fedha za bure kwa wananchi kupitia mafuta. Wakati tulipopata changamoto ya mafuta, alitoa fedha za bure kabisa ambazo tulikuwa tukizitumia. Kwenye eneo la kilimo pia ametoa fedha za bure na bado anaendelea kutoa fedha za bure. Hapa ninawashauri wananchi wote, hususan wananchi wangu wa Jimbo la Lulindi, kutumia fedha hizi za bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ametoa fedha za bure kwenye pembejeo za kilimo. Pembejeo zote, kwa mfano, kwenye upande wa korosho tunapewa bure kabisa, hatulipii hata senti moja. Ni fedha za bure kabisa. Mheshimiwa Rais ametoa fedha za bure kwenye mbolea. Hapa ametoa takribani fedha nyingi sana zinazowezesha wananchi kupata fedha za bure.

Kama wataamua kulima takribani nusu ya mapato yao inatokana na fedha za bure walizopewa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais pia ameendelea kutoa fedha za bure kwenye mradi wa *BBT*. Huu ni mradi ambao unalenga katika kumwezesha kijana popote alipo ili apate fedha za bure kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika Mheshimiwa Rais amewezesha pia upatikanaji wa fedha za bure kwenye miundombinu ya umwagiliajia kwenye mabwawa. Kwa mfano, mabwawa yote yanayojengwa, yanajengwa na fedha za bure kabisa, ambapo kama wananchi wataamua kwenda kwenye kilimo na kufanya kazi hii ya kutafuta fedha za bure watazipata, ni za bure kabisa, ziko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawashauri, kama nilivyosema tangu huko mwanzo, wananchi kwa nguvu kabisa tuzichukue fedha hizi, ziko wazi kabisa, wala hazihitaji shida yoyote, wala hazihitaji msukumo wowote. Ni kuamua tu kwenda na kuzipata pale. Ziko bure kabisa, twende tukazichukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa upande wangu natamani pia fedha hizi za bure nizipate katika jimbo langu. Katika kata takribani kama sita saba hivi; Kata ya Mpindimbi, Kata ya Mbuyuni, Kata ya Lupaso, Kata ya Sindano, Kata ya Lulindi, Kata ya Lipumburu, Kata ya Mnavira, na Kata ya Mchauru. Kata hizi zote pamoja na Kata ya Lulindi, ni kata ambazo zinawezesha kilimo cha umwagiiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, kama miundombinu ya umwagiliajia itajengwa pale ambayo itawawezesha wananchi wangu wa kata zile kupata fedha za bure, hakika jimbo langu litastawi kweli kwa sababu ni ustawi ulio wazi ambao umepewa nyenzo za kukua kwa haraka kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atakapokuja ku-*windup* hapa, anihakikishie na mimi katika jimbo langu fedha hizi za bure naweza kuzipata

vipi, hususan katika maeneo haya niliyomwambia? Mimi na yeye tulikaa huko nyuma tukaanza kuzungumzia suala la kuweza kutoa pia ruzuku mbalimbali kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, kuna jambo ambalo tumeona halifanyiwi kazi. Kwa mfano, benki. Kama benki imekuwa ikipitia fedha nyingi sana za wakulima. Kwa mfano, Pato letu la Taifa katika nchi hii ni takribani kiasi cha bilioni 80 fedha za kigeni. Bilioni 80 dola, hayo ni mapato ya nchi hii. Sasa, katika pato hili kilimo kinaingiza takribani 26%. Ukifanya mahesabu yako, 26% ya pato hili ni takribani shilingi trilioni 54 za Kitanzania. Fedha hii yote imekwenda benki, imepitia benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, fedha hizi benki wamekuwa wagumu sana kuwasaidia wananchi, kwa sababu chanzo cha mapato yao makubwa, hiyo shilingi trilioni 54 inatokana na wakulima, lakini wao hawatoi mkopo kwa wakulima ambapo ndiyo chanzo chao kikubwa cha mapato hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, nilimtaja Mheshimiwa Tabasam, lakini atakuwa wa mwisho. Tunaanza na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Chaya. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam, nimesema utakuwa wa mwisho. Tunaanza na Mheshimiwa Manyinyi, anakuja Mheshimiwa Dkt. Chaya, wewe utakuwa wa mwisho.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hii Wizara ya Kilimo. Mimi pia naungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wameendelea kuifanya katika hii sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, mimi nichangie tu kwenye maeneo mawili, hasa yale ya *BBT* kwa ajili ya wale ma-*giant* wakubwa lakini pamoja na hawa wadogo wadogo. Nianze na lile la wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale wakulima wakubwa, nimshauri Mheshimiwa Waziri atengeneze tu ile *data bank* ya wakulima wakubwa, wafahamike. Wakishafahamika, yaani hao wala hahitaji hata kuchukua fedha ya Serikali katika kuwasaidia. Anachohitaji kufanya hapo ni kazi ndogo tu. Aangalie tu hata yale mashamba ya Wizara yote ambayo yako tupu na ambayo najua yako mengi. Hayo mashamba ukiangalia leo, yako mazao ya muda mfupi, lakini bado yanafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nilikuwa najaribu kuangalia hapa kwa mwaka 2023/2024 kuna zao kama la ufuta ambalo limeingizia Serikali, siyo chini ya shilingi trilioni mbili, zimeingiza fedha za kigeni. Sasa, ufuta ni zao ambalo unalima tu katika kipindi kifupi, tayari unaweza kuvuna. Yako pia mazao mengine kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nini kifanyike? Kumbe cha kufanya ni kwamba, akiwashirikisha hao wakulima wakubwa ni rahisi sana wakafanya kazi hiyo. Tena wakati mwingine anaweza katika lile soko akafunga *ile forward contract*, ukajua kabisa kwamba tani kiasi kadhaa zinatakiwa kwenye nchi fulani, akawahamasisha wakalima. Kwa hiyo, ndani ya muda mfupi tayari yale matokeo yakaweza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika yale maeneo yote ambayo tuna mashamba makubwa, hao wafanyabiashara wakubwa wengi wanahitaji tu elimu na waelekezwe kwamba

hapa kuna fursa, atatumia fursa zake. Hata pale ambapo hana uwezo; leo nimemwona Mkurugenzi wa *CRDB,* ninadhani amekuja hapa na amekaa kwa muda mrefu. Ni kwa sababu naye nadhani ameanza kuwa na *interest* katika kilimo. Kwa hiyo, anaweza naye akatusaida, pamoja na benki nyingine kwenye upande huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapokuja kwenye lile suala la wale wakulima wadogo, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, asichukue ile mikoa 21 tu. Hebu *BBT* hii ya wakulima wadogo iende kila mkoa. Nitoe tu mfano, na nimwombe siku moja apate nafasi aje pale kwangu, nami ni mkulima, ninalima pale Bunda. Yaani pale pembeni yangu ziko *eka* zaidi ya 500 lakini unakuta kila mkulima anaweka ka-*pipe* ka inchi moja na nusu, anatumia hivi vi-*honda*, kwa hiyo anahangaika, yaani usiku mzima wanahangaika. Yaani unaangalia hawa watu, kumbe wanachohitaji hapa ni vifaa tu, na wala siyo vifaa vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanahitaji tu bomba la inchi sita, wanahitaji ile *pump* ya shilingi milioni mbili pamoja na ile *motor* ya milioni tatu *horsepower* 50. Wale watu Mheshimiwa Waziri akiwavutia kwa kuwawekea hivyo vifaa vyote, akivi-*consolidate* havivuki shilingi milioni 50 mpaka 100. Kwa hiyo, akiwawekea pale wanaweza kumwagilia eka 500. Sasa, leo tujiulize, kwenye nchi hii hao wakulima, yaani hayo maeneo ya eka 200, eka 500 yako mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kumbe leo akiamua ndani ya mwaka mmoja wakulima wengi kabisa wa nchi hii, hao wadogo wadogo wanaweza wakafanya kazi. Watu wa kusaidia kusimamia, yaani badala ya yeye sasa kwa *level* yake, anahitaji aanze kufikiria mambo makubwa. Badala ya kufikiria habari ya kwenda kuangalia vijana wa Chinangali, sijui vijana 200, vijana 100... *(Makofi)*

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, atakuja Mheshimiwa Tabasam, ajiandae Naibu Waziri.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuchukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia leo kwenye Wizara ya Kilimo. Kipekee, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kule Manyoni upande wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Waziri Bashe, Naibu Waziri na Katibu Mkuu Mweli kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika ku-*transform* Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme kwamba Mheshimiwa Bashe naye akiwa na Mheshimiwa Rais wameitendea haki sana Manyoni. Upande wa umwagiliaji, kuna miradi ilikuwa imeongelewa zaidi ya miaka 15. Kila ilani ilikuwa inataja Bwawa la Mbwasa na *Scheme* ya Umwagiliaji ya Udimaa, lakini ndani ya hii miaka minne ya Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Bashe akiwa Waziri wa Kilimo, ameweza kuweka historia ya kutangaza tenda ya ujenzi wa Bwawa la Mbwasa la Umwagiliaji, na tayari mkandarasi ameshapatikana na tayari ameshakabidhiwa *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mkandarasi amekabidhiwa *site,* lakini hayupo *site*. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, huyu mkandarasi afike sasa *site* aanze kazi, na wananchi wananiulizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Bwawa la Udimaa la Umwagiliaji, vilevile nimshukuru Mheshimiwa Waziri, alitangaza tenda Udimaa ya ujenzi wa bwawa. Tayari mkandarasi ameshapatikana. Naomba vilevile huyu mkandarasi aweze kwenda na kuanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ningeshauri, tukiacha hii miradi mikubwa ya umwagiliaji, kuna hawa wakulima wadogo wadogo wa mboga za majani ambao kimsingi wangeweza kuhitaji umwagiliwaji katika *small scale*. Ningeshauri, Mheshimiwa Bashe aangalie, tunawezaje kuja na mfumo wa *pump* kwa ajili ya kusawaidia hawa wakulima wadogo wadogo wa umwagiliaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, najua hii miradi mikubwa ni kwa ajili ya *Large Scale Irrigation System*, lakini anaweza akaja na mfumo mzuri kwa ajili ya hii miradi midogo ya umwagiliaji. Nakumbuka niliwahi kufanya kazi *Word Vision*, tulikuwa tunatumia *pump* fulani zinaitwa *Money Maker Pump*, ambazo kimsingi zilikuwa zinasaidia sana wakulima wale wadogo wadogo. Tuangalie ni jinsi gani Serikali inaweza ikasaidia hata kwa kuweka ruzuku, ili nayo tuwasaidie wakulima wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni korosho. Kwa kweli Manyoni tunalima sasa korosho. Watu wa Mtwara walikuwa wanatucheka Manyoni hatulimi korosho, lakini Mheshimiwa Bashe pamoja na Mheshimiwa Rais wameleta mapinduzi makubwa kwenye kilimo cha korosho. Mwaka huu tumeweza kuuza zaidi ya tani 100,000 za korosho, lakini vile vile hata bei ya korosho tumeuza katika daraja la kwanza 3,167. Haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya hiyo, Mheshimiwa Bashe ameweza kujenga ghala Manyoni, ameweza kujenga Kituo cha *TARI* Manyoni, ameweza kupeleka pikipiki nyingi pale Manyoni, na ameweza kupeleka wataalamu pale Manyoni. Kwa hiyo, mimi namshukuru sana Mheshimiwa Bashe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, korosho ya Manyoni bado ina changamoto. Moja, ni tembo. Hili Mheshimiwa Waziri analifahamu, yeye na Waziri wa Maliasili. Naomba tukatatue changamoto ya tembo wale wa Manyoni kwa sababu wanamharibia korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine namshukuru ametoa ruzuku ya dawa kwa wakulima wa korosho wa Manyoni, wanashukuru, lakini wanaomba vile vile ifike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu tumbaku. Manyoni tunalima tumbaku. Namshukuru sana Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku, alifika Manyoni na wataalamu wake wamehamasisha watu kulima tumbaku. Tunaomba sasa Mheshimiwa Bashe aje Manyoni. Mbali na korosho, sisi tuna maeneo mengi ya kulima tumbaku na wananchi wamehamasishwa kulima tumbaku. Tunataka vilevile kuwekeza kwenye tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, mimi nakushukuru tena. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais, nimshukuru na Mheshimiwa Bashe na ninamwombea. Najua atarudi kuwa Mbunge na atarudi kuwa Waziri wa Kilimo. Akirudi aendeleze kilimo cha umwagiliaji Manyoni, hasa Tarafa ya Kintinku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tabasam, jiandae Naibu Waziri.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi nami kuwa mtu wa mwisho kuchangia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa anza mchango wako, acha kushukuru. *(Kicheko)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kuna mambo mengi sana yanaendelea ndani ya Afrika Mashariki na Tanzania kwa ujumla, hasa katika masuala ya biashara ya kilimo. Biashara za mazao ya kilimo kumekuwa kuna matatizo katika mipaka yetu ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo limetokea, tumeona mfano bidhaa zetu zimezuiwa kuingia *South Africa*, zimezuiwa kuingia Malawi; lakini imekuwa ni kampeni kubwa sana, na kampeni hizi zinaendeshwa na wanaharakati ili kuhakikisha kwamba Tanzania hatuwezi kufanya biashara ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wanaharakati hawa wamekuwa sasa wanataka kuingilia hata msimamo na masuala yetu ya siasa za ndani ya Tanzania. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kuwa-*lock* hawa watu ambao walikuwa wanataka kuingia kupitia Uwanja wetu wa Ndege wa Dar es Salaam, na wakarudishwa kwao. Tunatakiwa Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono jitihada za Mheshimiwa Rais kulinda nchi na mipaka yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo limeongelewa mpaka na Wabunge wenzetu wa Kenya, kwamba kuna watu wanaofanya chokochoko za kwenda katika nchi nyingine. Kwa hiyo, maamuzi yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais yanatakiwa kuungwa mkono kwa nguvu kubwa sana na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengi ambayo kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi yetu, ni kwamba masuala yoyote yatakayokuwa Mahakamani, sisi hatutakiwi kuyajadili hapa. Sasa kumekuwa kuna watu ambao kwa kupitia baadhi ya *NGO,* wanataka kutumika vibaya kuja kuharibu usalama wa nchi yetu na usalama wa biashara zetu za kilimo na mazao haya tunayoyalima hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo ambalo ni baya zaidi ni kwamba, sasa wanaanza kutumika hawa watu katika masuala mengi sana ya kuhusiana na mazao yetu ya kilimo pamoja na mifugo. Sisi Tanzania kama nchi, maamuzi anayoyachukua Mheshimiwa Rais, kwa ajili ya nchi yetu, tunatakiwa tuwe imara na Bunge lako pia limuunge mkono kwa maamuzi ya kuilinda nchi. Siyo lazima tuilinde nchi kijeshi, tunaweza tukailinda katika mipaka yetu, kuzuia watu wanaokuja kuharibu taswira na amani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaanza kuchangia. Tuna mazao yetu ya kilimo, hasa zao la pamba katika Mkoa wa Mwanza, Simiyu, Geita, Tabora, Katavi, Singida, na Kagera kidogo na sasa hivi Kigoma, zao la pamba linalimwa kwa kiwango cha juu sana. Zao hili la pamba limekuwa likipata bei za mkanganyiko mpaka kiasi ambacho pamoja na Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, imesema zao la pamba ifikapo 2025 tuwe tuna uwezo wa kuzalisha tani milioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo halitawezekana kama zao la pamba na lenyewe halitachukuliwa kwa uzito mkubwa kama ilivyochukuliwa korosho. Unajua kabisa wakati Mheshimiwa Bashe, amekaa katika kiti hiki ambacho mimi nipo hapa sasa hivi, nilikuwa namwangalia sana wakati huo mimi sijawa Mbunge, anazungumzia pamba. Pamba imekuwaje? Amesahau haya maneno ya pamba, au mkishaingia ndani ya *game* mnasahau haya mambo? Naye bahati nzuri ni mtoto wa Wasukuma anatokea Nzega, anajua kabisa mambo ya pamba yalivyo. Pamba inavyokuwa na shida. Ulimaji wa pamba una shida kwa kiwango cha juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ifikie mahali ambako tunashukuru, pamoja na kuweka kwamba Igunga peke yake iwe ndiyo *pilot* ya kulima kwa ajili kupata mbegu za pamba, lakini pamoja na Igunga kuwa ndiyo inayotakiwa kuzalisha mbegu za pamba, zisambazwe zifike kwa wakulima. Sisi ruzuku bado haijatufikia na tunachotaka, uundwe mfuko wa pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aje awaeleze Watanzania wanaolima pamba zaidi ya mikoa 17, awaambie kwamba, "pamba sasa itapata ruzuku, limeni pamba tufikishe tani milioni moja, tuinue uchumi wa nchi yetu." Leo tunakuwa tunavaa mashati, ukilivaa tu unapigwa shoti. Unavaa shati unapigwa shoti! Sijui haya mashati ni ya nailoni, wakati sisi tuna pamba hapa. Kwa nini tuvae nguo za namna hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nguo zote yaani unapigwa shoti. Yaani kama vile umepigwa shoti ya umeme, kumbe unavaa shati.

Sasa haya mashati haya na sisi tunalima pamba, hebu tulilinde hili zao la pamba lisije likapotea katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninavuka Daraja la Magufuli sasa ninaingia jimboni Sengerema; ninamshukuru Mwenyezi Mungu daraja limekwisha, sasa sijui Mheshimiwa Bashe ana kizuizi gani cha kuja Sengerema? Kwa sababu alikuwa anaogopa *ferry*, sasa je, atakuja Sengerema kuona tuna Kiwanda chetu cha Buyagu, tuna *ginnery* ipo Buchosa kule kwa mdogo wangu Mheshimiwa Eric Shigongo, na yenyewe kule ilikuwa inazalisha mafuta, lakini tuna viwanda vipo Nyambiti kule vyote vinakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tuna kiwanda kipo Manawa kule Misungwi, tuna kiwanda kipo Ukerewe, na viwanda vingine vipo Magu. Naomba Mheshimiwa Waziri aje aangalie namna ya kufufua hivi viwanda. Nyanza ina zaidi ya shilingi bilioni mbili, sasa hivi bilioni mbili na nusu. Kama kuna bilioni mbili na nusu, waruhusiwe hizi pesa wakanunue *ginnery* mpya kule India au hata wakanunue *used* ambazo zina hali nzuri kwa sasa hivi, ili tufufue zao la pamba, tuanze kulima pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Nyanza inaanzishwa Mheshimiwa Bashe, mwaka 1972 wananchi wa Mkoa wa Mwanza walikuwa 840,000 leo wananchi wa Mkoa wa Mwanza wapo zaidi ya shilingi milioni 2.7. Sasa kwa hali hiyo, sasa hivi Mheshimiwa Bashe anatakiwa amwambie huyu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika aje naye kule, tupige mkutano awasikilize Wanamwanza wanataka nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Wilaya ya Mwanza ambayo ilikuwa Wilaya ya Mwanza ina Ilemela na Nyamagana, hawana hata sehemu *plot* ya kuchimba choo. Hawa bado wanahitaji, wao ni wakulima wa pamba, hawa wanahitaji sasa hivi kufuga samaki, wanahitaji kufuga kuku, kufuga ng’ombe na huu ushirika ulianzishwa kwa ajili ya kulima pamba, lakini pamoja na hali hiyo, Geita tayari imeshakatwa, wameanzisha mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna wilaya nyingine na yenyewe tena tumewaazima watu wa Simiyu Busega, tukawapa kule, kwa

hiyo yaani Nyanza inaendelea kukatwa katwa tu hivyo hivyo. Sasa kwa hali hiyo ukubwa wa Nyanza sasa hivi na ma-*godown* yaliyopo na viwanda vyetu, vyote sasa hivi wameanza kuweka stoo, wanaweka mbolea, wanaweka *cement*, wanakodisha wanaweka magodoro...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Tabasam, mchango wako ni mzuri sana, ahsante.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Bashe, akija hapa atuambie, sasa huu Ushirika wa Nyanza, je, bado utaendelea kuwa ushirika wa pamba?

**NAIBU SPIKA:** Haya, mengine utamfuata baadaye utamwambia. Mheshimiwa Tabasam, utamfuata kwenye meza utamwambia.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi, na ninamtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa Kimataifa *(National competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Katika kipindi chake akiwa Waziri wa Kilimo, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na taarifa ya Wizara ya Kilimo, Tanzania ina hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo cha

mazao, kwa wastani hekta milioni 10.8 tu sawa na 24% ndizo zinazolimwa kila mwaka. Sekta hii kwa mwaka 2024/2025 imeendelea kuchangia takribani 26.1% kwenye pato la Taifa, imetoa ajira kwa wananchi kwa wastani wa 65% na imechangia 65% ya upatikanaji wa malighafi za viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya kilimo ni mhimili wa uchumi wa nchi na inachangia pato la mkulima mmoja mmoja, kaya na Taifa kwa ujumla. Sekta ya kilimo na hususan sekta ndogo ya mazao imechangia 15.4% katika pato la Taifa na zaidi ya 100% ya upatikanaji wa chakula kinachozalishwa nchini na kupelekea utulivu wa mfumuko wa bei kwa takribani 59%.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kujitosheleza kwa chakula na kuchangia katika uchumi wa Taifa, takribani mazao yote yanazalishwa kwa tija ndogo katika eneo husika. Uzalishaji wa mahindi wa chini ya tani mbili kwa hekta moja ni 29% tu ya uzalishaji unaotegemewa wa tani sita kwa hekta moja. Uzalishaji huu wa chini kwa mazao yote kwa kiasi kikubwa unatokana na ukosefu wa ushauri wa watalaamu wa kilimo ikiwemo matumizi yasiyo sahihi ya mbolea na pembejeo nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hii, kilimo hakijamsaidia mkulima, kwa kiasi kikubwa tunajinasua kwenye umaskini na kimeendelea kutoa mchango mdogo kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hii ya takribani 65% ya Watanzania kuchangia 26% tu ya pato la Taifa, inahitaji kuweka mikakati ya kimageuzi ili sekta ya kilimo ichangie zaidi ya mara mbili ya sasa. Pia, kuwepo na mkakati wa kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na wakati huo huo kupunguza asilimia ya wananchi wanaotegemea kilimo kwenda kwenye sekta nyingine za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa mbolea nchini hadi Februari, 2023 ulikuwa tani 748,890 ambayo ilikuwa juu ya mahitaji ya tani 667,730. Pamoja na bei za mbolea kwenye Soko la Dunia kuwa juu, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa ruzuku ya

karibu 50% na kupelekea tani 300,179 kununuliwa kwa bei ya ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii muhimu ni mafanikio makubwa katika safari ya kuleta tija kwenye kilimo nchini na napendekeza kuendelea na ruzuku ya pembejeo pamoja na kuanzisha *Price Stabilization Fund* kwa pembejeo hasa mbolea ili kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iendelee kuimarisha usalama wa chakula nchini kwa kununua na kuhifadhi nafaka kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula. Kutokana na vita inayoendelea ya Urusi na Ukraine kunaashiria kuendelea kuwa na upungufu mkubwa wa nafaka na kwa kuzingatia gharama kubwa za uzalishaji wa karibu 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ichukue hatua za makusudi kusaidia wakulima wapate bei nzuri ya *NFRA* badala ya kuuza kwa walanguzi na kutorosha chakula nje ya nchi. Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, kufikia mwaka 2030, biashara ya mazao ya chakula inakadiriwa kufikia Dola za Kimarekani trilioni moja. Serikali ichukue hatua za makusudi kuboresha uzalishaji wa mazao ya chakula kutosheleza soko la ndani na nje. Uzalishaji wenye tija kwenye kilimo utaongeza upatikanaji wa fedha za kigeni na kupunguza pengo la urari wa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie fursa za Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kuanza uzalishaji wa viuatilifu inayotokana na pareto ambayo inazalishwa hapa nchini na imekuwa inauzwa nchi za nje kama *semi-finished product* kwa bei ndogo ya kutupa. Viuatilifu kutokana na pareto ni suluhisho la soko la pareto na pia suluhisho kwa upotevu wa mazao kushambuliwa na wadudu *(post-harvest losses)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ianze mchakato wa kuanzishwa viwanda vya mbolea kwa kutumia madini *(calcium carbonate, agricultural lime, phosphates, natural gas etc.)* yanayopatikana kwa wingi hapa Tanzania, kuanza uzalishaji wa mbolea hapa nchini. Kutokana na athari za vita ya Urusi na

Ukraine zinazoendelea, iwe fursa kwetu kwa kuanza kutumia rasilimali zinazopatikani nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha bajeti ya mwaka 2022/2023, Serikali ilitenga shilingi 834,382,834,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo sehemu kubwa ilielekezwa kwenye miundombinu ya umwagiliaji. Utekelezaji wa miradi hadi kufikia Februari, 2023 hasa utekelezaji kwa fedha za nje uko chini sana. Sehemu kubwa ya miradi inategemea kuchukua miezi 24 na kuna matumaini ya utekelezaji kwenda kama ulivyotarajiwa. Matumaini pekee ni hatua zilizooneshwa kwenye bajeti ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na Serikali iweke mikakati madhubuti kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa bajeti hii ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali iangalie utelezaji wa miradi ya mabwawa kuunganisha uratibu kwa mahitaji ya jumla kama vile mahitaji ya Wizara ya Mifugo na hata Wizara ya Maji, kunaweza kuwa na tija kuwa na chombo kimoja chenye nguvu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati hii pia iweke nyongeza za ujenzi wa mabwawa hasa maeneo yenye mafuriko makubwa ikiwa ni pamoja na kuzuia mafuriko. Pia, napendekeza Serikali iweke msukumo mkubwa wa kuharakisha utekelezaji wa miradi iliyomo kwenye Mradi wa Bonde la Mto Songwe *(Songwe River Basin Development Programme - SRBDP),* wenye ofisi zake Kyela, Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unaotekelezwa kwa pamoja na Serikali za Tanzania na Malawi, ni muhimu sana kwa sasa kutokana hasa na ujenzi wa mabwawa ambayo pamoja na manufaa mengine, yatasaidia kupunguza mafuriko ya Bonde la Kyela. Mabwawa haya yamelenga kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji, shughuli za uvuvi na hata utalii ambao unahitajika sana katika Wilaya ya Mbeya na ukanda wote wa Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ichukue hatua za haraka kuleta Bungeni mapendekezo ya Sheria ya Kilimo ambayo pamoja na mambo mengine itawezesha usimamizi wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo ambayo inaendelea kupotea kwa matumizi ya makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kutokana na changamoto za tabianchi, kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa mazingira na ongezeko la upungufu wa vyanzo vya maji. Uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu umepelekea misitu mingi kuharibiwa na uchomaji moto, ukataji mkaa na hata kilimo kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali iongeze msukumo kwa Wizara za Maji, Kilimo, Maliasili na Mazingira kufanya kazi kama timu moja ili kukabiliana na janga hili kubwa ikiwemo ujenzi wa mabwawa makubwa katika maeneo yanayokumbwa na mafuriko. Kama ilivyo kwa athari za mafuriko ya Kyela, hata Ziwa Rukwa linaathirika sana na kujaa mchanga na udongo unaosombwa na mito kutokana na mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwa moyo wa dhati wa kuwekeza kwenye kilimo kwa rasilimali fedha na watu katika kilimo. Uwekezaji kwenye fedha kupitia Serikali yake, ameongeza bajeti ya kilimo, hivyo kuboresha mipango ya kuendeleza kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, uwekezaji kwa rasrimali watu, amewekeza kwa kumteua Waziri wa Kilimo bora na Katibu Mkuu wake wenye *passion* na kilimo na kwa kweli kumwacha Waziri muda mrefu katika Wizara hiyo ili aendelee kutimiza maono yake ya muda mfupi, wa kati na mrefu juu ya maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maombi yafuatayo kwa mijini ikiwemo Mji wa Iringa. Mji wa Iringa ni mji wa kitalii, na kwetu

sisi mazao ya mbogamboga ni muhimu sana. Sasa naomba ufanyike ukarabati mkubwa wa *scheme* ya umwagiliaji Mkoga iliyopo Kata ya Isakalilo ambako inazalisha mbogamboga kwa ajili ya kulisha mji wetu. Pia, tunaomba kuchimbiwa bwawa kwa ajili ya umwagiliaji katika eneo la Kata ya Kiwele, Kitongoji cha Mapinduzi ili tuweze kulima mazao ya mbogamboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa kweli kuwapongeza sana viongozi wa Wizara hii, kwani wapo tayari kufanya kazi kwa ushirikiano bila urasimu usiokuwa wa lazima. Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu, kwa kweli na wataalamu wao wanafanya vizuri. Utendaji kazi wa Wizara hii unapaswa kuigwa na Wizara nyingine. Ushauri wangu *BBT* isiachwe, bali iboreshwe zaidi kwa kushughulikia changamoto zilizojitokeza kwenye utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tuendelee kutoa mafunzo kwa kushirikiana na sekta binafsi na JKT. Halafu tuwawezeshe wale waliofanya vizuri na kuwasimamia warudi na kuendeleza ujuzi huo kule walikotoka na siyo kuwapa maeneo sehemu nyingine ili kusambaza ujuzi huo sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mbegu za kienyeji litiliwe mkazo na zihifadhiwe zikiwepo na za mifugo, mwashauri pia. Tunaomba sasa mikoa ile yenye kilimo ufanyike utaratibu wa kuzitafuta mbegu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo, nampongeza Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa bajeti hii miradi jimboni Busanda, Mradi wa Umwagiliaji wa Nyamalulu Kata ya Magenge, na ombi la mradi wa umwagiliaji Kayenze (Saragulwa) Kata ya Nyamwilolelwa vifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mpango wa ruzuku kwenye pembejeo za kilimo uendelezwe na kuimarishwa na kupelekwa kwa wakati ili shughuli za kilimo maeneo yetu hususan Jimboni Busanda ziimarike. Usimamizi wa shughuli za kilimo uangallwe upya, Maafisa Ugani na shughuli za ugani hazikidhi maono makubwa yaliyopo sasa na baadaye.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mbunge; Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ernest Silinde, Mbunge; Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Mweri, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi; na watumishi mbalimbali waliopo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wamekuwa wasikivu na wenye kutekeleza. Pale wanapokuwa wanapelekewa hoja wanakuwa ni watu wa kufanya maamuzi kwa wakati na kutoa majibu yanayoleta tija; na amekuwa akifanya kazi kwa weledi na ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wanampenda na wanasema kuwa Wizara yake wameiweka kiganjani. Hii yote ni kwa sababu ya usikivu wake na utii kwa Waheshimiwa Wabunge pale wanapompatia hoja zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nitumie fursa hii kipekee kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa kwenye sekta hii ya kilimo. Tumeona kwa miaka mitatu mfululizo bajeti ya Wizara ya Kilimo inazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka hadi kufikia shilingi trilioni 1.2. Hii inaashiria maono makubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais juu ya sekta hii na tija yake imeshaanza kuonekana katika ukuaji wa sekta ya kilimo, mchango mkubwa katika pato la Taifa na ongezeko la uzalishaji kwa mazao mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wakulima wa korosho tunamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais jinsi alivyotoa kipaumbele kwenye tasnia ya korosho; kwanza kwa kutoa *Export Levy* ambayo Wizara na Bodi ya Korosho *(CBT)* imesaidia kupatikana kwa pembejeo za kilimo kwa wakulima wa zao. Pia kutuwezesha kupata kongani ya viwanda pale Maranje ili

kuongeza thamani ya zao la korosho. Wanamtwara wameahidi kumpatia kura za kutosha ifikapo Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuishauri Serikali mambo makubwa mawili. Jambo la kwanza ni kuhusu suala la kuweka utaratibu maalumu kwa wenye viwanda vya ndani kupata malighafi ya kutosheleza kwa mwaka mzima; na pili kupewa motisha mbalimbali kama vile motisha ya kikodi ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi na kuwapatia mikopo yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali ifanye hivyo kwa sababu watu hawa wanatoa ajira kwa akina mama na vijana. Nchi kadhaa wametengeneza utaratibu huu, mfano Benin, Msumbiji, Burkina Faso na *Ivory Coast*, wamefanya hivyo na wamefanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali itoe fedha Za *Export Levy* kwa Wizara ya Kilimo kwa wakati ili zitumiwe kama zilivyopangwa. Fedha za *Export Levy* za msimu uliopita hadi leo hazijatolewa, hivyo kuleta malalamiko kwa wazabuni ambao wamesambaza pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naiomba Serikali itoe fedha hizo kwa wakati ili wazabuni walipwe mapema, na tusipofanya hivyo watashindwa kuleta pembejeo za msimu ujao na kuathiri uzalishaji wa korosho kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza Wizara na Waziri Bashe kwa ubunifu, uzalendo na uchapakazi wake. *Allah* aendelee kumhifadhi na kumpa afya njema. Nawasilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimpongeze sana Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein M. Bashe, Mbunge; na Naibu wake Mheshimiwa David Silinde, Mbunge; Katibu Mkuu, Ndugu Gerald G. Mweli; Naibu Makatibu Wakuu, Dkt. Hussein Mohamed Omar na Dkt. Stephen Nindi; na wataalamu wa Wizara na taasisi zote zinazosimamiwa na Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita kwenye uhitaji wa miche bora ya kahawa na miradi ya umwagiliaji katika Jimbo la Moshi Vijijini ambako hulimwa kahawa, ndizi, mpunga, mahindi, maharage, mbogamboga na matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa kulipatia jimbo langu miche ya ruzuku ya kahawa. Naiomba Serikali iendelee kutoa miche bora ya kahawa kwa njia ya ruzuku kwa wakulima. Bado kuna uhitaji mkubwa wa miche ya kahawa katika Jimbo la Moshi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji Tanzania ni mbinu ya kilimo inayotumia mifumo ya kusambaza maji ili kumwagilia mazao badala ya kutegemea mvua pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kilimanjaro na hasa wakulima wa Jimbo la Moshi Vijijini hujihusisha na kilimo cha mpunga (ukanda wa tambarare), mahindi, maharage, mbogamboga, matunda, ndizi (kanda zote) na kahawa (ukanda wa milimani). Jimbo hili limebarikiwa kuwa na vyanzo vya maji vya uhakika vya asili vinavyotumika kumwagilia mashamba ya wakulima wadogo na wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa maji katika kulima kwa tija, naiomba Wizara itusaidie kwenye miradi ya umwagiliaji jimboni kwangu. Nina uhakika tukijengewa miradi nitakayopendekeza, sisi wa Jimbo la Moshi Vijijini tunaweza kubadilisha uzalishaji wa mazao, kipato cha wakulima, na kuchangia kwenye kuleta usalama wa chakula na kuzalisha mazao ya biashara kama kahawa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Umwagiliaji wa *Lower Moshi Irrigation Scheme (LMIS)* ulijengwa kwa msaada wa Serikali ya Japan mwaka 1987. Mradi huu ni maarufu hapa Tanzania na umesaidia kuongeza tija ambapo uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka kati ya tani 1.8 - 2t/ha za mpunga hadi tani 5.5. Mradi huu una miaka 38 na miundombinu imezeeka, maji yanapotea njiani. Naiomba Serikali ije kufanya uwekezaji kwa

kuboresha miundombinu iliyopo na kutafuta chanzo kingine ili maji yaongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wa ukanda wa milimani katika kata 14 kati ya kata 16 za Moshi Vijijini wanatumia skimu za umwagiliaji za asili na wengi wanakabiliwa na tatizo sugu la ubovu wa skimu hizo. Naiomba Serikali ije kukarabati na kujenga mifereji yote ya asili katika Jimbo la Moshi Vijijini ili wananchi wa ukanda wa milimani na kati wanufaike na umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Kibosho Magharibi, kuna kero kubwa ya kukosekana kwa huduma ya maji ya mifereji kumwagilia mazao yao ya kahawa, migomba na mbogamboga. Kwa ujumla, kuna ukosefu mkubwa wa maji ya kumwagilia. Shida hii imesababisha kuchelewesha maendeleo katika eneo la Vijiji vya Manushi na Umbwe lenye wakulima zaidi ya 500. Naiomba Serikali iharakishe ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Makeresho ambayo bado haijapata mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa kutoa fedha za ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Mandaka Mnono katika Kijiji cha Mandaka Mnono. Naiomba Serikali ikamilishe ujenzi wa skimu hii ili wananchi waanze kunufaika na mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa kutuma wataalamu na kutembelea eneo la ukanda wa tambarare huko Kata ya Arusha Chini. Kwa kuwa tayari tumesajili Chama cha Wananchi Wanaomwagilia Mazao katika eneo hili, naiomba Serikali itekeleze ahadi ya kujenga skimu mpya katika Kata ya Arusha Chini katika Mto Ronga itakayohusisha Vijiji vya Mikocheni na Chemchem ambako kuna takribani 2000 ha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba kilimo cha umwagiliaji kitatoa nafasi kwa wakulima kupata faida kubwa kwa sababu watalima zaidi ya msimu mmoja na kupata mavuno ya juu na mazao yenye ubora. Kumwagilia mashamba kutasaidia wakulima kupata mazao ya uhakika hata wakati wa ukame au vipindi vya mvua kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, ninaunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake makubwa ya kuwezesha na kuboresha kilimo. Kilimo ni mkombozi wa Watanzania walio wengi ambao ni wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Bashe, Waziri wa Kilimo, kweli yeye ni jembe. Mawazo yake na mipango yake imeleta mapinduzi makubwa kwenye kilimo. Mkoani Kagera bei ya kahawa imepaa kutoka shilingi 1,200/= hadi shilingi 5,000 kwa kilo. Haya ni mafanikio makubwa na manufaa makubwa kwa wakulima wa kahawa wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirika nawapongeza kwa kuendelea kukuza ushirika nchini. Mkoa wa Kagera kuna tatizo kubwa la benki ya wakulima iliyofungwa na Benki Kuu mwaka 2018, eti haina mtaji wa kutosha. Baada ya Benki Kuu kuongeza kiwango cha mtaji wanaotakiwa kuwa nao kama benki, wafanyakazi walifanya kazi kubwa ya kushawishi watu wajiunge na benki hii na wengine walishawishiwa waweke *fixed deposit*. Mwezi mmoja hadi miwili benki ikafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki ya *Kagera Farmers Cooperative Bank (KFCB)* ilifungwa ghafla. Waliokuwa wameweka amana zao, wanalia. Benki ilifungwa mwaka 2018. Walipewa shilingi milioni 1.5 mwaka huo na mwaka 2022 walilipwa 43% ya fedha zao. Wapo wastaafu ambao waliweka kiinua mgongo chao humo, hawakuwahi kukopa toka benki hii ianze. Wako wanalia, hawana mshahara na fedha za kiinua mgongo kimefungiwa benki. Kuna fedha za wakulima, vikundi vya akina mama, kuna fedha za Chama Kikuu cha Ushirika *(KCU)* na za wafanyakazi, wote wanalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliokuwa watumishi wa benki hii hawajalipwa haki zao za kiutumishi. Walilipwa nauli isiyozidi shilingi 150,000, leo ni miaka minane wanateseka. Wanazunguka ofisi

nyingi, lakini hawajapata suluhu. Waliniletea tatizo lao ili nilifikishe kwa Mheshimiwa Waziri, nikaenda Tume ya Ushirika, nimefika Wizara ya Kilimo, Waziri hakuwepo, nikaongea na Katibu Mkuu, nimeenda Benki Kuu Kitengo cha Ufilisi, kote sijaona dalili ya suluhu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kwa nini badala ya kuifilisi benki hii, hawakuiunganisha *KFCB* na mabenki mengine ili kulinda mitaji ya wakulima, wastaafu na wote waliokuwa wameweka fedha zao humo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri Bashe atutatulie hili tatizo. Ni mwiba mkubwa Mkoani Kagera. Watu walioathirika wanaumia na wanapiga simu kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, hawa wahanga ni lini watalipwa fedha zao? Ni lini waliokuwa watumishi wa *KFCB* watalipwa haki zao za kiutumishi wakati taratibu nyingine zinaendelea? Je, Serikali haiwezi kutafuta fedha mahali fulani, wakawalipa wahanga hawa ambao hawakuwa na hatia, tukaondoa huu mwiba?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri akija ku-*wind up* alizungumzie, awatie moyo, maana maumivu ni makali na wana hasira kali, *please*.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nachukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema. Pia, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uchapakazi wake na kuongeza bajeti kwenye sekta hii ya kilimo na jitihada zake za kuhakikisha anawanyanyua wanyonge. Naomba pia nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa uchapakazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Wizara mambo maiwili. Moja, mazao yote yanayouzwa kwa kilo sokoni, basi yanunuliwe kwa kilo hata shambani. Mfano, vitunguu na nyanya,

sokoni vinauzwa kwa kilo, ila kutoka kwa mkulima vinauzwa kwa tenga na lumbesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwenye kila ukanda lazima tuweke mkazo na kufufua mazao yetu ya kimkakati na ya kibiashara. Kwa mfano Kusini wameshajipambanua kwa korosho, parachichi na kahawa. Sisi Tanga tunalo zao la minazi, korosho na chungwa. Mazao haya yanafanya vizuri ukanda huo, lakini ni kama kwa sasa yanakufa. Tunaomba Wizara iweke jitihada kama ilivyoweka kwenye mkonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kuunga mkono hoja ya Wizara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii kuungana na Bunge lako Tukufu, kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo ya mwaka wa fedha 2025/2026. Mtu anayefanya vizuri anapaswa kupongezwa, anapaswa kutiwa moyo na kuungwa mkono hadharani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na Bunge zima, kwanza, kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Rais ni mwanamapinduzi wa uchumi wa kijani, tangu ameingia madarakani katika kipindi chake cha miaka minne, kila mmoja amekuwa shuhuda katika eneo lake namna ambavyo amefanya mabadiliko makubwa katika Kilimo. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu wa pili na muhimu sana kumpongeza ni Waziri, Mheshimiwa Hussein Bashe, ni Waziri mwenye maono, mbunifu na mwenye uthubutu. Amekuwa ni mtu ambaye anajaribu kufanya kila linalowezekana na yupo tayari kukosolewa ili mradi lile jambo liwe bora kwa faida ya wakulima hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nimejifunza sana kwake na moja ya jambo kubwa kwenye Wizara yetu alilolileta ni kufanya

kazi kama *teamwork* na ndiyo maana leo unaona haya yote ni matokeo ya kufanya kazi *as a teamwork*. Unavyomwona Waziri wangu, ndivyo alivyo Katibu Mkuu, ndivyo walivyo Naibu Makatibu Wakuu, ndivyo walivyo Wakurugenzi na Maafisa wote wa Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, hili niliona ni vizuri niliseme kwa sababu *teamwork* ndiyo ambayo imetufikisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, alituelekeza kuwekeza katika Kilimo cha umwagiliaji, wakati anaingia madarakani. Leo hii tunavyozungumza hapa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati anaingia madarakani, mwaka wa fedha 2020/2021 kulikuwa na miradi 13 tu ya umwagiliaji, leo tunavyozungumza kuna utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji 780 ndani ya miaka minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, alisema wazi kabisa kwamba anataka twende kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa sababu kubwa mbili; Kilimo kinahitaji maji, hakihitaji kutegemea mvua peke yake. Tuondoke kwenye kilimo cha bahati nasibu ili tuweze kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais, ameyaweka kwenye Wizara yetu na ndiyo maana alipandisha bajeti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Wakati anaingia ilikuwa shilingi bilioni 46 peke yake. Leo Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka wa fedha huu tunaokwenda kuumaliza ilipokea shilingi bilioni 403 ambazo zinaendeleza uwekezaji kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, wakati Mheshimiwa Rais, anaingia madarakani eneo la hekta ya umwagiliaji nchini lilikuwa chini ya hekta 700,000 nchi nzima. Hiyo ni miaka 60 tangu tumepata uhuru. Mheshimiwa Dkt. Samia, sasa hivi anatekeleza miradi yenye ukubwa wa hekta 534,000 ndani ya miaka minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaona kabisa kwamba lengo lake ni kuhakikisha kilimo kinakuwa cha uhakika, tulime *throughout the year* ili tulete tija kwa wakulima wetu. Mheshimiwa Rais, ametuelekeza vilevile kwamba tununue magari kwa ajili ya

kuchimba visima ili tuweze kumsaidia mkulima mdogo mdogo kule chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaona juzi tulikuwa tunapokea magari saba ya umwagiliaji ya kwanza yameshafika, mengine 11 yapo baharini na bodi zetu tumeshazielekeza na zenyewe zitakuwa zinanunua magari ili tuweze kuwafikia wakulima kwenye kila mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya oparesheni tunayokwenda kuifanya hapo mbele, haya magari sisi hatutagawa kwenye Mkoa, yaani tunaondoka na gari zetu zote, tukifika kama ni Mkoa wa Songwe magari yanafanya kazi yanamaliza pale, yanahamia mkoa mwingine. Tunataka kuona tija katika kilimo kama Mheshimiwa Rais, alivyotuelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alituelekeza baada ya kuona changamoto kubwa katika bei za mazao hapa nchini, akasema sasa tubadilishe mifumo, twende katika mifumo ya kidijiti ili mkulima apate bei rafiki ambayo inaweza kumsaidia. Leo hii unaweza kuona watu wamekuwa wakizungumza hapa na nitatolea mfano baadhi ya mazao. Kwa mfano kahawa kabla ya mfumo wa kidijiti wa kutumia *TMX* Kahawa ilikuwa chini ya shilingi 1,000, au shilingi 1,200. Leo Kahawa imefika shilingi 6,000 kwa kilo, yote haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye kokoa, bei ilikuwa chini ya shilingi 8,000 wakati Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, anaingia madarakani, leo kokoa tunauza kati ya shilingi 24,000 mpaka shilingi 34,000 kwa kilo moja. Sasa fikiri haya ni mabadiliko madogo tu kwamba sasa tunabadilisha mifumo, kilimo cha mazoea ambacho watu walikuwa wanakiishi miaka mingi. Leo hayo ndiyo matokeo ya uwekezaji na maelekezo ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mbaazi wamezungumza Wabunge. Mbaazi ilikuwa inauzwa kilo mpaka shilingi 100, leo kwenye mbaazi tumefika shilingi 3,000. Kwenye korosho tulikuwa

chini ya shilingi 2,000, leo korosho tumefika mpaka shilingi 4,200. Sasa haya yote yanayofanyika ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, tubadilishe mifumo ili tupate bei nzuri na masoko ya uhakika kwa wakulima wetu. Safari bado inaendelea, kazi bado inafanyika, na ndiyo maana mnaona haya yote yanatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, hata ukiangalia kwenye mauzo ya mazao nje ya nchi, wakati Rais Mheshimiwa Dkt. Samia anaingia madarakani, mauzo ya nchi mwaka 2021 yalikuwa dola za Kimarekani bilioni 1.2, uki-*convert* kwa wakati ule ilikuwa kama shilingi trilioni tatu. Leo katika mwaka wa fedha 2024/2025 mauzo ya nje yamefikia wastani wa Dola bilioni 3.54 za Kimarekani, sawasawa uki-*convert* kwa leo ni zaidi ya shilingi trilioni 9.6 fedha za kigeni zinazotokana na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote ni mambo ambayo Mheshimiwa Rais, ameelekeza, utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, na ninyi Wabunge mmeona matokeo ambayo yanaendelea kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alituelekeza vilevile tuanze kutoa ruzuku kwenye pembejeo za kilimo ili tuweze kumsaidia mkulima mdogo kuongeza tija na uzalishaji. Sasa matokeo yake leo kwenye hizo tija ambazo tumeziongeza kwa kutoa ruzuku kwenye pembejeo kwa maana ya mbolea, mbegu na viuatilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati anaingia madarakani mwaka 2020/2021 mahindi tulikuwa tunazalisha tani milioni 6.4 kwa mwaka. Leo katika mwaka huu uliokwisha tumezalisha tani milioni 12.2, mwaka wa fedha 2023/2024, hayo ni matokeo ya kuongeza ruzuku kwenye pembejeo. Ndani ya miaka minne tume-*double* na leo tumekuwa nchi ya pili Afrika kwa uzalishaji wa mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaona kabisa kwamba kumbe kilimo kinahitaji uwekezaji. Kilimo kinahitaji uthubutu, kilimo kinahitaji watu wenye maono ndiyo maana unaweza kuona tu mambo yanatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo kwenye korosho kupeleka tu viuatilifu, ruzuku ya viuatilifu kwenye korosho; uzalishaji umetoka tani 210,000. Leo tunavyozungumza, tumefikia tani 528,000 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.598. Fedha hizo zimekwenda kwa mkulima wa korosho. Haya yote ni utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ambao leo Watanzania wanaona kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, Mheshimiwa Rais, vilevile alituelekeza kwamba, Benki ya Ushirika ambayo ndiyo ingeweza kuwasaidia wakulima moja kwa moja na wanaushirika, ambayo imekuwa ikielezwa muda mrefu kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, akasema nataka kabla hatujakwenda kwenye Uchaguzi Mkuu, Benki hii iwe imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninyi wote ni mashahidi, tarehe 08 mwezi wa Nne, mwaka huu Rais mwenyewe amezindua Benki ya Ushirika, ambayo inakwenda kuleta mabadiliko makubwa kwa wanaushirika na wakulima kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaona kabisa kwamba kuna dhamira ya dhati na ya kweli katika sekta ya kilimo ambayo inatokana na mwanamapinduzi wa ukweli ambaye ni Mheshimiwa Rais, ameweka uwekezaji mkubwa sana katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tutaendelea tu kuwaomba Bunge Tukufu, mtupitishie hii bajeti ili twende tukatekeleze yale ambayo tumeyaanza, yapo katikati, tuyamalize yale ambayo tunakwenda kuyaanza upya, lakini yote uwekezaji huu na niwaambie kabisa kabla ya mwaka 2030 matokeo yake yatakuwa ni makubwa sana na watu wataanza kuona sasa kweli kilimo ndiyo *game changer* wa uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tumepewa maelekezo na Mheshimiwa Rais, sisi Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI tuhakikishe tunakuja, tuna *model* yetu inaitwa *Morogoro model*.

Sasa tutapeleka kilimo kwa wanafunzi wa shule za msingi na wanafunzi wa sekondari katika yale mazao ya kibiashara kama karafuu ama kokoa. Yaani mwanafunzi atapewa mche, tutagawa bure kwa kupitia taasisi yetu *COPRA* ndiyo wamepewa hilo jukumu. Atapewa mche kama ni wa karafuu, atakuwa anamwagilia, unapanda pale nyumbani kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, mche mmoja wa karafuu ukikua, unampa mkulima wastani wa shilingi milioni moja mpaka milioni tatu kwa mche mmoja. Ukiwa na miche 10, maana yake una wastani wa kati ya shilingi milioni 10 mpaka shilingi milioni 30 unapokuwa umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maana yake ni nini? Utamsaidia mwanafunzi yule aweze kujimudu mpaka anapokuwa mtu mzima. Kwa hiyo, hayo ndiyo malengo yetu na ndiyo *vision* ambayo tuliyonayo sasa hivi kuhakikisha tunakwenda kubadilisha kila kitu katika Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana leo kila mmoja hapa anaweza akazungumza na akaona ukweli kabisa kwamba hiki kinachofanyika ni kwamba tulijaribu kuangalia wapi kwenye programu za kilimo zilizofeli, kuanzia "Kilimo ni Uti wa Mgongo", "Kilimo ni Siasa", "Kilimo ni Kujitegemea", na "Kilimo Kwanza." Yote yale sisi tuliangalia ndiyo maana tukaja tukasema hapana, sasa tuna-*change direction totally,* na hii *direction* tunayoibadilisha ndiyo pekee inayoweza kubadilisha maisha ya Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kabla ya mwaka 2030 kilimo kitatoa malighafi kwa 100% kwenye viwanda vyetu hapa nchini. Nchi zote ambazo zimeendelea za viwanda, nchi za viwanda hawakuanza tu kutengeneza viwanda bila ya kuwa na malighafi, waliwekeza kwenye kilimo, wakapata sana kilimo, wakagundua kwamba *no*, sasa tunataka tutoke kwenye kilimo kwa kuongeza thamani, ndiyo wakaleta viwanda. Ndio maana ukienda kusoma *Industrial Revolution* ilitokana na *green revolution* katika *Europe* wakati ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mtu yeyote hawezi kutuambia kwamba tusiwekeze kwenye kilimo kwa maana ya mashamba makubwa, tusiwekeze katika Jenga Kesho Iliyo Bora *(BBT)* katika ngazi ya halmashauri, eti kwa sababu tunachukua maeneo makubwa. Tutafanya hivyo kwa sababu ndiyo njia sahihi na pekee ya kumkomboa Mtanzania wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba mtu yeyote ambaye anasema atamnyima kura Mheshimiwa Rais, kwa kutenda wema huu, basi ninaamini atakuwa hana anachokiona katika maisha yake. Maana yake mtu huyo hata ungemfanyia nini, hawezi kutoa kura, lakini hiki kilichofanyika kimekusudia kubadilisha maisha ya mwananchi mmoja mmoja wa kawaida hususan Mkulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kusema maneno hayo machache, nami nikushukuru sana kwa kuongoza Bunge vizuri na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde hongera sana na maamuzi yako ya kuhamia upande wenye manufaa makubwa ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Bashe, mtoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Pili, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema iliyotuwezesha kufika hapa leo, kutekeleza kazi hii na kumalizia jukumu lililo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa *support* anayotupa katika kutimiza majukumu ambayo ametugawia sisi kama wasaidizi wake. Vilevile, niwashukuru sana Naibu Waziri wangu ndugu yangu Mheshimiwa Silinde, kwa kuchangia na kujibu baadhi ya hoja na kutoa *clarification.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kwa dhati kabisa kwa *support* anayonipa mimi Waziri wake na ushirikiano na mahusiano ambayo tumekuwa tukijenga. Namshukuru Katibu Mkuu, nawashukuru wataalamu wote wa Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitumie nafasi hii kusema kwamba kwanza pongezi zinazotolewa kwa Wizara ya Kilimo anayestahili wa kwanza ni Mheshimiwa Rais, kwa sababu mimi kama Waziri, na bahati nzuri Waziri wa Fedha yupo hapa, anafahamu kwamba kukiwa na changamoto yoyote ni kwa namna gani huwa anakuwa *summoned* Waziri wa Fedha kwa ajili ya kuhakikisha shughuli za kilimo zinakwenda hasa zinazohusiana na matatizo ya wakulima wadogo. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hizi pongezi nataka niseme tu kwamba Watumishi wa Wizara ya Kilimo wanastahili hizi pongezi, ni za kwao. Wanafanya sana kazi nami mbele ya Bunge lako Tukufu. Nawashukuru sana kwa *support* ya ushauri wanayonipatia kama Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwa uchache, mara nyingine huwa wanakuwa wakali sana kwangu kama Waziri pale ambapo kuna mambo ya kitalaam, mimi na wao tunatofautiana, mahali ambapo nataka matokeo yatokee kesho, wenyewe huwa wanakuwa wakali sana. Nami nataka niwatie moyo, wawe na haki ya kunikosoa mimi kama Waziri ndani ya *boardroom,* kwa sababu ni wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge. Katika Bunge hili nimekuwa Naibu Waziri chini ya kaka yangu Mheshimiwa Hasunga, yule pale. Nataka niseme tulikuwa na bajeti ya shilingi bilioni 270 hivi, au shilingi bilioni 280, tulikuwa tunapata *disbursement* asilimia 30 na yeye yule pale shahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunakuja hapa *pressure* juu, tunalalamika tuna maumivu, hakuna fedha, lakini nimefanya kazi chini ya Mheshimiwa Prof. Mkenda, tukawa na shilingi bilioni 297, tukasema mimi na Mheshimiwa Prof. Mkenda hatuna hela.

Mheshimiwa Naibu Spika, hela *allocation* iliyoko ni shilingi bilioni 290 *something,* tupeleke wapi fedha? Tukasema tuwekeze kwenye utafiti tu angalau tutafsiriwe kwenye suala la utafiti na ugani. Ndiyo dhana ya kuanza kufanya *reform* ya *research* ilikoanzia pale. Hatukuwa na fedha, *disbursement* ilikuwa isiyozidi 60%, au 70% ya shilingi bilioni 290. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaelewa sana Waheshimiwa Wabunge kwa hoja ya kwamba kweli hakujawa na *disbursement* inayotakiwa ya *hundred percent.* Ni matamanio ya kila mtu, lakini nataka niwatie moyo *six hundred billion shilling* tuliyoipokea mpaka Aprili na tumeendelea kuwa na *engagement* na mwenzangu Waziri wa Fedha tunatarajia kuendelea kupata fedha ndani ya mwezi huu wa Tano, tutapata fedha mwezi wa Sita. Ninaamini kwamba tutakapoumaliza mwaka huu wa fedha, sehemu kubwa ya matarajio yetu yatakuwa yamepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu mkubwa ni kutafuta fedha nje ya mfumo rasmi wa kawaida. Namshukuru Waziri wa Fedha, namshukuru ndugu yangu Waziri wa Mipango, wametukubalia kutengeneza taratibu za kutafuta fedha katika njia ambazo siyo za kawaida kutegemea kapu moja tu la Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tumeanza kupata fedha kutoka *World Bank,* na juzi ametusaidia kutupitishia fedha kwa ajili ya kupewa kutoka *World Bank,* zaidi ya dola milioni 54 ambazo zitaenda kwenye mabwawa *hundred percent,* hizi fedha zote zitaenda kwenye mabwawa. Ametuidhinishia, tumepata fedha kutoka *World Bank* dola milioni 300 za *P4R,* tutakazoanza kuzitumia katika sekta ya kilimo. Hii ni njia mpya ya kutafuta fedha katika mfumo ambao siyo wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi wakati Mheshimiwa Rais anazindua Benki ya Ushirika, tumepata fedha kutoka *African Development* dola milioni 120 na kidogo ya Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo. Hizi ni fedha ambazo tunaenda kuzitumia kwenye Programu ya *BBT* na *agricultural financing.* Tumepata fedha vilevile kutoka *IFAD* zaidi ya dola milioni 40. Hizi fedha

zitaanza kuonekena matumizi yake kuanzia mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haikuwa kawaida, Mheshimiwa Hasunga, yupo hapa na ninyi Wabunge mmekuwa mfano mliokuwepo hapa kwa muda mrefu. Haikuwa kawaida Wizara ya Kilimo kuidhinishiwa kupata fedha kwa mfumo wa *P4R* ambao unatumika katika sekta ya elimu. Haikuwa kawaida. Nasi ndio tutakuwa moja ya nchi ya Afrika ambayo inatumia *P4R modal* kwenye *agriculture*. Kwa hiyo, namshukuru sana Waziri wa Fedha, ni matamanio yetu sote tupate *hundred percent*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri pale Wizara ya Fedha nina kabechi kwa *PST*, kwa Kamishna wa Bajeti, kwa Kamishna wa Madeni na kwa Waziri mwenyewe naenda bila *appointment,* nitakaa kwenye foleni kuhakikisha kwamba tunapa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatieni moyo, tutapata fedha za sekta ya kilimo kwa sababu nao wameona *remittance* za *agricultural export,* wameona namna gani uchumi wetu umekuwa imara, umekuwa *stable* wakati tuna *Covid* hii nchi, wakati kuna matatizo ya dunia. Wengine wakiingia kwenye matatizo, sisi bado uchumi wetu ulikuwa imara, ni kwa sababu ya uimara wa sekta ya kilimo. Kwa hiyo, naomba niwatie moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zimesemwa hoja nyingi na Waheshimiwa Wabunge, nami nitajaribu kuzijibu baadhi. Katika hizi hoja, moja ya hoja ambayo imeongelewa na ninaomba tu niseme kwa ufupi, Mheshimiwa Asenga, kuhusu *issue* ya Wakulima wa Kilombero, nataka tu niwahakikishie, tulikaa mimi na yeye, niliambie Bunge hili Tukufu akiwepo Mheshimiwa Londo, *AMCOS* zote za Bonde, Kiwanda cha Kilombero. Tulikubaliana tunaita *gentlemen agreement,* tu-*form* timu ya wataalam ambayo itaongozwa na Bodi ya Sukari, Wizara ya Kilimo, *TBS,* Wakulima na Kiwanda. Timu tumeshaunda na inaendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusubiri matokeo ya timu, tusikihukumu kiwanda kabla ya matokeo ya timu. Nikuhakikishie

wewe na wakulima wote, maslahi ya wakulima yatalindwa bila uwoga wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wakulima waliokatiwa mazao yao ya kakao niombe tu, tupewe fursa, nitakaa na wenzangu wa Wizara ya Maliasili, tutakaa na Serikali ya Mkoa tutapata *solution* kwa tatizo hili tuweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee, zao la pamba. Amesema Mheshimiwa Boni, amesema kaka yangu Mbunge wa Sengerema na wameongea wengine. Mimi ninatoka kwenye pamba na tumbaku. Cha kwanza, niongelee hapa hapa, niseme ukweli, kama sisi wanasiasa tunaotoka kwenye ukanda wa pamba, na viongozi tunaotoka kwenye ukanda wa pamba hatutakubali kubadilika na kuheshimu sayansi kwenye pamba na kuigeuza pamba kuwa zao la siasa, hatutaondoka kwenye umasikini wa wakulima wa pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya msingi ya pamba; moja, ni kukataa sayansi. Tunaambiwa tusichanganye mazao ndani ya pamba. Wote tunafahamu kule Usukumani tunakubaliana kwenye vikao vya ndani, tukienda kwenye mikutano ya hadhara, kuna yale maneno, "kwani wewe shamba la kwako? Mwache tu achanganye pamba na mahindi." Hawezi kupata tija. Hoja ya pamba siyo bei tu, hoja ya pamba ni tija. Nami nataka niwape takwimu ili tukubaliane sote kubadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie, waulize ndugu zangu wa tumbaku wa Tabora, tulikamatana na nikawaambia wanasiasa wenzangu wakae pembeni. Leo tumbaku imenyooka, kila mmoja anashangilia. Sasa zao lililobaki kwenye nchi hii ni haya mawili. Mamlaka yangu kama Waziri wa Kilimo yanaisha baada ya kuapishwa mwingine. Nina pamba na chai, na nikimaliza hapa nakuja kwenye pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivi, naomba tusikilizane. Wakati sisi leo bei yetu ni shilingi 1,150, pamba hailimwi Tanzania peke yake, Zambia wanalima. Mkulima wa Zambia anapata shilingi

800, mkulima wa Malawi anapata shilingi 864, mkulima wa Msumbiji anapata shilingi 918, tumezi-*convert* kwenye shilingi, Mkulima wa Zimbabwe anapata shilingi 800, na hawa wote hawapati ruzuku ya aina yoyote kutoka Serikali zao. Kwa nini? Hakuna kelele, wanapata kwenye ekari moja zaidi ya kilo 1,500 mpaka kilo 2,000. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaenda kule tunatuma watalaam, na wanasayansi tunasema kwamba *plant population* kwenye ekari ifike angalau miche 44,000 mpaka 50,000. Tunaenda kufanya mikutano ya hadhara tusizuiliwe, wewe weka na mahindi ukitaka. *Wallah*, nitawaweka ndani watu. Nataka niwe mkweli. Kwenye hili, nataka niwe mkweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Brazil mkulima mmoja kwenye hekta anapata kilo 6,500. Mwaka 2024 nilivyotangaza tunaanza Programu ya *BBT* kwenye kilimo cha pamba na tunapeleka matrekta tumewalimia wakulima wa pamba kwa shilingi 35,000/= kwa ekari, tumewapelekea mbegu na dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu sasa hivi wapo Mahakamani. Mbegu tunazo, wapelekewa, wanazichukua kwenda kuzipeleka kwenye *ginnery* kuzikamua mafuta. Wanaenda kuzikamua mafuta, ukimkamata unapigiwa simu na kila mtu unayemjua. Lazima tubadilike watu wa pamba kama tunataka kubadilika. Nimewaambia wataalam waweke hapo kwenye *screen* mwone. Mwaka 2019/2020, 2018/2019 tulifika tani 340,000 ya pamba. Ilifia humu ndani, Waziri wangu Mheshimiwa Hasunga yule pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa Manaibu Waziri wawili, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, wakati huo Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru, ameita vikao *BoT,* ameita wapi, Ofisi Ndogo ya Lumumba, nani waliiua. Sisi wanasiasa! Tukamdanganya Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli, tukamdanganya Waziri Mkuu, Waziri Mkuu akaenda akaita vikao pale Mwanza mpaka saa saba usiku. Tubadilikeni wanasiasa tulioko kwenye ukanda wa pamba. Huu ndiyo ukweli mchungu, lazima tubadilike, tukubali kilimo ni sayansi siyo magadala. Hili ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepeleka *BBT,* kelele! Tumbaku leo inashangiliwa, ni *contract farming.* Tunachokitafuta leo, tuna mkulima amepewa trekta na Mheshimiwa Rais amefika kilo 2,200 hapa hapa Tanzania na yupo Mkoa wa Shinyanga. Kwa nini, ametumia mbolea? Amefuata utaratibu wa kisayansi kapanda miche 44,000 kwenye shamba lake, kapata kilo 2,200.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila tukiongelea kichaka chetu, wakulima wa pamba wanaibiwa, anayetaka kuniletea mnunuzi akatayenunua pamba shilingi 3,000/= nitampa mkataba yeye pekee yake aje anunue, haipo. Nataka niwaambieni kwa nini haipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya dunia leo ni senti 64 dola, *CIF price*. Mwaka 2024 wakati sisi duniani iko senti 75 bei yetu elekezi ilikuwa shilingi 1,200 ikafika mpaka shilingi 1,400 na tulitumia ushirika kuipandisha hii bei kufika shilingi 1,400. Mwaka 2023 ilifika shilingi 2,000; pamba bei ya dunia ilikuwa dola 1.16.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, cha kwanza tufahamu kwamba bei ni *function* ya *supply and demand*, huo ndio ukweli. Tunachotakiwa sisi kupambana nacho ni tija na kuongeza thamani. Serikali inachukua hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeleta ruzuku ya dawa, mbegu, matrekta kwenye pamba tumepeleka ugani. Mwaka huu 2025 tutatoa tani 149,000, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutafika tani 400,000, au 450,000 za pamba. Nawaomba tusiende kuivuruga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya nini kama Serikali? Tunaenda hatua ya pili, tunafanya *value addition*. Tumeongea na Wizara ya Afya, tumekubaliana tunajenga *industrial park* ya kwanza Simiyu. Tumeshakubalina kutakuwa na ekari 1,000, tutaanza kujenga pale kama tulivyoanza kujenga Malanje, tutatoa ruzuku ya umeme, tutapeleka maji, na Serikali itaanza kujenga *infrastructure* ya maghala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo linaongelewa sana kuhusu wawekezaji. Hawa wawekezaji ni akina nani? Lazima uchumi huu ushikiliwe na wenye nchi, ndiyo Taifa hili litakuwa salama. Tukifanya makosa ya kuhakikisha uchumi wote unashikiliwa na *foreigners,* hautamsaidia Mtanzania wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajenga *industrial park* pale Simiyu ya kwanza ya pamba. Tutazuia *importation* ya vifaatiba vinavyotokana na pamba na Serikali itaweka fedha kwenye hili eneo. Tutazuia *importation* ya kamba za kufungia tumbaku. Tunatumia zaidi ya dola milioni 19 kuingiza hivi vifaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishaanza kuongeza thamani, Mwalimu Nyerere alijenga *ginnery* Igunga, akajenga kiwanda cha nyuzi Tabora, tumerudi wenyewe nyuma kwa sababu tuliamua *as a policy* kufanya *wrong privatization*, *that is the truth.* Huo ndio ukweli, dunia imetufundisha, tunarudi kwenye misingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunasema magodauni ya *SHIRECU* yaliyopo pale bandari na magodauni ya Bodi ya Pamba yafanyiwe uthamani? Ipatikane pesa, hiyo pesa ndiyo tutaenda kufanya uwekezaji, na pale tunaenda kujenga kiwanda cha kuchanganya mbolea. Nyerere alijenga Kiwanda cha Kuchanganya Mbolea Tanga akaweka bomba kutoka bandarini kuingia kiwandani, tulikiuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaenda kuwekeza kwenye Bandari ya Dar es Salaam kwa kutumia maghala yaliyokuwa yanamilikiwa na Bodi ya Pamba na maghala yaliyokuwa yanamilikiwa na *SHIRECU* na niwahakikishie, wana Ushirika wa *SHIRECU,* na *SHIRECU* inapata bilioni moja kwa mwezi au milioni 900.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, kwa mujibu wa Kanuni, ninaongeza muda kidogo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *SHIRECU* inapata karibu bilioni moja. Hizi fedha wanazitumia kwa matumizi ya kawaida tu, hawawekezi popote, zinaishia vikao, mikutano, posho. Tunafanya nini? Kweli mnataka niiache *SHIRECU* namna hiyo? *It will be very wrong for this country*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba wakulima wa pamba tutahakikisha tunawasaidia waongeze tija na vipato vyao viweze kuongezeka. Huo ndiyo mwelekeo wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limeongelewa sana na Wabunge ni eneo la mitaji kwenye sekta ya kilimo *(agricultural financing)*. Mheshimiwa Mpakate, amesema kuhusu akaunti za wakulima zinakuwa *dormant* baada ya muda mfupi. Niseme tu kitu kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, namshukuru Waziri wa Mipango na timu nzima ya *Planning Commission,* tumekubaliana na ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais tuunde timu ya pamoja kwa ajili ya kutengeneza *technical team* kwa ajili ya kuandaa *Agricultural Financing Policy*. Lazima tuwe tuna sera ya ukopeshaji kwenye kilimo. Kilimo hakikopeshwi kama kuuza vitu vingine, ni tofauti kabisa. Kwa hiyo, sera itakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Benki yetu ya Ushirika tunachukua hatua gani? Tunashirikiana na *Commercial Bank*, nami niwashukuru sana. Namshukuru Majid, Mwenyekiti wa Tume ya Ushirika. Namshukuru sana, nawashukuru *NMB*, nashukuru benki zote za *Commercial Bank*. Leo hii wanatoa mikopo na mikopo hii wanayotoa kwenye *input* haina *guarantee* yoyote, ni kuaminiana na ni makaratasi tu, na ninawashukuru sana kwa hatua hii, tumefika shilingi trilioni nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachukua hatua gani? Tutashirikiana Tanzania *Agricultural Development Bank*, *Agricultural Trust Input (AGITF),* tutashirikiana na Benki yetu ya Ushirika. Tutaanzisha *window* ndani ya Benki ya Ushirika itakayokuwa na mambo matatu. Moja, itakuwa ina *guarantee*

*scheme* kwa ajili ya wakulima wadogo ambayo watakopeshwa kwa kiwango kisichozidi asilimia saba, lakini vilevile itakuwa na *equity fund* na itakuwa na *direct land. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali kupitia *AGITF* tunatafuta fedha. Mfano kama sasa hivi tunawapelekea shilingi bilioni 17 *Agricorp Bank* ambayo inaenda kama *guarantee* ili wao watoe mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 51 kwa riba isiyozidi asilimia saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile inaenda kama dhamana, hatutaki kui-*distort bank* kufanya *commercial function* yake, lakini tunaanzisha dirisha maalum ndani ya Benki ya Ushirika ili iweze kuwahudumia wakulima kwa riba ndogo na nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana na *African Development Bank* kwenye fedha alizotuidhinishia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, nami niseme hapa, na Waziri wa Fedha anasikia, kama *AFDB* hawatakubali kufuata utaratibu wetu, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu huo mkopo tusiuchukue kwa sababu hawatupatii msaada, wanatupatia mkopo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *agricultural financing* fedha yake yote itaenda *AGITF* na *Coop Bank*, itaenda kuwekwa kama *guarantee* na *equity fund* dola milioni 35. Hizi fedha zote zitaenda kuwakopesha wakulima kwa kiwango kisichozidi asilimia saba. Tumefungua *window*, tutaziruhusu *commercial bank* zinazotaka ku-*access* hizo fedha, tutawapa ili waweze kuwakopesha kwa masharti tunayotaka sisi, siyo masharti wanayoyataka wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili, najua litaleta mjadala sana kwenye sekta ya fedha kama Waziri, *I will be ready to face that discussion,* lazima mfumo wa ukopeshaji ubadilike katika sekta ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilikuwa ninataka niseme kuhusu *BBT*, ninawashukuruni sana, *BBT is a program,* ita-*evolve,* itabadilika. Nilikuja na wazo la *block farm,* mmeshauri sana, sasa tumeenda kwenye Halmashauri, tumeenda kwa

wakulima wadogo, tutaendelea kubadilika. *BBT* maana yake nini? Nia na madhumuni ni kuhakikisha kizazi kijacho cha nchi hii kinamiliki mali yake, kinamiliki ardhi yake, kinamiliki uchumi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilitaka niseme kuhusu umwagiliaji. Kama nchi hatutaamua kuwekeza kwenye eneo la umwagiliaji kwa nguvu, kwa muda mrefu hatutawaondoa maskini walioko kwenye sekta ya kilimo kwenye umaskini wao. Hili ni muhimu sana na hapa nimeorodhesha miradi pamoja na ile 780 ambayo tunaendelea kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wanasema, kwa nini usifanye kidogo ili matokeo yaonekane? Hebu naomba kuuliza, hiyo kidogo nianzie wapi? Yaani ni wapi wakubali kusubiri wakati kidogo inakuja? Nadhani tusiogope kuvamia hii bahari kubwa. Tuogelee kama tuna-*plan,* tutafika mwisho na tutatoka mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumetangaza *feasibility study* na *detail design* ya mradi wa Lake Tanganyika na Lake Victoria. Huu mradi utakuwa ni wa jumla ya hekta milioni tatu, na ninataka niwaambie nendeni mkasome kuna mradi unaitwa *The Largest African Irrigation Scheme,* inaitwa *Gezira Scheme*. Ipo wapi? Ipo Sudan, imeanza kujengwa 1904, ina hekari milioni tatu. Wameijenga kwa zaidi ya miaka 100. *The largest Irrigation Scheme*, inaitwa Gezira. Tusiogope kuwekeza kwenye umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nimeorodhesha mabonde yote na maeneo yana jumla ya hekta 5,383,850 na yote haya yanaenda kufanyiwa *feasibility study* na *detail design* na yataanza kujengwa ili yasiishie njiani. Niwaambie tu wote mjue, kila bonde tumeanza heka 500, heka 1,000, heka 2,000, yatamalizwa tu, hata sisi wote tusipokuwepo humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere alifikiria kizazi kinachokuja, hakufikiria kizazi chake. Tuombe kwa Mwenyezi Mungu, tuache kufikiria leo, tufikirie wanaokuja kwa sababu *we*

*are surviving,* kuna wengine walifikiria *on our behalf,* hii ndiyo njia pekee ambayo inaweza kutuondoa kwenye matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mabonde yote Mheshimiwa Rais kaidhinisha, tuendelee. *Irrigation* ya Victoria kaidhinisha tumeshaanza, tumeshatangaza *feasibility study* na *detail design,* tumeanza kujenga kule kwa Prof. Muhongo, tumeanza kujenga Ngono. Ngono waliofanya *visibility study* ya kwanza, wamekufa, hawapo. Tusiogope, *this is the right direction,* tuna Mheshimiwa Rais, tunaenda kwenye uchaguzi mwezi wa Oktoba kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu atashinda, atarudi ana *commitment* na wakulima. *We have this advantage,* tuitumie kwa ajili ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeamua kununua mbolea kwenye viwanda vya ndani, tani 200,000 za mbolea. Tunaanza mwaka kesho, zitakuwa ni *targeted subsidy program*, haitaathiri ile ruzuku. Wote wanaofikiri kwamba tunatoa ruzuku kwa bahati mbaya*, it is well calculated.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ruzuku ya mbolea ni well *calculated*, ruzuku ya mbegu tuliyoianza ambayo tumeianza mwaka huu imepata changamoto, na ninyi mnakumbuka tulivyoanza ruzuku ya mbolea ilikuwa ina changamoto. Leo *we are all happy*. ruzuku ya mbegu, na nimewaambia juzi makampuni sitasita kumfutia leseni hata awe kampuni ya Kimataifa, atafuata utaratibu tunaotaka sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ruzuku ya matrekta tunaanza, mwaka huu Mheshimiwa Rais katuidhinishia kuanzia *mechanization center* 1,000, trekta 10,000. Kwa Wilaya za uzalishaji tuna uwezo wa kupeleka kila Wilaya zaidi ya trekta 50, kila Wilaya zitaenda kulima kwa ruzuku, siyo kwa bei ya soko, ni kwa bei ya ruzuku na hii inaanza mwaka huu. Siyo bahati mbaya, *it is* well *calculated*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaanza kuchimba visima kwa ruzuku kwa sababu sisi tutapata fedha kwenye mazao yatakayotoka. Hatuhitaji kupata fedha kuliko kwenye uchimbaji

wa kisima. Wakulima wadogo, maskini watachimbiwa bure kwa sababu ndiyo wameibeba hii nchi kuifikisha hapa ilipo. Tutaujenga ushirika kwa nguvu, wezi tutawafunga, ushirika hatuufuti, tutaendelea kuujenga pole pole ili uweze kuushikilia uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, nami niseme tu, Bunge hili litaenda kwenye uchaguzi likiwa limeacha msingi imara kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye zao la chai, nataka tu niseme, wataalam wa Wizara ya Sheria wa Kilimo wanamwandikia *AG*, tunampelekea *AG*, tutatumia sheria za nchi hii kuyachukua yale mashamba kwa maslahi ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi, nami nawaambia hatuwezi *DN* na wenzake kwa sababu tu wanaitwa wawekezaji kushikilia nchi hii kuwa mateka *for a very long time*. Tumewapa *option* ya kuyachukua yale mashamba, Mheshimiwa Rais kaagiza, ongea nao uyanunue yale mashamba, imekuwa shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni zote zilizomilikishwa, ninawashukuru *WATCO* nataka tu niwaambie watu wa Rungwe, Mwenyekiti wa Bodi ya Chai yule pale juu, Majid, nimeshampa maelekezo. *WATCO* wamekubali, tunakinunua kile kiwanda, tunakikabidhi kwa wakulima wadogo, watamilikishwa viwanda vile. Tumeshanunua viwanda viwili, vinakuja kwa ajili ya kufungwa kwa wakulima wa Rungwe na Kilolo kwa ajili ya kuchakata chai. Chai tuna changamoto, lakini tutazimaliza kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa dhati na kuwapa *commitment* ya Wizara ya Kilimo, tutaendelea kufanya kila ambacho kimo ndani ya uwezo wetu kuondoa matatizo yanayoikabili sekta ya kilimo. Hayataisha leo, yataendelea kuwepo, tutaendelea kukabiliana nayo kwa sababu tuna Jemedari Mheshimiwa Rais mwenye nia thabiti ya kuwalinda wakulima nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…..............................Sh. 6,758,597,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye *guillotine*. *(Makofi)*

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1002 – *Finance and Account Unit*...............Sh. 2,157,122,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*..................Sh. 5,369,828,000
Kifungu 1004 – *Agriculture Training Institute*...........Sh. 44,953,960,000
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*.................................Sh. 723,080,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*.....Sh. 1,015,663,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*.........................................................Sh. 690,757,000
Kifungu1008 – *Legal Service Unit*...............................Sh. 808,068,000

Kifungu 1009 – *Management Information System Unit*.......................................................Sh. 815,913,000
Kifungu 1010 – *Environment Management Unit*..................................................Sh.  65,846,569,000
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*.......Sh. 1,154,644,000
Kifungu 2001 – *Crop Development*.........................Sh. 45,468,556,000
Kifungu 2002 – *Agricultural Mechanization*..............Sh. 7,708,993,000
Kifungu 2003 – *Agriculture Land Use Planning and Management*…..........................Sh. 1,027,172,000
Kifungu 2004 – *Plant Breeders' Unit*.........................Sh. 54,647,673,000
Kifungu 5001 – *National Food Security*..................Sh. 135,983,889,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kifungu1001 – *Administration and Human Resources Management*.....................................Sh. 3,400,171,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…….........Sh.402, 852,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation*...................................Sh. 725,782,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*….Sh. 175,273,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*........Sh. 544,049,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*……………………..Sh. 261,943,500
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit*……………..…………..Sh. 125,650,000
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit*…….………………. Sh. 158,920,000
Kifungu 1009 – *Environmental and Social Management Unit*……………………………………..Sh. 5,924,560,500
Kifungu 2001 – *Design and Research Division*…………………………………Sh. 52,937,526,500
Kifungu 2002 – *Irrigation Infrastructure Development*………………………….Sh. 2,726,341,000
Kifungu 2004 – *Operations Division*……………….....Sh. 11,671,139,000
Kifungu 2005 – *Compliance and Quality Assurance Section*...........................................Sh. 73,416,447,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika**

Kifungu1001 – *Administration and Human Resources Management*…..................................Sh. 2,025,827,427
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.................Sh. 362,429,130
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*………………..............................Sh. 437,545,130
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*….Sh. 303,664,310
Kifungu 1005 – *Legal Service Unit*................................Sh. 201,929,745
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*........Sh. 207,821,745
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit*……...............................................Sh. 867,361,745
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*……………….........Sh. 230,125,745
Kifungu 1009 – *Research and Training*......................Sh. 4,918,209,287
Kifungu 4001 – *Cooperative Promotion and Coordination Section*..........................Sh. 398,943,900
Kifungu 4002 – *Cooperative Microfinance Section*....Sh. 404,790,900
Kifungu 4003 – *Regional Cooperative Offices*.........Sh. 7,857,594,573
Kifungu 4004 – *Cooperate Marketing and Investment Section*..................................................Sh. 973,593,520
Kifungu 4005 – *Registration Service Section*................Sh. 305,028,720
Kifungu 4006 – *Inspection and Supervision Services Section*................................Sh. 21,879,669,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*......................................Sh. 2,000,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*..............Sh. 466,614,000,000
Kifungu 1004 – *Agriculture Training Institute*...........Sh. 40,482,900,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*.....Sh. 300,000,000
Kifungu 1009 – *Management Information System Unit*…..............Sh. 0

Kifungu 1010 – *Environmental Management Unit*…....................Sh. 0
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*.......Sh. 1,600,000,000
Kifungu 2001 – *Crop Development*........................Sh. 80,805,081,000
Kifungu 2002 – *Agricultural Mechanization*...........Sh. 19,000,000,000
Kifungu 2003 – *Agriculture Land Use Planning and Management*....................................Sh. 4,800,000,000
Kifungu 5001 – *National Food Security*.................Sh. 702,275,933,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation*....................................Sh. 907,700,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 86,304,0000
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit*.........................................................Sh. 588,900,000
Kifungu 1009 - *Environment and Social Management*.....................................Sh. 1,034,000,000
Kifungu 2001 – *Design and Research Division*........Sh. 52,000,000,000
Kifungu 2002 – *Irrigation Infrastructure Development*.................................Sh. 249,592,801,000
Kifungu 2004 – *Operations Division*.......................... Sh. 1,904,160,000
Kifungu 2005 – *Compliance and Quality Assurance*.....................................Sh. 308,721,961,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika**

Kifungu 4001 – *Cooperative Promotion and Coordination*........................................Sh. 418,305,600
Kifungu 4006 – *Inspection and Supervision Services Section*.................................................Sh. 697,176,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Kilimo Fungu Na. 43, Fungu Na. 24 na Fungu Na. 05 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naomba kwa sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa sasa nitawahoji, kwamba sasa Bunge likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, bajeti yako sasa imepita rasmi, Wabunge wameipitisha. Ahsanteni na hongera sana

Mheshimiwa Waziri. Umepewa maelekezo na Mheshimiwa Rais na umeyatekeleza, wewe, Naibu Waziri na timu yako ya Wizarani, hongereni sana. *(Makofi)*

Wanasema wazungu *"failure is not to fail; failure is not to try."* Mnaweza mkaanza mkafanya makosa, lakini mkajirekebisha mkapata maendeleo makubwa sana. Kuna nchi walitoka *from sand to silicon.* Mama Samia alitutoa *from sand to food security.* Huyo ndio Rais mwenye maono kwenye nchi hii, na huyo ndiye Rais tutakwenda naye kwenye uchaguzi mwaka 2025. Nawapongeza sana, mmefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Nawaomba, hii Benki ya Ushirika, tusianze kukopeshana sisi wenyewe kwa wenyewe, mtafanya makosa makubwa sana. Benki ya Ushirika umkopeshe Mheshimiwa Zungu, ninakuja pale na cheo changu naomba shilingi milioni 20 mnanipa, nakwenda kuzichezea. Wapeni wakulima, mnawajua. *Data* ya wakulima mnayo, nendeni mkawape.

Nawaomba, kuna mambo mengi mmeshindwa kuyajibu kutokana na muda, tafuteni muda, kaeni kwenye *media*, wewe na Naibu Waziri wako, elezeni umma mikakati ambayo Mheshimiwa Rais amewapeni na namna mtakavyokwenda kuitekeleza kwa wananchi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunayo ya kusema kwa wananchi, msiwe na unyonge wala hofu, haya siku zote tunayasema, nendeni mkaseme. Mabadiliko ya kilimo, mabadiliko ya kwenye miundombinu, mabadiliko ya afya, mabadiliko ya shule, tunayo ya kusema. Chama ambacho hakina cha kusema, kitaanza mikwara, sisi twendeni tukaseme kwa wananchi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya. nawashukuru sana. Lingine *procrastination*, neno la Kiingereza lina maana nzito sana, kutokufanya maamuzi na ku-*delay* kujadili mambo ya maslahi mapana ya Taifa letu. *File* linakuja ofisini halishughulikiwi, mtu anafanya mambo mengine. Nawaomba sana, ku-*delay* maagizo ya Serikali, maagizo ya Rais ni kosa kubwa sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.57 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa Tarehe 23 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*